Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

HUDUMA YA KUWAIMARISHA VIONGOZI WA KANISA AFRIKA MASHARIKI

MAHUBIRI YA UFAFANUZI

na Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Cornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders East Africa, Inc.
714 S. Summit St., Appleton, WI 54914
+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

December 2007; imerudiwa May 2013; imesahihishwa Julai 2014

Mahubiri ya Ufafanuzi—m.y, jinsi ya kuchambua, kuhubiri, na kutumia Biblia vizuri—huelezwa na kudhihirishwa. Umuhimu wa mhubiri mwenyewe huelezwa. Kila kipengele cha mahubiri mazuri, kuanzia utangulizi, kuja kujenga hoja na ufafanuzi wake, hadi kinavyotumika na hitimisho lake, huainishwa na kuwekwa wazi. Jinsi ya kuandaa na kupamgilia mahubiri mazuri huangaliwa, miundo mbalimbali ya kimpangilio imetolewa, na undani wa mihtasari ya mahubiri imejumuishwa pia. Nini hufanya mawasiliano yawe yenye mvuto, na mtindo wa mhubiri, imejadiliwa.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

YALIYOMO

I. Mahubiri Ya Ufafanuzi—Utanguliz……3
- **A.** ***Mahubiri ya ufafanuzi yaelezwa*** **..... 3**
- **B.** ***Sababu na manufaa ya mahubiri ya ufafanuzi*** **..... 4**
- **C.** ***Mahubiri ya ufafanuzi yanavyotofautiana na ya kichwa cha somo*** **..... 5**

II. Kuhubiri Kupitia Vitabu vya Biblia……6
- **A.** ***Desturi nyingi hutoa jumbe zao zinazopatikana kwenye mwongozo*** **..... 6**
- **B.** ***Kuelezea vifungu visivyoungana juma hadi juma huacha kando mada ya vifungu hivyo*** **..... 6**
- **C.** ***Njia mojawapo ya mahubiri ya ufafanuzi ni kuhubiri kupitia vitabu vya Biblia*** **.....6**
- **D.** ***Ziko sababu na manufaa kadhaa ya kuhubiri kufuatia vitabu*****..... 6**

III. Maisha ya Mhubiri..... 7
- **A.** ***Wale wanaolitangaza na kulihubiri Neno la Mungu wameitiwa kuishi maisha matakatifu*** **..... 7**
- **B.** ***Kazi ya Roho Mtakatifu katika mahubiri ya ufafanuzi huhitaji wahubiri waishi Maisha matakatifu*** **……8**
- **C.** ***Kuishi kuendana na unachohubiri, ukiwa na uhusiano sahihi na Mungu na watu wengine, husaidia kwa kiwango kikubwa kuvutia kile unachokisema*****.....9**

IV. Kujali Dhana na Uelewa wa Wasikilizaji……10
- **A.** ***Kujali*** **dhana……10**
- **B.** ***Ingawaje njia za kuwasilisha hoja zilitofautiana kulingana na aina za watu waliohudumiwa na kusudi lililokuwepo, Yesu na wahubiri wengine na walimu wa Kibiblia mara zote walitumia "tatizo (au tukio)-linaloendana" kama mbinu ya kuhubiri na kufundishia*****.....10**
- **C.** ***Mahubiri yetu yafuate mfano wa Yesu na Paulo*****..... 11**
- **D.** ***Uelewa wa watu na matokeo ya mbinu ya kutumia matatizo (tukio) kama "Uzio wa reli"*****.....13**

V. Mambo ya Kuzingztia Kuhusiana na Kifungu cha Biblia Unachokielezea……14
- **A.** ***Lengo la*** **kifungu……..15**
- **B.** ***Kuelezea na kutolea mfano kifungu*****.....16**

VI. Kutumika Kwake……17
- **A.** ***Mabadiliko ya maisha ndiyo lengo la mahubiri ya ufafanuzi*****..... 17**
- **B.** ***Katika Biblia nzima, kweli za mafundisho huambatana na matumizi ya utendaji wake ambapo huthibitisha kile kweli inavyotakiwa kuonekana na jinsi kweli ile inatakiwa iwekwe katika maisha*****.....17**
- **C.** ***Matumizi huletea ufafanuzi maana*** **..... 17**
- **D.** ***Matumizi kimatendo kwaweza kuwa ni mabadiliko katika mtazamo pamoja na mabadiliko katika tabia*** **..... 18**
- **E.** ***Wahubiri wasidhanie tu kuwa kule kueleza au kuonyesha kile Biblia inachosema na maana yake, watu wataona mara moja jinsi ya kutumia kweli za Kibiblia maishani mwao*** **.....18**
- **F.** ***Ili kuhakikisha kutumika kwake kunalengwa zingatia maswali mawili ya muhimu sana*****..... 18**

VII. Sifa na Mpangilio wa Jumbe Zenye Ufanisi……20
- **A.** ***Ili kuwa na ufanisi zaidi, ujumbe unapaswa uwe na hoja moja, inayobeba ujumbe wote*****..... 20**
- **B.** ***Mawasiliano yenye kushawishi hurahisishwa na mpangilio ulio wazi*****..... 21**
- **C.** ***Vipengele vitatu vya ujumbe mara nyingi husahauliwa, lakini ni vya muhimu kuleta ufanisi wa mfundisho yako: Utangulizi; Mchakato wa mabadiliko; na Hitimisho*** **..... 22**
- **D.** ***Mambo ya kuzingatia katika mpangilio kwa*** **ujumla……..23**
- **E.** ***Miundo mbali mbali ya*** **mipangilio……..25**

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

VIII. <u>Mawasiliano Yenye Mvuto na "Mtindo" wa Mhubiri</u>……..26
A. ***Hakuna mtindo wowote ulio sahihi wa kuhubiri.*** **..... .26**
B. ***Tabia au mtindo wa kuhubiri utatofautiana kulingana na mada na lengo la ujumbe husika, mazingira tunayohubiria, na uelewa na mahitaji ya wasikilizaji*****……..27**
C. ***Kanuni za hotuba za hadhara zenye mvuto hufaa pia kwa mahubiri na kwa Hutuba nyingine za hadhara*****……28**
D. ***"Upako" wa mhubiri hauna uhusiano na misisimko*****……..29**

NUKUU ZILIZONUKULIWA..... 30

DIBAJI A— MASOMO YA BIBLIA YA KINA KWA MAHUBIRI 31

DIBAJI B— HATUA ZA UJUMBE: VIDOKEZO VICHACHE KABISA KWA WAHUBIRI 33

DIBAJI C—Math 6:19-24—Muundo wa Fundisho wa Dondoo za Ujumbe 40

DIBAJI D—Waef 2:11-16— Muundo wa Fundisho wa Dondoo za Ujumbe 42

DIBAJI E—Kut 1:1-22—Muundo Elekezi wa Dondoo za Ujumbe wa MKM 44

DIBAJI F—Ufu 19:11-21— Muundo Elekezi wa Dondoo za Ujumbe wa MKM 47

DIBAJI G—Zab 73:1-28— Dondoo za Ujumbe wa Muundo Simulizi wa kisa.....49

DIBAJI H—Ufu 19:11-2— Dondoo za Ujumbe wa Muundo Simulizi wa kisa 52

DIBAJI I—1 Sam 30:1-31—Dondoo za Ujumbe za Muundo wa Mimi-Sisi-Mungu-Wewe-Sisi 53

DIBAJI J—MAHUBIRI YENYE UWEZEKANO MKUBWA WA KUFANIKIWA..... 55

DIBAJI K—JE UNAPOTEZA MUDA WAKO WA MAANDALIZI YA MAHUBIRI?.....57

DIBAJI L—FUMBUZI-ZISIO-RAHISI SANA ZA MAHUBIRI 58

MWANDISHI 60

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

MAHUBIRI YA UFAFANUZI

I. Mahubiri Ya Ufafanuzi—Utangulizi

A. *Mahubiri ya ufafanuzi yaelezwa*

1. Ingawaje Biblia iliandikwa miaka Maelfu yaliyopita, Roho Mtakatifu huongea nasi kupitia Maandiko, na hufanya maneno ya Maandiko kuwa hai na yenye kuendana nasi leo.

a. *Vifungu kadhaa hutumia vitenzi vya wakati wa sasa kwa Maandiko, kuonyesha kwamba Roho bado yuko katika kunena nasi kupitia Biblia leo (**Waeb 3:7; 4:7; 10:15-17; 12:5-6**).* Hata matukio ya Agano la Kale yalitokea kama mifano kwa ajili yetu, yakaandikwa yawe maelekezo kwetu, na watu waliohusika katika matukio hayo bado wanena kwetu (**1 Wakor 10:6, 11; Waeb 11:4**). Mitume na waandishi wa Biblia mara nyingi hutumia vitenzi vyote viwili; vya wakati uliopita na wakati uliopo wanapotaja Maandiko, kuonyesha kwamba kile kilichoandikwa kale bado "ni Neno linaloishi kwa ajili ya watu walio hai, kutoka kwa Mungu anayeishi" (Stott 1982: 100). John Stott anaelezea umuhimu wa hili: "Wakati tunapopokea ukweli kuwa Mungu "Bado anena kupitia kile alichokwisha kukinena," tutakuwa tumejilinda kikamilifu kutoka makosa mawili yaliyo kinyume. La kwanza ni kuamini kuwa, ingawaje ilisikika nyakati za kale, sauti ya Mungu iko kimya siku hizi. La pili ni kuwa Mungu hakika bado aongea leo, bali Neno lake halina uhusiano, au linahusika kidogo sana na Maandiko. . . Usalama na kweli huwepo katika kuwa na uhakika kwamba Mungu amenena, Mungu hunena, na kwamba jumbe zake hizo mbili zinahusiana kiukaribu sana kati yao, kwa sababu *ni kupitia* kile alichokinena ndicho anachokinena." (Ibid.: 102)

b. *Vifungu vingine vinaonyesha kwamba, wakati Roho Mtakatifu anaponena kupitia mtu anayeihubiri Biblia kiusahihi, NDILO Neno la Mungu (**Mdo 4:31; 6:4; 11:14; Warum 10:17; Wafil 1:14; 1 Wathes 2:13; Waeb 13:7; 1 Petr 1:22-25; 4:11**).* Kwa hiyo, pale mhubiri anapolifanya lile analotakiwa kulifanya, mhubiri huyo, Roho, na Neno huunganika kikamilifu katika shughuli hai, muhimu, isiyo ya kawaida.

2. Mahubiri ya Ufafanuzi hutokana na kweli hizo ziliotajwa.

a. *Vipengele vya mahubiri ya ufafanuzi ni:*

(1) Mahubiri ya ufafanuzi huwa na msingi, na maelezo kutoka katika kifungu cha Biblia;

(2) Mahubiri ya ufafanuzi yanajiaminisha kwa msisitizo, mafundisho, kazi ya kifungu husika, na kusudio la mwandishi aliyekiandika.

(3) Mahubiri ya ufafanuzi hukitumia kifungu kwenye maisha ya wasikilizaji wake.

b. *Mahubiri ya ufafanuzi yafafanuliwa.* Mahubiri ya ufafanuzi yanaweza yakafafanuliwa kama, "kufungua andiko lenye uvuvio kwa uaminifu na umakini mkubwa kiasi kwamba sauti ya Mungu inasikika na watu wa Mungu humtii yeye." Bryan Chapell anaongeza, "Ili kuweza kuelezea kifungu, mhubiri lazima aeleze, akijenga ile maana, na kuonyesha matokeo katika namna ambayo kundi husika maalum la wasikilizaji litaona inavutia, inaeleweka, na inaweza kufanyiwa kazi" (Chapell 1994: 127).

3. Msemo "ufafanuzi" unaonyesha "kuanika wazi" kile kisemwacho na Biblia, maana yake, na kuhusu nini; ndio moyo wa mahubiri. Mkondo huo ulianzishwa na makuhani katika Nehemia, ambaye "alisoma kutoka kitabuni, kutoka Sheria za Mungu, ambacho kilitafsiri [au "kueleza"] kwa maelezo ambayo yalieleweka wakati wa kusomwa" (**Neh 8:8**). Stott anaelezea hili: "Kule kufafanua maandiko, ni kuletesha kile kilichoko katika andiko lile, na kukianika kionekane. Mfafanuzi, hufunua kile ambacho kilikuwa kimefunikwa, na kuweka bayana ambacho kimefichika, kufungua ambacho kimejifunga, na kulainisha kile ambacho kilikuwa kimebanwa mno. Kinyume cha ufafanuzi, ni "Kulazimisha," ambako ni kuweka kitu katika andiko ambacho hakiko hapo. Lakini hiyo "dhana" inayohusika yaweza kuwa ni mstari, au ni sentensi, au hata ni neno moja tu. Yawezekana pia kuwa ni kifungu kabisa, au ni sura, au kitabu kizima. Ukubwa wa dhana haujalishi, ili mradi ni wa Ki-Biblia. Kinachojalisha ni kile tunachofanya nayo. Andishi liwe ni refu au fupi, jukumu letu kama wafafanuaji, ni kulifungua kwa namna ambayo linanena ujumbe wake wazi wazi, vizuri, kiusahihi, na kuleta maana, pasipo kuongeza, kupunguza au kukosesha. Katika mahubiri ya ufafanuzi, hiyo dhana ya andishi la Ki-Biblia huwa si utangulizi wa ujumbe wenye malengo mengi, mapana tofauti; wala si msumari ukutani wa kuninginizia mfuko wa kuwekea mawazo mbali mbali, bali ndio kiongozi atamkaye na kutawala kile kisemwacho." (Stott 1982: 125-26)

4. Mahubiri ya ufafanuzi hushughulikia vipengele vilivyoandikwa. Mchungaji Mark Harris anaeleza, "Dhana ya andishi yaweza kuwa ni wazo, ulizo, au simulizi fulani. Yaweza kuwa mstari moja, kifungu, au sura kadhaa. Katika kila andishi, wazo kuu muja kikawaida hutawala, na mengine yanayozungukia hutia nguvu hilo. Hili ni "wazo kuu" (Harris 2004: 22) Chapell naye anaita sehemu ya andiko inayohubiriwa kuwa "sehemu

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

inayofafanuliwa," ambayo anaitafsiri kama "sehemu kubwa au ndogo ya andiko ambayo mhubiri anaweza kuonyesha ukweli moja wa kiroho, kwa hoja za kutosha zinazounga mkono, au mada zinazopatikana kutokana na uwigo wa andishi hilo" (Chapell 1994: 53). Kuliangalia Andiko kama kipengele cha andishi, au cha ufafanuzi kunawachochea wahubiri kutazama vifungu vya maandiko kama "mkusanyiko wa vipakiti vya fikira zilizoungana, badala ya kuona kama ni vitawi vya mawazo ya mistari isiyoungana." (Ibid.: 52).

5. Mahubiri ya ufafanuzi ni zaidi ya kuhubiri peke yake. Mhubiri anakabiliwa na kazi ya kujifunza, kuelewa, na kuitafsiri vizuri Biblia. Mahubiri ya ufafanuzi kisha huchukua hatua inayofuata ya kupeleka habari iliyopatikana hapo kwa watu ambao *hawakujifunza hii* kwa jinsi ambayo wataielewa *kama kwamba wao wenyewe ndio waliokwenda kujifunza.* Lakini mahubiri ya ufafanuzi hufanya kitu cha zaidiChuleta kweli ya Biblia katika namna ambayo wasikilizaji watavuviwa *kubadili maisha yao* kama matokeo ya kile walichojifunza kutoka kwa mhubiri. John Piper anaeleza hili: "Wakati Paulo anamwambia Timotheo katika 2 Timotheo 4:2, 'Lihubiri Neno,' neno analolitumia kwa 'hubiri' ni neno la 'julisha' au 'tangaza' au 'Pasha habari' (*keruxon*). Si neno la 'kufundisha' au 'elezea.' . . . Mimi huita huku kujulisha *kuletesha furaha kuu.* Kuhubiri ni kuletesha furaha kuu kwa watu kuhusu kweli iletwayo. Siyo isiyovutia, au iliyopooza, au isiyo na upande wowote. Siyo simulizi tu. Ni ya kiudhihirisho na yenye shauku ya kuambukiza kile inachokisema.

Hata hivyo, kupasha habari huku ndani yake kuna kufundisha. Waweza kuliona hilo unaporudi na kuangalia 2 Timotheo 3:16- Andiko (ambalo huzaa mahubiri) lafaa kwa *mafundisho.* Na unaweza kuona hilo unapotazama mbele sehemu iliyobakia ya 2 Timotheo 4:2, 'Lihubiri neno . . . karipia, kemea, na kuonya, kwa uvumilivu wote na mafundisho.' Kwa hiyo kuhubiri ni ufafanuzi. Hushughulika na Neno la Mungu. Mahubiri ya kweli si maoni ya mtu tu. Ni ufafanuzi wa uaminifu wa Neno la Mungu. Kwa hiyo uko msemo, kuhubiri ni *ufafanuzi wa kuletesha furaha kuu."* (Piper 2004: 10-11)

6. Mahubiri ya ufafanuzi lazima yahusishe siyo tu akili, lakini pia moyo na maisha ya mhubiri. Sababu ni kuwa Roho Mtakatifu *kwanza* hulifanyisha kazi andiko *kwa mhubiri* na baadaye, kumpitia yeye, hulitumia kwa watu. Ili kuhubiri ufafanuzi, mchungaji anawajibika kujifunza kikamilifu kuhusiana na andishi, ambalo litashibisha nafsi yake mwenyewe, likamtia nguvu yeye, nalo likamfanya mchungaji bora zaidi na mtu mzuri zaidi. Mkondo huo ulianzishwa na Ezra ambaye "alikuwa ameuelekeza moyo wake kuitafuta sheria ya BWANA, na kuitenda, na kufundisha maagizo na hukumu katika Israeli" (**Ezra 7:10**). "Jifunze-Litende-Lifundishe" unapaswa uwe bado ni mkondo kwa wahubiri leo.

7. Mahubiri ya ufafanuzi pia lazima yahamasishe akili, moyo, na maisha ya washirika. Piper anasema, "Kwenye kuabudu kwa kweli siku zote kuna *kuelewa* kwa akili na siku zote kuna *kijisikia* kwa moyo. Kuelewa siku zote lazima kuwe ndiyo msingi wa hisia,au la yote tutakayokuwa nayo ni hisia za misukumo isiyo na msingi. Lakini ufahamu wa Mungu ambao hauleteshi hisia za ki-Mungu huwa ni za kiakili tu na ufu" (Piper 2004: 10).

8. *Kusudi* au *lengo* la Mahubiri ya ufafanuzi *siyo* tu ni kuwafundisha watu kile Biblia inachosema na kumaanisha; bali ni *kubadilisha maisha.* Kama mchungaji Andy Stanley anavyosema; lengo ni "kuwafundisha watu kuishi maisha yanayoakisi thamani, kanuni, na kweli za Biblia" (Stanley and Jones 2006: 95). Mabadiliko ya *maisha* yetu (siyo tu mawazo yetu au imani zetu) yako katika moyo wa kile ambacho ndicho Ukristo unachomaanisha (ona **Warum 8:29; 12:1-2; Waef 4:17-24; 5:8**). Yakobo aliliweka hili wazi aliposema "imani pasipo matendo haizai" (**Yak 2:20**), na "lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya wenyewe" (**Yak 1:22**). Yesu alitoa ishara moja itakayowafanya watu wajue kwamba tu wanafunzi wake: "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (**Yohn 13:35**). Hatimaye, hilo ndilo lilikuwa lengo la maagizo ya Paulo: "Walakini mwisho wa agizo hili ni upendo utokao katika moyo safi, na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki" (**1 Tim 1:5**). Ona jinsi lengo la upendo linavyoathiri *maisha yote ya mtu:* moyo unasafika; dhamiri inafanywa kuwa njema (kwa sababu hakuna tena tofauti kati ya yale asemayo mtu na yale ayafanyayo); na imani ya mtu inakuwa haina unafiki (imani inaambatana na matendo ya ki-Mungu ili kwamba imani isiwe katika kutokufaa tena).

9. Kwa vile lengo la Mahubiri ya ufafanuzi ni mabadiliko ya maisha, *matumizi ya neon—KWA maisha ya wasikilizaji, na NDANI yamaisha YA wasikilizajiCndiyo kiini.* Neno la Mungu siku zote huhitaji mwitikio: "Wakati unapojizatiti kuhubiri ili kuleta badiliko la maisha, matayarisho yako hayakamiliki mpaka uwe umejibu maswali muhimu mawili: Ili nini basi? na Sasa nini? Mahubiri yetu hayawezi kuleta tofauti kubwa kama watu wetu hawajui tofauti gani inatakiwa kuletwa Ufunguo kwa mkabala huu ni kukataa kusimama kuhutubu mpaka ujue majibu ya hayo maswali mawili: Ni kitu gani kimoja ninachotaka wasikilizaji wangu wajue? [na] Nataka watu wafanye nini na hicho kitu?" (Stanley and Jones 2006: 97, 104)

B. ***Sababu na manufaa ya mahubiri ya ufafanuzi***

1. Ufafanuzi "huandaa mipaka" kwa maana kwamba: hutudhibiti katika kuelezea mada ya kimandiko. Mhubiri huwa na uelekeo mdogo zaidi wa kujaribiwa kufundisha "wazo lake" ama mapendekezo yake. Pia anakuwa

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

katika usalama wa kumudu mkandamizo wa washirika kumlazimisha ahubiri kile tu ambacho "wanakitaka kukisikia." Huo *mpaka* wa nini kihubiriwe ndio *humweka huru* mchungaji kuhubiri shauri lote la Mungu katika namna ambayo inasaidia kuhakikisha yote mawili: *unyofu* (uhuru kutokana na kujaribiwa na mkandamizo wa maswala ya kuyahubiri) na pia ana *uwiano* (m.y., uwiano kati ya sehemu tofauti za Biblia, na uwiano ndani ya kitabu chenyewe) katika mahubiri yake.

2. Ufafanuzi ulio safi humhitaji mwelezaji asigeuze Andiko. Mhubiri wa ufafanuzi lazima awe na unyofu wa kuweza kutambua kile waandishi wa Biblia walikimaanisha, na kukisema. Mhubiri wa kifafanuzi lazima "akae kwa unyenyekevu chini ya mamlaka ya Maandiko, badala ya kusimama kwa hukumu juu yake" (Stott 1982: 127-30). Kusema ukweli, ikiwa *hufanyi mahubiri* kwa mtindo wa ufafanuzi *unamwakilisha visivyo* kwa sababu, "unasema kwa jina la Mungu kile ambacho Mungu hakukisema: unatoa ahadi ambazo yeye hakuzitoa; unatoa ushauri ambao yeye hakuutoa; na unatangaza kile ambacho yeye hakukitangaza. Kwa kifupi, unaagiza [wasikilizaji wako] katika mtazamo wa kimakosa wa Mungu. Kwa kufanya hivyo, unakuwa mwalimu wa uongo na kujiweka mwenyewe chini ya hukumu ya Mungu." (Harris 2004: 26)

3. Neno linawapa wahubiri mamlaka yao halisi. "Mamlaka ya Neno hutuwezesha kusema mambo yanayotia changamoto kuliko yote kwa mtu yeyote pasipo kuomba msamaha, lakini mamlaka hiyo hiyo hututaka tunene kwa upole pasipo kulazimisha." (Chapell 1994: 89). Vivyo hivyo, kuanika wazi kunatupa ujasiri kuhubiri kwa sababu hatuelezi maoni yetu tu au yale ya kuweza kukosesha ya watu wengine. Badala yake, "Twalinena Neno la Mungu kwa unyofu na uaminifu"; kwa hiyo, "tunaweza kuwa na ujasiri mkubwa" (Stott 1982: 132). Kusema ukweli, utafiti wa watu 263 wa kawaida katika makusanyiko 28 tofauti (9 ya Wamarekani Weusi; 16 yasiyo ya Kihispania, ya asili ya Ulaya; na 3 ya mchanganyiko wa rangi tofauti kutoka madhehebu 13 ya Magharibi ya kati Amerika ya Christian Theological Seminary [utafiti wa CTS] ilionyesha kwamba, "kwa uwingi kabisa, kitu kimoja kilichotajwa zaidi kuhusika na mamlaka ya mahubiri kuliko kingine, ni jinsi mhubiri anavyoitumia Biblia," hasa itokeapo mhubiri anakuwa amejifunza kikamilifu na kuwa haneni maoni yake tu mwenyewe (Allen 2006: 65, 67-68). Utafiti huo ulithibitishwa na utafiti mwingine wa wahubiri 102 na wasikilizaji 479 kutoka sehemu mbali mbali za Marekani, uliopatikana kutoka makundi ya umri, madhehebu, sehemu, na makabila tofauti [Utafiti wa GASS], uliogundua, "Moja ya sifa inayopatikana kikawaida kwenya mahubiri mazuri, kulingana na wasikilizaji waliofanyiwa utafiti, ilikuwa kwamba inapaswa iwe 'na msingi wa Maandiko'; sifa ya msingi ya mahubiri mabaya ilikuwa ni uhusiano usioeleweka kati ya Kifungu cha Andiko na hoja muhimu ya (za) mahubiri" (Carrell 2000: 27).

4. Mahubiri ya Ufafanuzi huwakilisha na hutumia *nguvu* ya Neno, na *mamlaka* ya Neno, ambalo ni kazi ya Roho Mtakatifu (**Isa 55:10-11; Yer 23:29; Mdo 18:28; Waef 4:17; 1 Wathes 2:13; Waeb 4:12; Yak 1:18; 1 Petr 1:23**). Mchungaji anaweza akatarajia kwa ujasiri kuona mabadiliko ya kiroho yakitokea kwenye kusanyiko lake kama matokeo ya mahubiri yake, kwa sababu "tunapotangaza Neno, tunaleta kazi ya Roho Mtakatifu kuzaa katika maisha ya watu wengine. Hakuna kweli inayotuhakikishia matumaini makubwa zaidi katika mahubiri yetu na kutupatia sababu zaidi za kutegemea matokeo kutokana na juhudi zetu." (Chapell 1994: 24)

C. ***Mahubiri ya ufafanuzi yanavyotofautiana na ya kichwa cha somo***

1. Ujumbe wa somo ni mahubiri kuhusu masomo yaliyochaguliwa na mhubiri au wengine. Mara nyingi jumbe za kuteua masomo sio za ufafanuzi. Mhubiri huchagua vichwa na kisha huvipanua kulingana na mawazo yake mwenyewe, siyo kulingana na asemacho Mungu katika biblia. Mistari michache "ya kuthibitisha" kutoka kwenye Biblia huweza kutajwa; lakini katika mahubiri ya aina hiyo malengo au hoja kuu huwa "zimepangiliwa kulingana na somo hilo badala ya kulingana na matakwa ya andiko", na "jinsi hoja kuu za [mahubiri] zilivyojengwa , hutokana na vyanzo nje ya andiko lililosomwa" (Chapell 1994:127-28).

2. Jumbe za somo zaweza kuwa za ufafanuzi. Katika "Somo la Ki-Ufafanuzi," kule kuhubiri "ujumbe huanzia na lengo, mafundisho yake, dhambi, hitaji linalosumbua, nk., na kisha huenda kwenye Andiko kuona nini Mungu anasema kuhusu somo husika" (Harris 2004: 30). Kwa mfano, katika kuhubiri kuhusiana na utoaji mimba, itakubidi kuangalia mistari kutoka vifungu mbali mbali katika Biblia kwa vile hakuna kifungu rasmi kinachoshughulikia kipekee swala hilo. Yule ahubiriye ujumbe kwa Ki-Ufafanuzi bado lazima azingatie kuelezea kile Biblia inasema au inataka kuhusiana na jambo hilo; Biblia inatakiwa iwe ndiyo msingi wake wa kuzingatiwa na mamlaka yake; na mhubiri atakuwa "anawajibika kutoutumia mstari nje ya maana yake iliyokusudiwa awali" (Ibid.). Somo kwa Ki-Ufafanuzi linaweza pia kuwa ni kifungu kimoja kutoka kwenye Biblia kama ndiyo "Nanga" ya msingi kwa ujumbe, na kisha ukatumia vifungu vingine kuelezea zaidi kiufasaha ule mtazamo ambao Biblia inasema kuhusiana na somo husika. Tofauti kati ya "Somo kwa Ki-Ufafanuzi" na "Ufafanuzi wa dhana ya andishi" ni kwamba katika ufafanuzi wa dhana ya andishi, mhubiri *"huanzia na andishi na* na *kuliacha lijipangie* 'wazo kuu' la ujumbe. Mkazo kwa ufafanuzi na tafsiri ya

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

maandiko ndiyo utakaoongoza mwelekeo wa ujumbe." (Ibid., msisitizo umeongezwa)

3. Somo kwa Ki-Ufafanuzi bila shaka una nafasi yake:

a. Husaidia kutoa pumziko kati ya (au hata ndani ya) mfululizo wa jumbe kuhusiana na kitabu kimoja au hoja kuu fulani, ili watu waweze kusikia vitu vingine.

b. Kushughulikia maswala maalum ambayo hujitokeza katika maisha ya washirika au katika desturi ambayo yanahiyajika kuwekwa sawa wakati fulani.

c. Huweza kushughulikia maswala yanayojitokeza kulingana na kalenda (n.k., Krismasi, Pasaka, sikukuu muhimu ya taifa) ambayo inatakiwa kufafanuliwa.

d. *Somo kwa Ki-Ufafanuzi huweza yenyewe kutokezesha mfululizo wa jumbe zenye msingi wa hoja ya Ki-Biblia (n.k., "uwakili" au "tabia za Mungu").* Katika hali kama hiyo, mhubiri huweza kuchagua kuelezea kifungu fulani cha Maandiko, kila kimoja kikiendana na hoja ya mfululizo wa jumbe husika hata kama zote zinatokea vitabu tofauti vya Biblia. Bila shaka, mhubiri anaweza kuamua kufanya mfululizo huo kulingana na somo kuu *ndani ya kitabu* (k.m, "Utukufu wa Mungu" kutoka Isaya)—kwa hapo, kitabu hicho bado ndicho kitaweka agenda, lakini si kila kifungu katika kila kitabu kitaelezwa.

II. Kuhubiri Kupitia Vitabu vya Biblia

A. *Desturi nyingi hutoa jumbe zao kutoka vifungu vipatikanavyo katika mwongozo*

Mwongozo ni vifungu vilivyoandaliwa kwa mzunguko wa miaka mitatu, huwa ni vifungu vilivyochukuliwa kutoka Agano la Kale, Zaburi, injili, na Nyaraka, kwa kila juma la mwaka. Mwongozo una faida kwamba una vifungu ambavyo tayari vimeshachaguliwa, na mchungaji anajua tangu mapema ni kifungu gani atakuwa anakihubiri. Zaidi ya hapo, vifungu huwa vinajitosheleza kimaelezo, kwa hiyo kwa kipindi cha miaka kumi na mbili, sehemu kubwa ya Biblia inaweza kuwa imekamilika kufundishwa. Katika kuandaa miongozo, juhudi huwekwa kuunganisha vifungu vya Biblia kwa kalenda ya kila juma la kanisa. Ingawaje inawezekana kuhubiri Somo kwa Ki-Ufafanuzi kutoka vifungu vinavyotokana na miongozo hiyo, juma-kwa juma vifungu hivyo, kwa kiwango kikubwa, vimejitenga mbali na vingine.

B. *Kuelezea vifungu visivyoungana kutoka juma hadi juma huweka kando dhana ya vifungu hivyo*

Hasara kuu ya kuelezea mistari isiyoungana au vifungu tu kila juma, hata kama vifungu hivyo vimechaguliwa kutoka katika miongozo, ni kwamba, huweka kando *dhana* iliyoko kwenye mistari au kifungu husika. Hilo huzuia wasikilizaji kuona muunganiko kati ya vifungu vinavyoelezwa, na vifungu vingine kabla na baada yake; ambavyo vingeelezwa kama mhubiri angekuwa anahubiri kitabu kizima. Matokeo yake, washirika hawataweza kupokea lengo kuu la *kitabu* ambacho mstari huo unapatikana.

C. *Njia mojawapo ya mahubiri ya ufafanuzi ni kuhubiri kupitia vitabu vya Biblia*

Mahubiri ya ufafanuzi kimsingi yatakuwa ni *mfululizo* wa jumbe kuhusu kitabu fulani cha Biblia. Hilo ni kwa vile vitabu vingi vya Biblia ni virefu mno kuweza kuelezewa katika kipindi kimoja. Vitabu *si lazima* vifundishwe kwa mpangilio kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Vitabu virefu kikawaida vifuatiwe na vitabu vifupi, au vitabu vya mwandishi moja vifuatiwe na vya mwandishi mwingine, au vitabu vya Agano Jipya vikatengwa kati na vitabu vya Agano la Kale, au mfululizo wa vitabu unaweza ukaingiliwa au kubadilishwa na ujumbe wa somo fulani ili kuleta utofauti. Hata kama hauhubiri mfululizo wa masomo kutoka katika kitabu chote, waweza kufikiria mfululizo wa masomo kutoka mafundisho *muhimu* ya vitabu (k.m., masomo kutokana na maisha ya Yusufu [**Mwanzo 37, 39-50**] au masomo kutokana na Mafundisho ya Mlimani [**Mathayo 5-7**]). Mfululizo kama huo, huleta manufaa sawa na kuhubiri kuhusu kitabu kizima (ona chini).

D. *Ziko sababu na manufaa kadhaa ya kuhubiri kufuatia vitabu*

1. Katika kutupatia Biblia, Mungu hakuamua kutupatia Neno lake katika hali ya mistari iliyotengana, lakini katika hali ya vitabu. Katika vitabu hivyo, mistari yote hufanya kazi pamoja kujenga hoja zinazoendana pamoja na mikondo ya mawazo. Matokeo yake, "kitabu [chote] ni kikubwa zaidi ya jumla ya vipande vyake [mistari na vifungu]." Katika kuhubiri kufuatana na vitabu vya Biblia, mhubiri anaweka mkazo kisahihi kwenye Neno la Mungu, anaheshimu sura ya Andiko lenyewe, na kutusaidia kufikiri kwa hali ya upana zaidi wa Maandiko kuliko mistari binafsi tu.

2. Kuhubiri jumbe za ufafanuzi kupitia vitabu vya Biblia huunda ufahamu ambao ni mpanaC na wa kinaCwa Neno la Mungu kwa pande zote; kwa mhubiri na kwa ushirika. Mhubiri anavyohubiri kupitia kitabu, jumbe zinazoelezea vifungu vilivyo kabla na mbele ya kifungu kinachohusika zinaweza kutaja mambo yaliyopo

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kwenye kifungu husika, hivyo kuimarisha dhana yote kwa njia ya, na kwa uelewa wa, mwelekeo wa kifungu husika.

3. Mahubiri ya ufafanuzi hufuata mfano na mkondo uliotumiwa katika Agano la Kale, na Kristo, na Mitume kwenye Agano Jipya. Ezra alifafanua Maandiko katika Agano la Kale (**Neh 8:5-8**). Yesu alielezea kile kilichonenwa na Maandiko yote kumhusu yeye (**Luka 24:27, 32**). Hao wote; Yesu, Paulo, na Apolo, walisoma, wakaelezea, na kisha kuweka wazi matokeo au mahimizo yaliyoko kwenye Maandiko (ona **Luka 4:14-27; Mdo 17:1-4; 18:4-5, 24-28; 1 Tim 4:13; 2 Tim 4:2**).

4. Hao washirika wana uwezekano wa kuelewa andiko la leo kuhusiana na jumbe nyingine zilizohubiriwa karibuni. Kwa hiyo, mhubiri hatahitaji kutumia muda mwingi katika kutambulisha dhana ya kila ujumbe.

5. Uelewa wa watu utakua kiurahisi. Kwa vile huhitajika zaidi ya mahubiri mamoja kuwafanya watu "kupata hoja husika," matumizi ya asilia ya kurudia ambayo huandamana na kuhubiri kwa kupitia kitabu, husaidia kufanya imara zaidi hoja kuu zinazolengwa na vitabu hivyo. Ujumbe moja utaimarisha nyingine.

6. Maandalizi ya mhubiri hurahisishwa. Kwa kule kuzingatia kuhubiri kupitia vitabu vya Biblia, mchungaji hatahitaji kuwa na shauku ya kwenda pembeni (au kuwajibika kupoteza muda kujaribu kudhania) nini cha kuhubiri kila juma.

7. Watu watajua jinsi ya kutafsiri Biblia kwa ajili yao wenyewe. Zaidi ya kujifunza ile mada ya Neno la Mungu, ushirika utajifunza juma baada ya juma jinsi ya kutafsiri Maandiko, kwa dhana yake, kwa ajili yao wenyewe.

8. Mahubiri ya Ufafanuzi huwezesha kiurahisi usharika kushiriki kwenye jumbe. Maswali yanaweza yakatolewa juma moja kabla kuweza kusaidia kusanyiko hilo kuingia katika dhana ya andishi na kulifikiria hilo, vikundi vidogo vidogo vya majadiliano vinaweza kuandaliwa kwa washirika wa kusanyiko kujadili na kujifunza kitabu wenyewe, na huku ujumbe huo ukitoa rasilimali nzuri.

9. Maswala magumu yanaweza kushughulikiwa kwa njia ya kawaida. Kwa kuhubiri kupitia vitabu vizima, mhubiri anaweza yote mawili: *kulazimika* na *kuwezeshwa* kujifunza na kuhubiri "shauri lote la Mungu." Watu wataona kwamba mchungaji anashughulika na hoja zinazogusa kwa vile kiasilia tu amekuja kwenye somo hilo katika kitabu anachokielezea. Matokeo yake, watu hawatashangaa "kwa nini mchungaji anaongelea hili?" Au "Hivi mchungaji anamlenga nani katika ujumbe wake?"

10. Kuhubiri kwa kufuatia vitabu vya Biblia husaidia kuhakikisha kwamba mahitaji ya msingi ya ushirika yatakidhiwa. "Maandiko yote ni ufunuo wa ukombozi uliovuviwa kuielenga hali ya kuanguka ya mwanadamu (au kutokukamilika kwake)" (Chapell 1994: 270-71). Kuhubiri kwa kupitia vitabu kunamaanisha kwamba, Biblia itawekwa wazi kwa ushirika kwa jinsi ya ufahamu zaidi. Kama *Westminster Confession of Faith,* sura ya 1, kipengele 6, kinavyoliweka: "Shauri lote la Mungu kuhusiana na mambo yote ya lazima kwa ajili ya utukufu wake mwenyewe, wokovu wa mwanadamu, imani na uzima, huwa ama yameelezwa wazi katika Maandiko, au kwa matokeo mazuri na ya lazima yaweza kutolewa kutoka kwenye Maandiko ambayo hakuna chochote wakati wowote ule kinatakiwa kiongezwe, iwe kwa mafunuo mapya ya Roho, au tafsiri za wanadamu."

III. Maisha ya Mhubiri

Yeyote aliye mhubiri au kiongozi kwenye kanisa la kikristo anawajibika kuishi maisha yanayomtukuza Kristo (ona **1 Tim 3:1-7; Tito 1:5-9**). Hilo ni kweli zaidi kwa wale wanaowania kufundisha Maandiko, kwa sababu Mungu mwenyewe hulitukuza Neno lake (**Zab 138:2**).

A. *Wale wanaolitangaza na kuhubiri Neno la Mungu wameitiwa kuishi maisha matakatifu*

1. Watumishi wa Mungu wameitiwa kuishi maisha ya utakatifu, na utiifu kwa Bwana. **Yohn 14:21—**"Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye." **Warum 6:19—**"vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki, mpate kutakaswa." **2 Wakor 1:12—**"Kwa maana kujisifu kwetu ni huku, ushuhuda wa dhamiri yetu,ya kwamba kwa utakatifu, na weupe wa moyo utokao kwa Mungu; si kwa hekima ya mwili, bali kwa neema ya Mungu; tulienenda katika dunia, na hasa kwenu ninyi." **2 Tim 2:15**—"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli." **Waeb 13:7**—"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao." **1 Tim 4:12—**"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi, na mwenendo, na katika upendo, na imani na usafi." Ona pia **1 Tim 3:1-7** na **Tito 1:5-9** kwa sifa za kuwa mzee wa kanisa au askofu.

2. Wahubiri hasa, lazima waishi maisha matakatifu, kwa sababu ni mashahidi wa Mungu, nao wanakabiliwa na hukumu yake. **1 Wathes 2:5, 10—**"Maana hatukuwa na maneno ya kujipendekeza wakati wowote, kama mjuavyo, wala maneno ya juu juu ya kuficha choyo; Mungu ni shahidi . . . ninyi ni mashahidi, na Mungu pia, jinsi tulivyokaa kwenu ninyi mnaoamini, kwa utakatifu na kwa haki bila kulaumiwa." **Waeb 13:17—**"Watiini

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu," **Yak 3:1—**"Ndugu zangu, msiwe waalimu wengi, mkijua ya kuwa mtapata hukumu kubwa zaidi."

3. Wahubiri lazima warejeshe na kudumisha mahusiano sahihi kwa Mungu na wengine.

a. *Unahitaji maisha yenye chapa ya msalaba ili kuhubiri msalaba.* Yesu alisema kwamba sisi wenyewe *hatuwezi* lolote lazima tuwe tumeunganika na mzabibu (**Yohn 15:1-10**). Lazima tubakie tukimtegemea Yesu kikamilifu na neno lake, kama vile Yesu alivyokuwa kabisa akimtegemea Baba yake na Neno lake (ona **Math 26:39; Yohn 4:34; 5:17-20, 30; 6:38; 8:28-29; 10:18; 12:49-50; 14:31; 17:4**).

b. *Kuunganishwa kiusahihi na Yesu, na kujitoa kwa Neno lake, kunamaanisha kwamba lazima tuwe na mahusiano sahihi na watu wengine.* Sifa mojawapo ya kuwa mzee katika kanisa, ni kuwa mkarimu (**1 Tim 3:2).** Kuwa mkarimu kuchukua muda kukaa na watu, kuwajua watu wa ushirika wako (matarajio yao, mashaka, masumbufu, matatizo, na maisha yao kiujumla) kunasaidia uwezo wako wa kuhusiana vyema na watu, na hivyo husaidia utendaji wako kama mhubiri. Yohana aliongeza kwamba, "Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona" (**1 Yohn 4:20;** ona pia **Yak 2:14-26; 1 Yohn 3:17**). Zaidi ya hapo, mtu anayeishi na kunena sawa sawa na Neno la Mungu, katika mahusiano yaliyo sahihi na Mungu na wengine, hawezi kunyoshewa kidole kushutumiwa kuwa ni mnafiki, lakini anaweza kwa ujasiri kuwaita wengine *kumfuata* yeye (ona **1 Wakor 4:16, 11:1; Wafil 3:17, 4:9; 1 Wathes 1:6**).

4. Ushauri wa kimatendo wa kujenga mahusiano sahihi na Mungu na wengineo.

a. Jitahidi kuwa na utakatifu wa kimatendo , wa kweli, wa moyo mkunjufu katika kila eneo la maisha yako.

b. Yafanye maisha yako chasa maisha ya kujifunza kwako maisha ya ushirika wa kudumu na Mungu katika maombi.

c. Soma vitabu vilivyoandikwa na watu waume na wanawake walioileta Biblia pale unapogusa maumivu yao makali, na ambao walisimamia kufa na kupona ukweli wanaoujadili.

d. Elekeza akili zako daima kwenye fikira za kufishwa.

e. Jali mafundisho ya Ki-Biblia kwa jinsi hii; kuwa wewe kama mhubiri, utahukumiwa kwa mkazo mkubwa zaidi.

f. Jali mfano wa Yesu.

g. Jitahidi kwa nguvu zote kumjua Mungu na kunyenyekea chini ya mkono wake wenye nguvu. (Piper 2004: 63-66)

B. ***Kazi ya Roho Mtakatifu katika mahubiri ya ufafanuzi huhitaji wahubiri waishi maisha matakatifu***

1. Katika mahubiri ya ufafanuzi ya kweli, ni Roho Mtakatifu ambaye anafunua kwa mhubiri kweli za kifungu, kutia nguvu maneno yake, na kuwagusa wasikilizaji kuwa watii (ona **Mdo 1:8; 4:31; 10:42-44; 11:12-21; 16:6-10, 14; 1 Wakor 2:4, 12-13; 2 Petr 1:19-21**).

2. Kuwepo kwa uongozi wa Roho Mtakatifu katika mahubiri, kwa kiwango kikubwa, hutegemea *mtazamo* wa mhubiri.

a. *Paulo alionyesha mtazamo unaotakiwa wa unyenyekevu, hata kwa "kuogopa na kutetemeka," mbele za Mungu.* Alitambua atakuwa ananena Neno la *Mungu*, kama chombo cha *Mungu*, kwa watu wa *Mungu*, kwa ajili ya utukufu wa *Mungu*—na kuwa atahukumiwa na Mungu kwa hayo (**1 Wakor 2:1-5**; ona pia **2 Wakor 2:14-17; 4:2, 7; 5:11**).

b. *Mtazamo sahihi unatambua kumtegemea kwetu Roho.* Piper anatuonya: "Phillips Brooks alikuwa anatoa ushauri kwa wahubiri vijana kwa maneno haya: 'Kamwe usijiruhusu mwenyewe kuwa sawa na kazi yako. Ikitokea unaona roho hiyo inakua ndani yako, ogopa.' Na sababu moja ya kuogopa ni kuwa Baba yako atakuponda-ponda na kukunyenyekeza Hatari za kujiona na kujiinua katika huduma ya kuhubiri ina madhara kwa vile Mungu atatupiga ikilazimu ili atuvunje- vunje kutoka katika kujiamini binafsi na matumizi ya kubahatisha ya mbinu za taaluma zetu.

Kwa hiyo Paulo aliinuka kuhubiri (anasema katika **1 Wakor 2:3**) 'katika madhaifu, na hofu, na matetemeko mengi'—akinyenyekea mbele ya utukufu wa Bwana, akiwa amevunjika ile hali yake ya kiburi cha asili, kusulubiwa pamoja na Kristo, kuepukana na majigambo ya ubingwa wa akili. Kukatokea nini? Kukawepo na udhihirisho wa Roho na nguvu (**2:4**)!

Pasipo udhihirisho huo wa Roho na nguvu katika kuhubiri kwetu, hakuna chochote cha thamani kinachopatikana hata kama ni watu wangapi wanaweza kusifu nguvu zetu, au kufurahia maelezo yetu, au kujifunza mafundisho yetu. Lengo la mahubiri ni utukufu kwa Mungu kwa kule

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kujitoa kikikamilifu kwa watu wake Au kwa maneno mengine, katika mahubiri, yeye awekaye agenda na kutoa nguvu ndiye anayepokea utukufu. Kwa hiyo ikiwa lengo la mahubiri linatakiwa lipatikane, kimsingi ni lazima tuhubiri Neno lililovuviwa na Roho wa Mungu katika nguvu itolewayo na yeye Roho wa Mungu." (Piper 2004: 42-43)

c. *Ili kutusaidia kudumisha hali ya kumtegemea Roho Mtakatifu, Piper anafuata hatua tano "katika kutafuta kuhubiri, si kwa nguvu zangu mwenyewe, lakini katika nguvu azitoazo Mungu."* Anazifupisha hatua hizo tano katika neno *KOTTS.* Wakati akili zake "zimezingirwa na hofu na upotofu," na kabla tu ya kuhubiri, "Huwa karibu mara zote naweka moyo wangu kupitia *KOTTS* mbele za Bwana." *KOTTS* inawakilisha yafuatayo. **K—**Kiri kwa Bwana kwamba pasipo wewe siwezi lolote; **O**—Omba upate msaada, ukihitaji uelewa wa ndani, nguvu, unyenyekevu, upendo, kumbu- kumbu, na uhuru ninaouhitaji kuhubiri ujumbe wako kwa ajili ya utukufu wa jina lako na furaha ya watu wako na kwa ajili ya kuwaleta pamoja wateule wako; **T**—Tumaini siyo tu katika wema wa kijumla wa Mungu lakini katika ahadi maalum ambayo ninaweza kuweka tumaini langu kwa saa ile; **T**—Tenda kwa kuamini kwamba Mungu atatimiza Neno lake; **S**—Shukuru Mungu mwisho wa ujumbe kuwa umefika na kwamba kweli ya Neno lake na kazi ya msalaba imehubiriwa kikamilifu kwa nguvu za Roho wake kwa utukufu wa jina lake (Piper 2004: 47-49).

C. *Kuishi kuendana na unachokihubiri, ukiwa na uhusiano sahihi na Mungu na watu wengine, husaidia kwa kiwango kikubwa kuvutia kile unachokisema*

1. Utakuwa unashawishi zaidi hata kama siyo mnenaji mzuri. Watu wengi waliziona nyaraka za Paulo kuwa ni "nzito na za nguvu" hata kama kuwepo kwake binafsi hakukuonyesha kuvutia na unenaji wake ulikuwa "Wa kudharauliwa" (**2 Wakor 10:10**). Kilichotia nguvu maneno ya Paulo kiasi hicho na mamlaka katika akili na maisha ya watu kilikuwa ni "jinsi tulivyo kwa maneno katika nyaraka tusipokuwapo, ndivyo tulivyo kwa matendo." (**2 Wakor 10:11**). Paulo alikuwa kielelezo cha ukweli huu, wakati wahubiri "Wanaonyesha kwamba mamlaka tunayohubiri nayo haitokani nasi binafsi, wala si katika nafasi za vyeo vyetu au wahubiri, wala si katika kanisa ambako sisi tu washirika wake na kutumwa nalo, lakini ni kuwa ndani kikamilifu ya Neno la Mungu tunalolihubiri Ndipo watu wawe tayari kusikia, hasa tunapoweka wazi pasipo shaka yoyote ukweli kuonyesha kwamba tunataka kuishi chini ya mamlaka hii sisi wenyewe" (Stott 1982: 58).

2. Mfano wa Paulo unathibitishwa na wasomi wa taaluma ya uandishi na hotuba. Mwanafalsafa wa Kiyunani Aristotle na wataalamu hao wa hotuba na nyaraka walijadiliana nini kinafanya hotuba iwe ya kuvutia miaka 400 kabla ya wakati wa Paulo. Aristotle aligawanya taaluma hiyo ya utoaji hotuba za kuvutia katika makundi matatu: *logos, pathos,* na *ethos. Logos* huhusika na "Mawazo, muundo, na dhana ya wazo la hotuba inapotathiminiwa kwa msingi wa nguvu ya mvuto wake" (Mack 1990: 36). *Pathos* ni "kulea mtazamo fulani kwa msikilizaji" (Cooper 1932: 8); ni kule kukamata *hisia* na *zile shauku za binafsi* za wasikilizaji (Stern 1991: 89). *Ethos* ni *ile tabia au sifa ya mnenaji.* Hiyo *ethos* ya mnenaji hutegemea utendaji wa hekima yake kimatendo, tabia stahiki, na matakwa mema (Jamar 2001: 73). Aristotle aliona kuwa *ethos* "ndiyo njia yenye nguvu zaidi ya mvuto" (Cooper 1932: 9). Wanafunzi wa kileo wa uhubiri, sheria, na hotuba za mvuto wanatambua kitu hicho hicho ambacho Aristotle alikielezea zaidi ya miaka 2300 iliyopita (Adler 1983: 29-45; Chapell 1994: 25-30; Stern 1991: 13, 87; Stott 1982: 262-98). Kwa hiyo, kuendana kati ya maisha ya mhubiri na maneno yahubiriwayo, zaidi ya kuwa ni muhimu kitheolojia na kiroho, pia yana matokeo ya kina zaidi kwa ajili ya *matokeo mazuri* ya mahubiri.

3. Unyofu wa kiroho*C ethos C* dhahiri kabisa ni wa lazima kwa mhimizo na kuelekeza ushirika jinsi ya *kutendea* dhana ya andishi katika maisha yao (ambayo ndiyo moyo na lengo la ujumbe). Chapell anafafanua hili: "Kutekeleza kimatendo pia kunahitaji uaminifu binafsi. Kwa nini watu wamsikilize mhubiri akiwaeleza kile wasichotaka kukifanya, ambacho hawajakifanya, au ambacho watahitaji kukibadili? Ikiwa jawabu si 'Ni kwa sababu wanajua mhubiri anawapenda wao na Bwana sana sana, kiasi kwamba hawezi kuificha kweli wanayoihitaji,' basi utekelezaji utakuwa umeangukia katika masikio yaliyo kiziwi. Hata inapoumiza, watu husikiliza jambo wanapopokea unyofu wa kiroho ndani ya mhubiri. Kuaminiwa huko hakutokani na uelewa wa usomi au ufundi wa kuandika ujumbe, lakini hutokana na maisha ya mhubiri yanayotoa picha ya Roho inayokaa ndani yake." (Chapell 1994: 222)

4. Wasikilizaji wako hawatapenda kusikiliza ujumbe wako ikiwa hutendi yale unayoyahubiri. "Wakati mahusiano kati ya mhubiri na msikilizaji huwa mara nyingi ni yale ya 'kukidhiana' kuliko 'ukaribu au urafiki wa dhati,' bado, hata hivyo ni uhusiano. Mhubiri ndiye kiongozi wa jumuiya; . . Bila kujali aina ya uongozi, maisha ya mhubiri hutazamwa. Hakuna hotuba nyingine yoyote ya hadharani inayodai mhusika awe na *sifa za kiwango cha juu* kiasi hiki." (Carrell 2000: 25) Katika utafiti wa CTS, watafiti waligundua kwamba: "Wasikilizaji wengi wanasema wanaona mamlaka ndani ya ujumbe wanapotambua kwamba maisha ya mhubiri

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

yanaendana na ujumbe wa mhubiri. Kinyume chake, huchukulia jumbe kilege-lege (au kutoujali kabisa) itokeapo maisha ya mhubiri anapokuwa nje ya madhabahu hayaendani na ujumbe wa mahubiri. Kuhusiana na hoja hiyo ya mbele, walio wengi wanasema, 'Simsikilizi yeyote asiyejaribu kutenda kile anachokihubiri.'" (Allen 2006: 68) Utafiti wa GASS ulibainisha pia: "Wasikilizaji hutazama maisha ya mhubiri.Wasikilizaji huambiana na wenzao kama liko jambo la unafiki limeonekana. Alisema mtenda kazi mojawapo aliye msikilizaji, 'Kila kitu asemacho kwenye mahubiri yake kuhusu kujenga jumuiya, upendo na kuwaheshimu wengine, husikika kizuri. Lakini namwona yeye mwenyewe akiwa katika vikao vya wafanyakazi. Najua jinsi anavyowahudumia wengine.' . . . Asilimia 17 ya wasikilizaji walikuwa na ujumbe moja kwa wahubiri: Fanyia kazi maisha yako mwenyewe ya kiroho." (Carrell 2000: 25-26, 98)

IV. Kujali Dhana na Uelewa wa Wasikilizaji

A. *Kujali dhana*

1. Maandiko yote yana dhana (m.y. yaliandikwa kwa mpangilio fulani wa kidesturi, na kutumia miundo fulani ya desturi. Biblia "haikuandikwa katika utupu, wala wala haikutolewa kwa ajili ya jamii ambayo ni ya kinadharia na isiyokuwepo. Siyo tu kwamba waandishi walikuwa wanaongozwa na desturi zao, lakini maandishi yenyewe yalitolewa kupitia mila na desturi mbali mbali, zijulikanazo kama maandishi ya michoro. Pia, watu waliyapokea maandishi, wakayasoma kuzungukia fikira za mtazamo wa desturi hizo." (Webb 2001: 23)
2. Katika kuutwaa mwili, Yesu alifanyishwa "dhana" kikamilifu: "Alitwaa dhana ya uanadamu katika 'sura ya udhaifu na mapungufu'—kama Myahudi Mpalestina wa kiume, 'aliyezaliwa na mwanamke, aliyezaliwa chini ya sheria' (Wagal 4:4)—katika wakati na mahali maalum. Alikuwa amezamia kabisa katika desturi yake ya Kiyahudi; alishiriki sikukuu zake na desturi zao; alisema lugha ya Aramaic akawa na lafudhi ya Ki-Galilaya; alikuwa na maungo ya kwake na tabia tofauti. Kama Charles Kraft anavyoonyesha, 'Mungu katika Yesu alifanyika sana sehemu maalum ya dhana ya kianadamu kiasi kwamba wengi hata hawakuelewa kwamba alikuwa ametokea mahali kwingine kabisa.'" (Flemming 2005: 20)
3. Yesu na wahubiri na walimu wengine wa Ki-Biblia walikuwa ni wa ki-dhana sana katika mahubiri yao na mafundisho. Yesu "Aliwasiliana na watu siyo kwa mawazo ya kitheolojia, bali kaupitia hali za kikawaida, thabiti—miujiza,maelezo na mifano kutokana na maisha ya kawaida, mithali na simulizi, mazungumzo ya bwana-mwanafunzi na mfano wa maisha yake kati yao. Ingawaje alitoa mafundisho yaliyo mapya tofauti, hakutunga lugha mpya ili kueleza hayo. Badala yake, alitumia picha za vitu vya kidunia vya maisha ya vijijini ya kila siku.Uvuvi na ukulima, magugu na mizabibu, udongo na chumvi ndivyo vilifanyika 'nyenzo' za shughuli zake za kitheolojia. Tangu mwanzo, Injili ilisikika katika hali za kienyeji, na za kidesturi." (Flemming 2005: 21)
4. Yesu na wahubiri wengine wa ki-Biblia na walimu walitofautiana njia walizotumia na *muundo* wa mahubiri yao na mafundisho kutegemeana na hali za wasikilizaji wao, na kusudio rasmi walilokusudia kulipata. Yesu aliweza kuwa mkali sana kwa wanafiki na wale waliokuwa wanamwakilisha visivyo Mungu (**Math 23:13-36**), lakini alikuwa mpole sana kwa watu wadhambi (**Marko 14:3-9; Yohn 8:1-11**). Paulo "anaiweka injili tofauti kwa Wathesalonike, na tofauti kwa Wakorintho ingawaje jamii zote hizo zilikuwa za mpangilio wa desturi za Kiyunani- Kirumi" (Flemming 2005: 20). Katika jumbe zake kuu katika **Matendo,** Paulo alibadilisha mwelekeo wake kulingana na walengwa: kwenye **Matendo 13,** alinena hasa kwa Wayahudi katika sinagogi, akikazia historia ya Israeli, ana kunukuu Agano la Kale, katika **Matendo 17** alisema kwa wanafalsafa wa kipafani huko Athene, akikazia tabia za Mungu, na kunukuu mashairi ya kipagani.

B. *Ingawaje njia za kuwasilisha hoja zilitofautiana kulingana na aina za watu waliohudumiwa na kusudi lililokuwepo, Yesu na wahubiri wengine na walimu wa ki-Biblia mara zote walitumia "tatizo (au tukio)-linaloendana" kama mbinu ya kuhubiri na kufundishia*

1. Karibu nusu ya matukio ya ufundishaji katika Injili yalianzishwa na watu waliokuwa na uhitaji wao wenyewe, tatizo, au jambo; katika nusu ya mafundisho ya Injili ambayo aliaanzisha Yesu, pia yeye "Alinena kwa kiwango cha mtu wa kawaida kwa sababu, ndivyo wanafunzi wake walivyoweza kuunganisha ukweli wa umilele na maisha yao wenyewe" (LeBar and Plueddemann 1995: 93). "Roho itatuayo matatizo hutawala Injili. . . . Wakati mwingine Yeye mwenyewe aliyachukua maswali yao kutoka akilini mwao na kutoa tatizo kama hivi, 'Je! mwadhani ya kwamba Wagalilaya hao walikuwa wenye dhambi kuliko Wagalilaya wote, hata wakapatwa na mambo hayo? Au wale kumi na wanane, walioangukiwa na mnara huko Siloamu—ukawaua, mwadhani ya kwamba wao walikuwa wakosaji kuliko watu wote waliokaa Yerusalemu?' (Luka 13:1-2)

Maswali yake ya kihalisia yalikuwa na makusudi ya kulipa sura halisi hitaji na kukazia mtazamo

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kumwelekeaYeye. Hakuwaagiza watu wamjibu maswali yake. Alikuwa akitafuta uelewa wa kiroho na matendo kwa misingi ya mafundisho Yake. Mara zote alitumia maswali ili kuwahusisha wasikilizaji wake kibinafsi katika mazingira ya yale mafundisho na kuwaongoza kwenye kweli." (Ibid.: 94)

2. Nyaraka za Paulo zote zilielekezwa kwa makanisa ya mahali pamoja au watu binafsi, ili kushughulikia uhitaji maalum, matatizo, na mswala. "Nyaraka nyingi za Paulo si tungo zilizoandikwa kwa mpangilio mzuri bali ni jumbe za maelekezo zenye vipengele vya mtu binafsi. Mara zote huwa zimeelekezwa kwa makanisa au watu fulani, daima zikijibu nyaraka zilizopokelewa. Kila moja, isipokuwa labda Waefeso, iliandikwa ili kushughulikia tatizo lilokuwepo pale, na pia hatimaye kuhudumia kizazi chote cha kanisa. Kauli za mafundisho huibuka kutokana na mazingira ya tatizo la mahali husika Hata sehemu zenye mafundisho ya kina ya Warumi yaliandikwa kutatua mahitaji ya mahali husika. Wakati mwingine Paulo alianzia na matatizo ya kanisa, na kuhusisha matatizo hayo na kweli ya Mungu. Nyakati nyingine alianzia na kweli na kisha akahusisha ukweli huo na maisha. Lakini hakuna popote ambapo Paulo anafundisha mambo yasiyohusiana na mahitaji na matatizo ya maisha." (LeBar and Plueddemann 1995: 131, 136)

C. ***Mahubiri yetu yafuate mfano wa Yesu na Paulo***

"Yesu kamwe hakufundisha maswala yaliyo nje ya maisha, wala hakufundisha majibu ya matatizo ya kiutendaji pasipo kufundisha Neno" (Plueddemann 1994: 46).

"Ufahamu huu kuwa kila Andiko unaelezewa kwa kiwango fulani kuhusu anguko la mwanadamu na kuwa umeandalika kuwaongoza wasikilizaji wake kuelekea lengo la utimilifu katika Kristo, kwenye matokeo zaidi, na pia nguvu ya kiustadi ya kuhutubia. Kuhusu uunganishi wa Maandiko, tafsiri ya ya kila Andiko lazima ihusishe kwa kiasi fulani mazingira lilipoandikwa na mazingira ya wasomaji wale wa mwanzo. Kutambua *tatizo maalum* lililosababisha Andiko kuwako pale mwanzoni, uhitaji wa wapokeaji wa awali, ni wa muhimu katika ugunduzi wa *kusudio la Ki-Mungu* katika kubuni jumuiya takatifu ambayo washiriki wake hukua kuelekea ukamilifu katika Kristo. Kuhusu nguvu ya kiustadi, katika kutambua jinsi tatizo la kiroho linavyojidhihirisha katika maisha ya wasikilizaji —licha ya tofauti zote za wakati na mahali na desturi na mwonekano wa juu—huleta mwelekeo wa uhakika zaidi wa uhusishwaji wa ujumbe wa Andiko kwa mazingira yetu ya siku za leo. Kwa vile kuhusishwa huko kwaweza kuonekana kunatokea moja kwa moja kwenye Andiko, hubeba yote mawili –usahihi kamili na mguso wa dhamira." (Johnson 2007: 71n.5)

"Wakiwa na moyo mkuu na kushawishika, wasikilizaji wetu katika kujifunza [kujifunza Agano Jipya] wanaonyesha uhitaji wa mahubiri yanayoshughulikia maswala yaliyo magumu zaidi ya kimaisha. Katika shauku yao ya kusikia njia za Mungu kati yetu na kukubaliana kwao juu ya ugumu na hatari za kuhubiri kuhusu maswala nyeti, wasikilizaji hawa wanaonyesha shauku kali ya kuhubiri ambako mara zote huletesha mkabala wa kina juu ya maswali ya kimaisha na utata wa imani ya Kikristo. Kwa umuhimu huo huo, maneno yao huonyesha uhakika walio nao kwenye Neno la Mungu katika maandiko nao huwataka wahubiri wachote katika rasilimali ya imani ya Kikristo kuelezea migongano ya dunia inayowazunguka." (Mulligan, et al. 2005: 108)

"Kama tunataka Yesu afundishe kwa njia yake kutupitia sisi, je mkondo wetu wa kawaida utaonekanaje? Tutaanzia walipo wanafunzi wetu, na mahitaji yao ya sasa, na kuwasaidia wapate majibu ya Mungu katika Maandiko, na kuanza kuitenda kweli juma hili." (LeBar and Plueddemann 1995: 99)

1. Muundo wa mafundisho ya Yesu na Paulo umeelezwa kama "Muundo wa Uzio wa Reli."



2. James Plueddemann, ambaye alitengeneza muundo huo anauelezea: "Muundo wa uzio wa reli umefanyishwa na reli mbili zilizoshikana pamoja kwa vyuma vya reli. Reli ya juu huwakilisha kweli. Reli ya chini huwakilisha uzima. Chochote kinachosaidia kuunganisha kweli na uzima ni nguzo ya reli. Nguzo ya reli inaweza kuwa ni uelewa anaougundua mwanafunzi kuhusu uhusiano kati ya kifungu cha Biblia na hitaji la maisha. Walimu wengi hutamani kujenga nguzo za reli kwa mbinu za mafundisho yao wenyewe. Uhakiki makini nao ni mfano mwingine wa nguzo kati ya kweli na uzima. Mwalimu afanyaye kazi na Roho Mtakatifu hutafuta kufundisha kweli katika namna ambayo huchochea uhakiki makini kati ya mahitaji ya maisha ya

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mwanafunzi na kweli ya Neno la Mungu.

Kweli bila uzima huleta imani mfu. Uzima pasipo kweli huzaa uasi wa kidini. Kufundisha kimoja tu pasipo kingine si ki-Biblia na si kichocheo kinachotakiwa kwa ukuaji kiroho." (LeBar and Plueddemann 1995: 101)

3. Kuutumia "Muundo wa Uzio wa reli" kwenye dhana ya mahubiri:

Unapoandaa ujumbe wako, unaanzia na "reli ya juu" (m,y, unakitafsiri vizuri kifungu cha Maandiko); lakini *unapoandaa* ujumbe wako, anza na "reli ya chini" (m,y, hitaji, tatizo, au swala katika maisha ya watu).

a. *Maisha ya watu wengi hayaendani na Neno la Mungu.* "Kikawaida huwa na mvutano kati ya viwango vya Mungu na viwango vyetu. Mvutano huo unasababisha mwenendo wa akili, hisia, na tabia. Itokeapo maisha yetu yanapishana na viwango vya Maandiko, kunakuwa na matatizo na mafadhaiko. Vurugu za kihisia ni matokeo ya mvutano huo." (LaBar and Plueddemann 1995: 101-02) Hali za watu huonekana namna hii:



b. *Ujumbe wako umeundwa kuwasaidia watu kuelewa hitaji lao, kuelewa jinsi Neno la Mungu linahusika na hitaji hilo, na kuleta maisha yao (ile "reli ya chini") husimamia kiuthabiti kwenye kweli ya Neno la Mungu ("reli ya juu").* Kwanza anzia kwa kuibua hitaji, tatizo, au swala linalowaathiri watu wa ushirika wako. Kwa kuibua swala linalowaathiri watu mwanzo wa ujumbe wako, ama kwa kuuliza maswali ya kiustadi, au unapata usikivu wa watu wako, kwa sababu wanajua utakuwa unashughulikia kitu ambacho ni muhimu katika maisha yao. Baada ya kulitaja jambo ("reli ya chini"), ndipo unaelekea kwenye "reli ya juu." Unaweza kusema kitu kama vile, "Hebu tuone Biblia inasemaje kuhusiana na swala hili." Kisha unawaonyesha watu jinsi ya kutumia kifungu hicho cha Biblia kinavyowasaidia kushughulikia matatizo yaliyoibuliwa mwanzoni. "Mchakato wa kufundisha, kama uzio wa reli, una mduara wenye hatua tatu. Mwalimu kikawaida huanzia kwa kuwasaidia wanafunzi kuona matatizo maishani mwao (ile reli ya chini) ambayo yanaweza kuunganishwa na Maandiko ya kujifunza. Kisha mwalimu anamsaidia mwanafunzi kuelewa dhana ya Maandiko (reli ya juu). Tatu, mwalimu anawapa changamoto, kuwachochea na kuwahamasisha wanafunzi kugundua uhusiano kati ya kilichomo kwenye Maandiko na tatizo lililopo kimaisha (Nguzo za reli). Kwa muujiza wa neema ya Mungu, watu wanaweza kukua kufikia ukomavu katika Kristo, kupitia nguvu ya Neno, Roho, na walimu wenye vipawa rohoni." (LaBar and Plueddemann 1995: 102)

4. Plueddemann anatumia mlinganisho mwingine wa kile mhubiri au mwalimu anachojaribu kufanya. "Mwalimu anayefaa ni kama mtu anayechukua kamba ngumu, na kufunga ncha yake mojawapo kwenye fikira kubwa za Maandiko, na kufunga ncha nyingine, kwenye dhana kuu za maisha, na kisha kupitia nguvu za Roho, hufanya juhudi kuyavuta hayo mawili yakutane" (Plueddemann 1994: 48).

5. Ujumbe unatakiwa uwasukume watu kuona kiuthabiti tofauti kati ya mambo waliyokutana nayo katika maisha; watofautishe na Biblia inavyosema. Swali la msingi ambalo wahubiri wanapaswa kujiuliza wenyewe wanaposoma na kuandaa ujumbe ni: "Ni Neno gani la Mungu kwa watu wangu, na linahusianaje na mazingira husika?" Mchungaji lazima atambue kwamba maisha—iwe katika kiwango cha mtu binafsi, kanisa, jumuiya, au ngazi ya taifa—haya endani na jinsi Maandiko yanavyosema yawe. Kwa hiyo: "Biblia inafundishwa vizuri kabisa, lakini kufundisha siyo mwisho—ni njia tu. Mwalimu lazima ampe changamoto mwanafunzi kuchunguza mvutano kati ya viwango vya Mungu na matukio ya maisha, na kumsaidia mwanafunzi kuyaleta hayo pamoja Mwalimu afaaye wa Biblia ni mwalimu mzuri wa mada yake, lakini pia huwapa changamoto wanafunzi wake kuhangaika na utendaji wa maagizo ya ki-Biblia kwenye njia panda za kimaadili, matatizo katika kanisa, na mwenendo binafsi wa mtu. Mwalimu anayefaa daima atashikilia Maandiko halisi katika ulimwengu huu wa uvutano mkuu wa ubunifu uliopo kwenye mawazo ya kileo na kisasa." (Plueddemann 1994: 49-50)

6. Huu ni mchakato ule ule ulioitwa "dhana ya kujikosoa": *"Kujifunza undani wa desturi/mila:* Hatua ya kwanza katika dhana ya kujikosoa ni kujifunza desturi/ mila za mahali hapo kwa jinsi wanavyojielewa

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

wenyewe [m.y, jinsi watu wanavyoelewa imani zao na mambo wanayoyafanya] *Kuyaelewa Maandiko na kuchunguza maana ki-kuhusisha:* katika hatua ya pili, mchungaji, au mmishinari huliongoza kanisa kujifunza Maandiko yanayohusiana na swala lililojitokeza *Mwitikio wa kujikosoa:* Hatua ya tatu ni kwa ushirika kwa pamoja kutathmini kukosoa desturi zao za kale kwa kusimamia nuru ya uelewa mpya wa ki-Biblia, na kufanya uamuzi kuhusiana na mwitikio wa hizo kweli mpya walizozijua. Injili siyo tu ni habari za kutangazwa. Ni ujumbe ambao watu wanapaswa kuonyesha mwitikio." (Hiebert 1987: 109-10)

7. Kutumia "Uzio wa Reli" kwa katika mbinu ya tatizo (swala) kama msingi katika jumbe kunafaa kwa kuwasaidia watu kubadili jinsi ya kuishi.

a. *Mbinu ya hapo juu imeshatumika kwa mafanikio kwa njia nyingi katika mipangilio tofauti duniani.* Hii ilikuwa mbinu ya Yesu mwenyewe. Ni mbinu ya waelimishaji wa Kikristo kama LeBar na Plueddemann. Mwelimishaji wa elimu ya kawaida, kama vile Paulo Freire aliandika kirefu kuhusu mbinu hiyo hiyo ya kuweka msingi kwenye tatizo (ingawaje hakujumuisha ile "reli ya juu" ya Maandiko), na aliitumia kuwafundishia watu masikini huko Brazil (Freire 1973). Waelimishaji wengine wa elimu ya kawaida na wanasaikolojia wametambua umuhimu wa mbinu hii (ona LeBar and Plueddemann 1995: 9-13). Plueddemann mwenyewe aliitumia mbinu hii kwenye masomo ya darasa la Jumapili aliyoyaandika, na semina za uongozi alizozibuni kama mkuu wa idara ya Sudan Interior Mission's Christian Education kwa ajili ya makanisa ya Ki-Injili ya Afrika Magharibi (Ibid.: 13).

b. *Utafiti wa CTS unaonyesha kwamba mbinu kama hii husaidia mahubiri kuwa ya kufaa.*

(1) Kitovu cha mbinu ya "Uzio wa Reli" ni kuwafanya watu waone kutounganika kwa maisha yao na jinsi Mungu anavyowataka wao waishi, na jinsi Maandiko yanaweza kuwaonyesha njia bora zaidi ya kuishi. Hii inamhitaji mhubiri kuwasaidia kufikiria mambo ambayo hawakuyafikiria zamani, au kufikiria mambo kwa njia mpya. Hivyo ndivyo vipengele vinavyoongoza kwenye mabadiliko: "Jambo linalodumu kuumbika ndani ya kauli za wasikilizaji ni kuwa mara zote hubadili mawazo na tabia wakati maisha yao yameparaganyika.[m.y; nje ya uwiano]. Hali yao ya mparaganyiko inaweza kutambulika kabisa na huweza kubadili mtazamo wa maisha (kwa mtu binafsi au kundi), au haiingii kwenye ufahamu wa msikilizaji mpaka itajwe kwenye mahubiri. Ni dhahiri, ujumbe unaweza kuletesha ufahamu wa mparaganyiko. Wasikilizaji wengi huitikia wakati kama huo katika hali ya kuwa tayari kwa uwezekano wa kuwa na mtazamo mpya na matendo mapya." (Allen 2008: 68-69)

(2) Kuonyesha mrandano kati ya maisha ya watu katika Biblia na maisha ya sasa ya washirika, huifanya Biblia kuwa "halisi" kwa wasikilizaji. LeBar anatukumbusha kwamba, "Kwa vile asili ya mwanadamu haibadiliki ghafla kwa karne kadhaa na Biblia inasema kwa hali za wanadamu, hushughulika na matatizo ya msingi licha ya tofauti kubwa za desturi. Watu waliomo kwenye Biblia wanapaswa kusomwa kwa dhana zao, hata hivyo, matatizo yao ni yetu pia." (LeBar and Plueddemann 1995: 98) Utafiti wa CTS uligundua kwamba: "Kusikia kwamba watu wa kwenye Biblia walisumbuka kama watu wa siku hizi, kuliwatia moyo wengi wa waliohojiwa. Kama moja asemavyo 'Nafikiri kitu kimoja mchungaji wetu hufanya vizuri sana ni kule kuwaelezea watu wa kwenye Biblia kuwa ni watu halisi. Wakati mwingine mchungaji hufika mahali pa kutumia simulizi fupi za kuchekesha kutusaidia kuelewa kuwa walikuwa watu wa kawaida.' Hilo ni muhimu kwa sababu 'Mara nyingi tuna watu wa ki-Biblia katika ghorofa ndani ya akili zetu, na wahubiri huwasiliana nasi kama watu halisi. Hilo hutusaidia sana.'" (Allen 2008: 66)

D. ***Uelewa wa wasikilizaji na matokeo ya mbinu ya kutumia matatizo (tukio) kama "Uzio wa reli"***

1. Kwa vile Maandiko yote ni ya ki-dhana. "Mahubiri ya ki-dhana ni kuhubiri ambako andishi na dhana nzima iliyopo *huendana kuunda* ujumbe unaojaribu kutolewa. Hii inamaanisha kwamba dhana ndiyo mhimili [m.y; ya lazima, ina nguvu kujenga] katika mchakato wa kuandaa mahubiri. Ni tu mhubiri akiendelea kutoka katika dhana, ndipo ujumbe wake unaweza kufundusha hali iliyopo ya kushirika wake katika namna ya maana." (Pieterse 1984: 5)

2. Ili kuleta matokeo zaidi, wahubiri wanatakiwa wawe na mchakato wa kimpangilio wa kukusanya vidokezo vihusuzo mahubiri yanayofuatia. Wasilizaji walio wengi wa kamwe hawazungumzi na wahubiri kuhusiana na mahubiri wanayoyasikia. Huo ni upotevu mkubwa wa rasilimali. Ingawaje wahubiri hutumia muda mwingi wa maandalizi ya mahubiri kwa kusoma Biblia, wahubiri kiukweli wana vyanzo viwili vya kusoma: Biblia na wasikilizaji wao. Wanapaswa kuelewa pande zote mbili. Mwandishi wa "Utafiti wa GASS" anasema: "Wahubiri, je mnayajua mawazo na hisia za wasikilizaji wa ujumbe au somo unaloandaa? Je mnaweza

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mkauweka kwenye kundi la kukidhi haja za wasikilizaji mnapoanza kuuandaa ujumbe wenu? Lazima uibuliwe utaratibu fulani wa kupokea mtazamo wa fikira za wasikilizaji. Wahubiri wanaweza kuimarisha mahubiri yao kwa ubunifu, upya, na yenye kuleta maana, kwa kujidhatiti kujua mitazamo ya wasikilizaji wao na kuingiza fikira zao katika kila mahubiri.

Wahubiri, maisha ya wasikilizaji wenu ndiyo rasilimali kubwa kuliko zote. Ikiwa kitabu hiki kinawaongoza kufanya badiliko moja, na liwe ni moja tu, nawasihi, undeni mchakato wa kuwawezesha kupata mawazo kuhusiana na mahubiri mnayoandaa. Tajeni vichwa na masomo mapema, weka 'kiboksi cha Kutegemeza Mahubiri' mahali palipo wazi, na uwakaribishe wasikilizaji wachangie mawazo, hoja, na maswali yao.'

Unda kundi la wasikilizaji ambao utazungumza nao kuhusiana na mahubiri yanayofuatia. Kama hali ya hewa inayoonyesha kutowezesha kukutana, basi toa visaidizi maalum vilivyochaguliwa vifanyizwavyo na vikundi vya usaidizi vya wasikilizaji wako, wakati ukijielekeza kwenye muundo wa ushirikiano, na kadiri unavyowaachia wasikilizaji wako kwenye mchakato wa mazungumzo ya uhalisia. Waweza pia kufanya mwaliko wa wazi kwa kifungua kinywa cha pamoja, chakula rahisi cha mchana cha mifukoni, au mlo mdogo wa jioni, ili uweze kuwasikiliza wasikilizaji wakiongea kuhusu ya kuwemo katika ujumbe wa mahubiri yafuatayo. . . .

Wahubiri, ikiwa kikundi cha kutegemeza mahubiri kitakuwa sehemu muhimu ya maandalizi ya mahubiri yako, siyo tu kutakuwa na badiliko la nguvu ya maneno ya ujumbe wenu, bali jumuiya ya kanisa itaimarika kutokana na mahusiano yajitokezayo." (Carrell 2000: 210, 212)

3. <u>Ili kuweza "Kuielewa vizuri desturi [au dhana]," kusudi kuweza kuunga ile "reli ya juu" na "reli ya chini" pamoja, mhubiri lazima ajihusishe kikamilifu na watu wake na kuwajua vizuri.</u> "Mhubiri lazima alowee, lazima *naye aishi* hiyo hali na dhana ya washirika wake. Mhubiri lazima ahusike na mambo yaliyo 'ya shinani kabisa' kimkabala, hisia na kimawazo ya washirika wa kusanyiko lake. Lazima aielewe theolojia yao. Ikiwa atakaa na jumuiya yake, kuteseka pamoja nao, kukata tamaa na kutumaini pamoja nao, kuasi pamoja nao kinyume na dhuluma na makandamizo, ndipo anaweza kuhusisha ujumbe wa Biblia na maisha yao. Hii ndiyo mbinu ya mahubiri ya dhana." (Pieterse 1984: 7-8) Katika Utafiti wa GASS, "asilimia kumi na saba ya wasikilizaji wanashauri kwamba wahubiri waongeze mahusiano na wasikilizaji wao. Jawabu la kawaida katika kundi hili ni, 'Wajue wasikilizaji wenu.'" (Carrell 2000: 97)

4. <u>Kujitambulisha na washirika kunaweza kukadhihirishwa kwenye ujumbe.</u> Kujitambulisha na washirika kunaongeza uthamani wa mhubiri na ufanisi wake. Utafiti moja wa Amerika ulionyesha kwamba hata kule kubadili maneno kutoka "ninyi" kuwa "mimi" katika mahubiri kunasaidia kumuunganisha mchungaji na watu wake, na "Kuongeza ushirikiano na usikivu" (Theis 1981: 51). Ikiwa mhubiri "ataishi hali na dhana ya washirika wake," maisha yake yenyewe yanaweza kuwa ujumbe wa nguvu. Kusikia simulizi zimhusuzo mhubiri mwenyewe ni muhimu kwa mkondo fulani wa watu walioohojiwa. Baada ya kumwelezea mhubiri anayesumbuka na wazo la mabadiliko, msikilizaji anasema, "Kuwasikiliza watu wengine wakisema waziwazi na kushuhudia imani yao husaidia nyakati fulani kuunganisha na kunisaidia kwenye jambo linisumbualo ambalo naweza kuwa nimelipitia, na ya kuwa wao nao wamewahi kulipitia na sasa wananisaidia kulishinda." (Allen 2008: 66)

5. <u>Mhubiri anaweza kuhubiri tu kile ambacho wasikilizaji wake wanaweza kuelewa na kupokea.</u> Katika kuandaa na kutoa jumbe zao, wahubiri wanapaswa kizingatia vitu vingi kuhusiana na wasikilizaji wao, kama vile; a. kiwango chao cha elimu; b. mgawanyo wa kijinsia; c. mgawanyo wa kiumri; d. walio waamini na wasioamini; e. kiwango cha kukua (kiroho na kimwili); f. ufahamu wa ki-Biblia; g. njaa ya Neno; h. historia za maisha; i. desturi, historia, na vipengele vingine vinavyoathiri na kuongoza wasikilizaji. Vitu kama hivyo huweza kuathiri vipengele vingi vya ujumbe, kama vile: a. urefu wa ujumbe; b. kiwango cha mfumo wa ujumbe uutoao; c. sehemu ya chanzo ambacho unatolea ujumbe wako; d. lengo la ujumbe wako; e. muundo wa ujumbe; f. kiwango cha undani wa ujumbe huo.

6. <u>Wahubiri wanapaswa kuwa makini kwa vipengele vingine maalum vya washirika wao.</u> "Mahubiri ya dhana" huhitaji kwamba ujumbe uendane na uwezo wa kimawasiliano na matarajio ya wasikilizaji. Zaidi ya hapo, mhubiri anahitajika kuwa msikivu kwa maswala kama: hali ya ndoa, uwezo/ kutokuwa na uwezo wa kupata watoto (pia maumivu na machungu ambayo kukosa watoto kunaweza kuleta); ujane; yatima; hali ya VVU/UKIMWI, nk. Kulingana na Utafiti wa GASS, "Wasikilizaji walio wengi ni wanawake (asilimia 61) na idadi kubwa sana ya kushangaza ya wahubiri ni wanaume (asilimia 84): . . . Kwa wasikilizaji wengi walio wanawake, utofauti huu wa kijinsia, huchangia kwa kiwango kikubwa kwao kuona mahubiri hayana maana na wahubiri kutowajua vizuri.'" (Carrell 2000: 145-46) Wahubiri wengi wa kiume hutumia mifano mingi ya michezo kwenye jumbe zao, bila kujali kwamba mifano kama hiyo inaweza isiwafae sana wanawake (m.y; ambao ndio walio wengi) katika ushirika. Watu wote huelekea kufikiri, kutenda, na kunena kwenye "uwanja

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

wao wa raha." Hata hivyo, ili uwe mhubiri mwenye kufaa, mchungaji lazima utoke kwenye eneo lako la raha na kuingia kiukweli katika dunia na dhana ya washirika wake.

7. Wahubiri wanapaswa wawe makini na wasikilizaji wao, na mwitikio wao, *wakati wa* mahubiri. Unahitaji kuhakikisha unawaangalia watu mbali mbali wakati wa mahubiri. Hilo litakusaidia "kujishika" na kusanyiko. Mwonekano wa sura za wasikilizaji, kuitikia kichwa, macho, nk vitakujulisha kama wanakuelewa, wanakubaliana, na wanaguswa na kile unachokisema: "Mwitikio wa wasikilizaji ni sehemu muhimu katika swala hili zima la usemaji. Kile ukionacho usoni au katika macho ya wasikilizaji wako kinakujulisha karibu mara moja iwapo unafikisha ujumbe, au vitu vingine vinavytokea. Mwitikio wa namna hiyo hauwezi kupuuzwa katika unenaji wa kufaa." (Adler 1983: 78)

V. Mambo ya Kuzingatia Kuhusiana na Kifungu cha Biblia Unachokielezea

Vidokezo vyenye undani mwingi kuhusu jinsi ya kuchambua na kujifunza kifungu cha Maandiko ili kukihubiri vizuri, vimeambatanishwa kama **Dibaji A ("Masomo Ya Biblia Ya Kina Kwa Mahubiri"),** na **Dibaji B ("Hatua za Ujumbe: Vidokezo Vichache Kabisa Kwa Wahubiri").** Mambo muhimu hasa ya kuzingatia kuhusiana na kifungu unachotaka kukihubiri yanajadiliwa hapa chini.

A. *Lengo la kifungu*

1. Mungu anayo *sababu* au *kusudi* nyuma ya kila kifungu cha Maandiko kilichoandikwa.

   a. *Maandiko yote ni ya kutukamilisha sisi, ili kwamba tuweze kuwa tumekamilishwa na kufaa kwa kila kazi njema ambayo Mungu ameiandaa kwa ajili yetu—bila shaka, ili kwamba tupate kuwa kama Kristo mwenyewe (ona* ***2 Tim 3:16-17; Warum 8:29; 15:4; Waef 2:10****).*Kwa hiyo, mhubiri lazima *ahusishe* kifungu hicho kwa wasikilizaji wake katika namna ambayo inaendana na sababu au lengo la Mungu aliyemfanya mwandishi aweke kifungu hicho katika Maandiko. Chapell anatueleza: "Hatuelewi kikamilifu somo mpaka tuwe tumefahamu pia *sababu au chanzo chake.* Kuzingatia dhana ya ujumbe hatimaye hutulazimisha tujiulize, 'Kwa nini maswala haya yanatajwa? Nini kilisababisha maelezo haya, hoja hii, au kuandika mawazo haya? Nini lilikuwa kusudi la mwandishi? Ni kwa kusudi gani Roho Mtakatifu aliweka maneno haya katika Maandiko?'" (Chapell 1994: 40)

   b. *Siiku zote inasaidia kuandika vidokezo vya kifungu unapokisoma, ili kuelewa mkondo wa mawazo ya mwandishi*—bila shaka, hutulazimisha sisi—kuona muundo na mtiririko wa fikira za kifungu, kwa hiyo lazima tuweke vidokezo hivyo kwenye karatasi. Kuweka vidokezo pia hutulazimisha kueleza kwa maneno yetu wenyewe hoja kuu za kifungu.

2. Hasa wakati wa kuhubiri AK (lakini pia wakati wa kuhubiri AJ) tunapaswa kujiuliza wenyewe, "Kristo yuko wapi katika hili?" "Haiwezekani kutoka Agano la Kale peke yake kuelewa kiwango kamili cha matendo ya Mungu na ahadi zake zilizoandikwa mle" (Goldsworthy 1991: 54). Sababu inayofanya Agano la Kale pekee lisionyeshe maana kamili, iliyojificha chini yake, ni msingi wa ufunuo wa hatua kwa hatua: m,y; zile kweli za Ki-Biblia hazikufunuliwa zote kwa mkupuo, bali zilifunuliwa pole pole kwa hatua kwa muda mrefu. Kwa hiyo, **AK** ni maandalizi ya zile Injili; na **zile Injili** ni udhihirisho wa Injili; **Matendo ya Mitume** ni mpanuko wa Injili; na **Nyaraka** ni maelezo ya zile Injili; na **Ufunuo** ni ukamilifu wa Injili. Maana kamili ya kifungu chochote kiwacho haiwezi kuwa wazi hadi Biblia yote na hatua za lazima zihusishe muunganiko mzima kama muktadha timilifu wa kifungu chochote." (Johnson 2007: 156). Yesu na waandishi wa AJ walielewa hilo. Waliona AK zima kinamna fulani kama kitabu kumhusu Yesu. Yeye ndiye mhusika mkuu na dhana inayolengwa (**Luka 24:25-27, 44-45; Yohn 5:39-40, 46; Mdo 3:18, 24; Mdo 10:43; Mdo 26:22-23; 2 Wakor 1:20; 1 Petr 1:10-12; Waeb 1:1-3**). Kwa sababu ya hili, "Uhusika wa *kila* muunganishi na mshiriki wa kiaganao—waanzilishi, nabii, kuhani, mwamuzi, mfalme, mume, baba, mwana, wazazi, watoto, mtumishi—hatima ya yote kutafsirike katika nuru ya uelekeo wa kuakisi (au kuonyeshe mapungufu ya kutoakisi) utii kamili wa kiagano unaotolewa na Yesu kama Bwana wa watu wake—kimajumuisho, utimilifu wa upatanisho utakaopatikana na Yesu Mwana wa Mungu na ndugu wa watu wake kwa hiyo, tabia mchanganyiko wa viongozi wa kiagano humfanya, kila moja, kwa sifa ya nafasi yake, kwa njia moja au nyingine, mfano wa Mkombozi Ajaye, ambaye ndani yake, majukumu ya nabii, kuhani, na mfalme yatakamilika kikamilifu." (Ibid.: 216) Mifano ya hii inaweza kuwa yote mawili **-** chanya na hasi. Mifano chanya ni pamoja na akina Yufufu ambaye alisalitiwa isivyo haki na ndugu zake mwenyewe, lakini akabakia mwaminifu licha ya magumu yaliyomkabili na majaribu, akaja kuinuliwa juu sana na kuwaokoa wengi (**Mwa 37: 1-36; 39:1-47:31; 50:1-26**), na Isaka (**Mwa 22:1-18**) ambaye kwa hiari yake alijitoa kwa baba yake na kujitoa mwenyewe kama sadaka. Mifano hasi ni kama ile ya Lameki (**Mwa 4:17-24**) ambaye aliudharau mpango wa Mungu wa ndoa (tofauti na Kristo—**Waef 5:25-32**), aliuawa akiwa katika kuasi agizo la Mungu (ona **Kut 21:23-25**), na kuonyesha roho ya kisasi badala ya msamaha (tofauti na Kristo —**Math 18:21-22**), na

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

maanguko ya "Waamuzi' na maamuzi yasiyo haki ya wafalme' [ambayo] yalionyesha kwa Israel uhitaji wa mfalme ajaye ambaye atatoa haki katika hali ambayo ni ya usawa na maarifa yote (Isa. 11:1-5)" (Ibid.). Kwa namna nyingine, ili kuhubiri kifungu cha Agano la Kale kiukweli katika utimilifu wa muktadha wa Biblia nzima, tunahitaji kufanya mambo mawili: "[1] kubainisha (kwa uthabiti tuwezavyo) jinsi wasikilizaji wale wa awali wangepaswa kuelewa; lakini pia [2] tuweke maana hiyo katika muktadha wa mtiririko wa muundo wa ki-Mungu wa historia ya ukombozi na ufunuo wa wokovu uliokuwa daima ukichochea mioyo ya waamini kuelekea kwa Kristo." (Ibid.: 330) Wasikilizaji wetu, kwa hiyo, wataweza kuona jinsi AK lilivyokuwa likilenga utimilifu kamili katika Kristo.

3. Wakati tunapochanganua kifungu, tunatakiwa tujibu maswali mawili ili kujua kusudi la kifungu:

a. *Kifungu hiki kinatueleza nini kuhusu Mungu (m.y, Kitu gain "Kigezo cha Ki-Ungu")?* "Biblia haimhusu Ruthi, Daudi, Yona na Petro, bali ni kumhusu Mungu wa Ruthi, Daudi, Yona na Petro" (Harris 2004: 66). Mungu yuko katika namna mbali mbali, na hutenda kwa njia tofauti, kwa dhahiri na kwa jinsi isivyo dhahiri, kila mahali katika Biblia nzima. Anatuita tuwe na ushirika na uhusiano naye. Tunahitaji kujiuliza jinsi gani alivyo katika kifungu hicho tunachojifunza.

b. *Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu watu na hali ya uanadamu? (M.y, ni kitu gani "Kigezo cha Hitilafu")?*

(1) Kwa sababu ya hali ya kuanguka kwa mwanadamu, watu wana uhitaji wa kila namna, matatizo, na maswala wanayojaribu (lakini wanashindwa) kutosheleza au kuyatatua mara nyingi kwa kutumia (daima kwa kukosea) njia nyingi (ambazo daima huishia kuwaletea matatizo mengi zaidi kuliko waliyoanza nayo). Chapell huiita hii *Mkazo wa Hali ya Anguko* (MHA), na huielezea kwa jinsi hii: "Kwa vile Mungu aliiandaa Biblia ili itukamilishe, yaliyomo ndani yake lazima yawe yanaonyesha kinamna fulani kuwa hatujakamilika. Kupungukiwa kwetu ni matokeo ya hali ya anguko ambayo tunaishi nayo. . . . Hali ya uharibifu wa dunia yetu na wa nafsi zetu, hulilia msaada wa Mungu. Yeye hujibu kwa Neno lake, akilenga vipengele fulani vya mahitaji yetu kila sehemu. *Hiyo MHA ni hali ya kunufaishana ya kianadamu ambayo mwamini wa sasa anashiriki na wale ambao waliandikiwa, ambao wanahitaji neema ya kifungu hicho.*" (Chapell 1994: 41-42)

(2) Kwa vile hiyo MHA ya kifungu imeanzia kwenye hali ya mwanadamu, MHA huweza kubadilika kutoka andiko hadi andiko jingine. Kwa mfano, hiyo MHA ya kifungu, yaweza kuwa ni swala lisilo la ki-dhambi au dhambi maalum. *Maswala yasiyo ya ki-dhambi yaweza kuwa ni:* uchungu, magonjwa, shauku ya kurudi kwa Bwana; uhitaji wa kutaka kujua jinsi ya kushirikisha Injili; jinsi ya kuomba vizuri, shauku ya kuwa mzazi bora zaidi, kupania mapenzi ya Mungu, kudumisha unyofu katikati ya upinzani; au kuelewa vipawa vya mtu. *Dhambi maalum huweza kuwa ni:* uchoyo, uasi; tamaa; kutowajibika, uwakili mbovu; kiburi, n.k. Hiyo MHA ("Kigezo cha Hitilafu") kwa kifupi ni kipengele cha hali ya uanadamu kinachohitaji maelekezo, ushauri, kuhimizwa, au kufarijiwa na Andiko.

B. ***Kuelezea na kutolea mfano kifungu***

1. Kuelezea kifungu. Kuelezea kunahitaji mhubiri kusimulia matokeo ya kufundishwa kiusahihi na kupania, kwa jinsi ya kueleweka na ya kukumbukika, kwa washirika. Kuelezea andiko kwaweza kuwa kufanyika kwa matokeo makubwa kwa njia kama: (a) *Kutaja kweli za mstari* (m.y; kuelezea mstari unamaanisha nini); (b) *kuweka kweli za mstari* (m.y; kuonyesha ni wapi katika mstari, ulilipatia wazo hilo); na (c) *kuthibitisha kweli ya mstari* (m.y; kueleza upya, kuhadithia, kutoa maelezo, kusimulia, kueleza maana yake, na kujadili ili kwamba ushirika wako uelewe kwa nini mstari unamaanisha hicho unachosema unamaanishaC uthibitisho wa namna hiyo unaweza kuwa unajidhihirisha wenyewe, au sivyo, kulingana na mstari husika) (Chapell 1994: 116-24).

2. Kuonyesha mfano wa kifungu. Wahusika wote, mhubiri na wasikilizaji huishi mbali kabisa, ki-wakati, mahali, na desturi zilizoko kwenye dhana ya Biblia. Mifano ni simulizi, mifano, matukio ya maisha, au vitu vingine vinavyoonyesha, kujenga, kueleza, au vinginevyo; huwezesha wasikilizaji kujifananisha na hali iliyomo katika kanuni ya ki-Biblia au mstari ambao unaelezewa. Mifano hugeuza ukweli ambao hauonekani wazi na huufanya halisi zaidi. Kama ambavyo mwalimu moja wa utoaji wa hotuba za kadamnasi anavyoliweka: "Hili ndilo daima kusudi la mnenaji: ni kuleta hoja yake wazi kwa wasikilizaji, kufanya yasiyo dhahiri kuwa thabiti, na hivyo halisi." (Buckley 1988: 15). Mifano hupanua na kuleta kina kwenye uelewa wetu wa mstrari. Inaweza kutolewa kutoka kwenye chanzo chochote: gazeti au kitabu, desturi ya kimila au tabia, jambo lililotokea, tukio fulani, au mambo mengine katika jamii ambayo yanajulikana na washirika hao; tukio katika maisha ya mhubiri mwenyewe; mkondo wa tabia za kiasilia; siasa; michezo, mila na desturi,

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

historia, televisheni; radio, sinema, mfano kutoka mahali fulani katika Biblia; kwa kifupi, kitu chochote ambacho washirika wanaweza kukielewa ambacho kitawasaidia kuweka wazi kweli ya Neno la Mungu. Kutumia visa vya kiasilia na mazoea na mithali zake hufaa sana katika jamii zisizo za ki-Magharibi ambako simulizi za hadithi ni jambo la kawaida, muhimu, na, pia hutarajiwa kuwa ndiyo njia ya kuelezea kweli. Yesu aliishi katika desturi za namna hiyo, na mara kwa mara alitumia simulizi na mithali kuelezea au kupeleka kweli za kiroho.

3. Mifano na maelezo pamoja: Mifano mizuri ni ya lazima kwa watu ili kupata kweli za ki-Biblia, lakini hazitoshi pasipo maelezo: "Kwa kuweka msingi wa kweli za Biblia kwenye hali ambazo watu wanazielewa, mifano huunganisha kweli za Biblia na matukio yaliyojitokeza, na, kwa kufanya hivyo, hufanya Neno lifikike, lieleweke, na halisi katika namna ambazo haziwezekaniki kwa kutumia kauli za maneno stadi tu. . . . Wasikilizaji wanaokutana na mafikirio ya dhanaChata kupitia wengine—kihalisi hujifunza zaidi kuliko wale ambao lazima wazingatie maneno na mawazo katika fikira tu. Kile wahubiri walichokijua kwa silka tu vizazi kwa vizazi kina msingi imara wa kisayansi. Wazo lenye maana husitawi linapokuwa limefungana na ukweli. Ugunduzi huu unafunua thamani iliyofichika ya maelezo. Wasikilizaji kimsingi huelewa kiundani zaidi na kwa upana zaidi tunapoonyesha kweli za Biblia katika jinsi ya matukio yanayotambulikana [Kulingana na mifano ya Yesu (**Marko 4:34**)] Ni mpaka maelezo yaendane na mfano, vinginevyo yanabakia kutokueleweka. Mifano au mithali pekee hutangaza kweli ya Biblia. Kipawa cha Maandiko kiko katika muunganiko wake kati ya mfano na kiungo ambacho sehemu zote mbili za ufafanuzi zinafunua na kuimarisha kweli za kingine." (Chapell 1994: 166, 173, 175n.39)

VI. Kutumika Kwake

A. *Mabadiliko ya maisha ndiyo lengo la mahubiri ya ufafanuzi*

"Lengo la Maandiko yenyewe siyo tu kutoa habari kuhusu Mungu, lakini ni kuwabadilisha watu wamfananie Yesu Kristo" (Chapell 1994: 45). Kwa vile Maandiko yote yameandaliwa ili kuwaandaa watu wa Mungu kwa ajili ya kazi aliyowaandalia (**2 Tim 3:16-17**), Mungu hutegemea tushughulikie matatizo (m.y, ile MHA) kwamba Roho yake na Neno lake linafunuliwa kwetu. Zaidi ya hapo, ushirika una haki ya kumuuliza mhubiri, *"Kwa nini ulinieleza yale yote?"* na kusema ule ujumbe, *"naelewa unafikiri nini—lakini ili nini—natakiwa kufanya nini kuhusiana na hayo?"* Mwandishi wa utafiti wa CTS anaelezea "Jaribio la tindikali la mamlaka ya ujumbe": "'Unakuwa na mamlaka ikiwa baada ya mimi kusikia, najikuta mwenyewe nikitenda kile nilichokisikia. Hayawezi kuwa na mamlaka mpaka hilo litendeke kwanza.' Wahubiri, ndipo wanaweza kupima mamlaka ya mahubiri yao kwa kiwango ambacho kwamba, kadiri wakati uendavyo, washirika wanaanza kutenda dhana kuu za jumbe walizosikia kutoka Jumapili moja hadi nyingine. Ongezeko la mabadiliko ya maisha linalohusiana na Injili linaweza kujipenyeza chini kiupana hadi kwenye jumuiya kubwa zaidi, kwa mategemeo kuwaongoza wengine kumkiri Yeye ambaye kwa jina lake na mamlaka yake, mtumishi anamhubiri." (Allen 2006: 74) Katika Utafiti wa GASS, ingawaje wahubiri wengi walisema kwamba "badiliko" la maisha lilikuwa ndilo lengo lao katika kuhubiri, hakuna msikilizaji aliyetaja hilo kama ndiyo sababu ya usikilizaji wao (35% waliorodhesha "kutiwa moyo; 30%—kuhusisha kimaisha; 21%—taarifa; 14%—uelewa): "Hata hivyo, wazo lingeweza kudhanika kuwa, kwa vile asilimia 35 ya wasikilizaji wanataka kutiwa moyo na wengine asilimia 30 wanataka kuhusisha kimaisha—mahubiri ya kutia moyo yenye mapendekezo ya kuhusishwa na maisha, yangeweza kuchochea shauku la badiliko katika Ingawaje wasikilizaji waliofanyiwa utafiti hawakuorodhesha lengo la usikilizaji wao kuwa 'Nataka kubadilika,' pale watafiti wa wasikilizaji walipouliza swali, 'Nini hasa ni mwitikio wako wa ndani kwa mahubiri yaliyo mengi?' Asilimia 14 ya wasikilizaji waliarifu kusema mwitikio wao wa ndani kabisa ni 'utayari wa kubadilika.'" (Carrell 2000: 151)

B. *Katika Biblia nzima, kweli za mafundisho huambatana na matumizi ya utendaji wake ambapo huthibitisha kile kweli inavyotakiwa kuonekana na jinsi kweli ile inatakiwa iwekwe katika maisha*

"Biblia siku zote huunganisha mafundisho na matumizi yake" (LeBar and Plueddemann 1995: 141). Kwa mfano, manabii katika Agano la Kale waliunganisha Neno la Mungu la maonyo na hukumu na kuwaagiza watu wao watubu na kubadili njia zao za kuishi. Yesu alifunua tabia ya Mungu, mwenyewe, na ufalme wa Mungu, na kuelezea jinsi tunavyotakiwa kuishi kuhusiana na ufunuo huo. Nyingi ya nyaraka ziliandikwa kushughulikia matatizo maalum au maswala yaliyowakabili washirika wa mahali. Waandishi wa nyaraka kimsingi walianza nyaraka zao kwa kuelezea mafundisho yao, na kisha wakaeleza mafundisho hayo yanavyohusu uhitaji wa maisha ya wafuasi wa Kristo.

C. *Matumizi huletea ufafanuzi maana*

Ni kule kuishi, kutenda, na kutumia zile kweli za Maandiko ndiko kunakoonyesha kuwa mtu anaelewa au haelewi kiukweli anayo imani halisi, inayookoa (ona, k.m, **Math 7:16-21; 28:20; Yohn 14:21, 23; 15:10; Yak 1:23-**

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

25; 2:14-26). Kwa hiyo, ujumbe lazima uunganishe matumizi kwenye ufafanuzi wake: "Maana halisi ya mstari hubakia umefichika, mpaka tutakapoelewa jinsi kweli yake itakavyotawala maisha yetu Usianze kuandika ujumbe pasipo kujua ujumbe unatakiwa kuleta nini. Matumizi lazima yatangulie maamuzi ya mwisho kuhusu muundo, maneno yake, na hata ladha ya ujumbe, vinginevyo mhubiri atakuwa anaandaa barabara kuu isiyo na mwisho *Utekelezaji kimatendo huleta maana iliyokusudiwa katika ufafanuzi. . . .* Hii inamaanisha kwamba, ni mpaka wahubiri watakapoweka utekelezaji wake, ufafanuzi wao utabaki kuwa haujakamilika." (Chapell 1994: 78, 202-03) Kusema ukweli, mwalimu moja wa Kikristo Lois LeBar anahitimisha, "Yakobo 4:17 huweka bayana kwamba kujua na kutenda ni hatua mbili tofauti. Tunapowafundisha watu kweli mpya pasipo kuzitumia, tunawafanya wao wadhambi zaidi kuliko walivyokuwa mwanzoni." (LeBar and Plueddemann 1995: 99)

D. ***Matumizi kimatendo kwaweza kuwa ni mabadiliko katika mtazamo pamoja na mabadiliko katika tabia***

Pasipo badiliko katika mtazamo—kuamini, msukumo, kujisikia—mwito wa kubadili tabia unakuwa ni uhalali wa kimorali tu. Matokeo yake, kutambua mtazamo ambao unatakiwa kubadilishwa (kiburi, upendeleo, ubinafsi), kuhimiza badiliko jema la mtazamo (kufurahia, imani, kumtumaini Mungu katikati ya mazingira magumu), au kuimarisha msimamo wa imani uliokwisha kuufanya (kung'ang'ania uhuru wa msamaha, kujituliza katika kweli za ufufuo, kupata matumaini upya kwa kutegemea ukuu wa Mungu), ni utekelezaji halali na muhimu zaidi ya kuagiza mabadiliko ya tabia. Kuwafanya watu wafikirie kwa njia mpya—k.m., "Kuwahimiza washirika waelewe kuwa kuna haja ya kubadilika," "kuwasaidia watu kuona vitu ambavo hawavielewi bado," na "Kuwasaidia kuona jinsi dunia inavyoonekana kwa watu walio tofauti na wale walio katika ushirika"—ni njia muhimu ambazo jumbe zinawaongoza watu kubadilisha njia zao za kimaisha (Allen 2008: 63, 67).

E. ***Wahubiri wasidhanie tu kuwa kule kueleza au kuonyesha kile Biblia inachosema na maana yake, watu wataona mara moja jinsi ya kutumia kweli za Kibiblia maishani mwao***

Tatizo la msingi kwa "matumizi" ya jumbe zilizo nyingi ni kwamba *hazina uelekeo rasmi na si za kutendeka vya kutosha.* Katika utafiti wa wachungaji 206 na washiriki wa makanisa 2,233, "kimtazamo wasikilizaji wachache zaidi kuliko wachungaji walisema jumbe zilikuwa zinahusu 'kushughulikia maswala ya maisha binafsi'" (Reed 1999: 84). Wahubiri huelekea "kuvuka juu ya" matatizo na maswala halisi ya maisha pasipo kuyaelezea moja kwa moja (Reed 1999: 84; Allen 2005: 371-72). Bila shaka, wahubiri lazima wawe wazi na dhahiri zaidi, na *kutoa jinsi ya utekelezaji* ambavyo watu wanahitaji. Kama Chapell asemavyo: "Matumizi yanalenga matokeo ya ujumbe mzima kuhusu (ma)badiliko ayatakayo Mungu kwa watu wake. Huu si wakati wa kutafuna maneno au kuamua kutojali. Matumizi kamili ya moja kwa moja *pasipo kupiga chenga—katika upendo.* Kutoka madhabahuni, sema hasa kile unachomaanisha kama jinsi ambavyo ungemwambia yule umpendaye sana. Vita vya kiroho vya wengine vinakuhitaji usifiche maana yako kwa kutoa maelezo ya mawazo yasiyo wazi, ambayo hayamsumbui yeyote na hayana uelekeo wa kukuingiza katika matatizo Kama kanisa halitapona mpaka kusengenyana kukome, useme hivyo. Ikiwa utofauti wa kisiasa unawagawa waamini, lieleze tatizo hilo. Sema kwa uangalifu. Sema katika upendo. Lakini usiache kusema kinachotakiwa, na Biblia inachotaka." (Chapell 1994: 223)

F. ***Ili kuhakikisha kutumika kwake kunalengwa zingatia maswali mawili ya muhimu sana***

1. <u>Watu wanatakiwa kufanya nini?</u>

   a. *Matumizi kiutendaji yanatakiwa yawe na msingi ambao mstari unasimamia.* Maelezo ya mstari yanapaswa yajenge umuhimu wa kanuni ambazo utendaji unahusika. Hii ni muhimu kwa sababu wasikilizaji walio wengi "huweza kupangwa kwenye kundi la 'kutojali' 'badiliko' linalolengwa na mhubiri kwani hawahudhurii wakiwa na matarajio kuwa watabadilishwa" (la wahubiri Carrell 2000: 151). Wasikilizaji lazima waweze kuamua: "Ni lazima tufanye hivi kwa sababu ndivyo Biblia inavyosema." Hii ni muhimu sana kwa sababu utendaji—ambao, kwa tafsiri, unahusu mabadiliko katika mtazamo au tabia—ni mahali ambapo wasikilizaji wanaelekea *kumpinga* mhubiri au ujumbe. Hii pia ndiyo sababu uchambuzi sahihi na maelezo ya kifungu cha ki-Biblia lazima yawe sahihi⊂wakati uchambuzi sahihi na maelezo yanapokuwa sahihi, ndipo utendaji unaibuka kutoka kwenye kifungu hicho (na kuonekana na watu kufanya hivyo), ndipo uchambuzi sahihi na maelezo, na matumizi kiutendaji vitakwenda kukamilishwa kwa mshikamano.

   b. *Matumizi kiutendaji uwe maalum⊂na mhubiri anapaswa atoe mifano maalum ya jinsi ya kufanya kile kinachotakiwa kufanyika.* Kuwahimiza watu "kuwapenda jirani zao" siyo matumizi kiutendaji. Kuwapenda jirani ni kanuni ya kijumla tu, inayojulikana sana na ushirika mzima. Inaanza kuhama kutoka kanuni ya ujumla na kuwa ya matumizi kimatendo pale mhubiri atakapotaja hali maalum zilizopo sasa ambazo wasikilizaji wanakabiliwa nazo ambazo wanatakiwa kutekelezea kanuni hiyo ya ki-Biblia (k.m, kumpenda jirani anayekipenda chama tofauti cha siasa, aliye na watoto wenye chuki,

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

anayeicheka imani yako; aliye wa kabila au ukoo mwingine). Hata hivyo, kusema hivyo peke yake hakutoshi. Mhubiri anahitaji kutaja matendo maalum ambayo yanaonyesha upendo wa namna hiyo ukoje (k.m, kuamua kukaa na mtoto huyo msumbufu kwa muda ili kumpumzisha mama yake mzigo, kuonyesha aina fulani maalum ya wema kwa jirani; kumwalika huyo jirani kwa chakula cha jioni). Mhubiri anatakiwa kutoa mifano maalum ya jinsi *aina mbali mbali za watu katika usharika* (vijana; wazee; watu waliooana; wanaume; wanawake) wanavyoweza kutumia kanuni hiyo ya ki-Biblia maishani mwao. Zaidi ya hapo, "kusikia simulizi za watu halisi [kuchanganya na za mhubiri mwenyewe] waliojisikia kutenda au kufikiri kitofauti, husaidia kuletesha mikondo mipya ya mawazo na tabia" (Allen 2008: 66).

c. *Matumizi kimatendo yanatakiwa yawe kiuhalisi.* LeBar anatukumbusha juu ya kweli muhimu: "Kwa asili huwa tunakataa badiliko kwa vile linamaanisha mpangilio mpya wa muundo wa nafsi ambao tumekuwa tukiujenga. Ni rahisi zaidi kuendelea na mkondo wenye upingamizi mdogo kuliko kupangua mitiririko ya zamani ya kufikiri na utendaji. Ikiwa mtu amehitajika afanye mabadiliko mengi mno mara moja, huzidiwa kimawazo." (LeBar and Plueddemann 1995: 175) Kwa hiyo, uwe mwangalifu kutowaagiza washirika wako kubadilisha mno maisha yao. Jaribu kutafuta kitu ambacho kila moja anaweza kukifanya—na weka mapendekezo maalum kwa makundi yaliyoko ndani ya wasikilizaji hao (vijana, wazee, waamini, wasioamini, nk.). Stanley anapendekeza yafuatayo, "Ninapowaagiza wasikilizaji wafanye kitu fulani maalum, mara nyingi huwa nawaomba wajiwajibishe katika hilo, kwa muda fulani maalum. Kufikia nusu ya mfululizo wa mafundisho ya sala ya Bwana niliwaagiza washirika kuanza siku saba mbele yao kwa sala. Ni siku saba tu. Mtu yeyote angeweza kufanya hilo. Na bila shaka hizo siku saba zingeanzisha tabia fulani." (Stanley and Jones 2006: 189) Kumbuka, unajaribu kubadilisha tabia za watu. Ni kama kujaribu kuondoa magurudumu ya mkokoteni ambao una kutu sana—si rahisi, na huhitaji muda na marudio. Hata hivyo,tabia moja mpya ya mawazo na matendo huwa imeanza; pole pole wataanza kuelewa kwa kina kadiri wakati uendavyo na marudio.

d. *Katika matumizi kiutendaji ni lazima tuhakikishe kuwaelekeza wasikilizaji wetu rasilimali walizo nazo katika Kristo Cunyenyekevu katika kutii, maombi, Neno lake, mfano wake, Roho, kutumainia utoaji wake, kutendea kweli zake Ckuwawezesha kufanya mabadiliko wanayoyahitaji katika maisha yao.* Wahubiri lazima wawe waangalifu kutokutoa "vivutio vya uelekeo wa uanadamu kuonyesha mafanikio zaidi kimwili" (Chapell 1994: 210). Ni "duni kikristo" kuwaambia wasikilizaji kiurahisi tu "Wawe kama [Musa, Gideon, Daudi, Daniel, au Petro]," "muwe wema," au "muwe na nidhamu" ambako "kunaonyesha kuwa tunao uwezo wa kubadili hali yetu ya anguko kwa nguvu zetu wenyewe" (Ibid.: 267-68, 280-86). Kuhubiri kile watu wanavyotakiwa wawe au wafanye, pasipo kumtaja Kristo, anayewawezesha kuwa, kunapotosha Injili—na ikizidi itazaa washirika wa Kifarisayo.

e. *Matumizi kiutendaji yanatakiwa yatumie rasilimali za kanisa.* Utafiti wa CTS ulionyesha kwamba, "wahubiri hawawezi kutegemea washirika kudilika mawazo na matendo kwa mwitikio wa kuhubiri ujumbe moja. Wahubiri kimsingi wanatakiwa kuelewa kuwa ujumbe moja, hutenda kazi na jumbe zingine na sehemu nyingine za mfumo wa ushirika [kuletesha mabadiliko ya maisha]." (Allen 2008: 74) Angalau mambo mawili yanaweza kusaidia:

(1) Elekeza watu wako kwenye rasilimali zilizopo katika kanisa na jumuiya. Ikiwa kanisa linatenda kazi kama linavyotakiwa, na kama mhubiri anawajua watu wake vizuri (vikiwamo vipawa na rasilimali zao), hao walioko katika parishi wanaweza kuelekezwa kwa walio katika mwili wa Kristo ambao watawasaidia wabadilishwe kumfanania Kristo. Hata kama kanisa halina huduma maalum za kuwasaidia wana parishi hiyo, kijiji au jumuiya inaweza kuwa na rasilimali hizo.

(2) Majadiliano ya vikundi vidogo vidogo. Makanisa mengi yanatumia vikundi vidogo vidogo (vya seli) vinavyokutanika kati kati ya juma. Makanisa mengine hata yana vikundi vinavyoshughulikia maswala yaliyoibuliwa kwenye ujumbe mara baada ya ibada kwisha. Vikundi hivi vinaweza vikajadili kuhusu ujumbe wa juma, hasa kukazia mwonekano na jinsi ya utekelezaji. Majadiliano ya vikundi vidogo vidogo ni njia muhimu ya kuwafanya watu washughulikie "kuwafanya wahusike" na ujumbe. Watu walio katika kikundi wana matukio na ufahamu unaotofautiana, unaoweza kuwasaidia wengine, na maswali kuhusu ujumbe yanaweza kujibiwa. Mortimer Adler anatueleza kwa nini majadiliano kama hayo ni muhimu sana: "Hasa ni kwa sababu hotuba isiyovurugika na usikivu wa kimya ni mgumu zaidi kuifanya vizuri kuliko kuandika na kusoma, yote hufanyika kufaa zaidi wakati ujumbe wa maelekezo unafuatiwa na mazungumzo ya kubadilishana—kwa kuongea au kujadiliana, kwa maswali na majibu, kwa jinsi ya kukaa pamoja ambapo mnenaji na msikilizaji wanaweza

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kubadilishana mawazo Itokeapo hotuba haikuandamana na majadiliano yanayomsaidia mnenaji kuhakikisha kuwa mawazo ya wasikilizaji yamefikiwa na kuguswa, na kama usikilizaji haukufuatiwa na kusoma pasipo kile kinachoweza kutimizwa kwa mjadala, basi hotuba inakuwa njia duni kuliko zote za kufundishia." (Adler 1983: 52)

2. Kwa nini wanahitaji kufanya hivyo?

a. *Tunahitaji kutoa msukumo unaotakiwa.* Matendo mazuri yakifanywa kwa sababu zisizo sahihi huweza kuwa si lolote zaidi ya uhalalishaji na unafiki. Badala yake, Ukristo unalenga maisha yaliyobadilishwa kutoka "ndani-nje" (ona **Warum 12:1-2**). Maisha yaliyobadilishwa kwa ndani kutaleta tabia iliyobadilishwa kwa nje. Ufunguo muhimu ni kuwaonyesha wasikilizaji kwa Kristo pia upendo na neema ya Mungu. Hatimaye, swala ambalo wahubiri wote lazima walikabili ni: je tunatakiwa tuwe watakatifu *ili kupata* kukubaliwa na Mungu, je tunatakiwa kuwa watakatifu *kwa sababu* ya kukubaliwa na Mungu? *Kuhukumiwa dhamiri* humsukuma *mkosaji* kwenda msalabani, lakini kwa *mwamini* uelewa mzuri wa *neema* ya Mungu unatakiwa ubadili kila kitu kuwa cha msukumo wa *shukurani*: "Itokeapo waamini wanaona kwamba maandiko yote—mfululizo wa ufunuo wote∁ni jukwaa la kuonyesha neema, mioyo yao huitikia kwa kicho na unyenyekevu. Miitikio kama hiyo huweka uwanja wa kuabudu na utii katika shauku zilizo sahihi na kufanya utekelezaji wa kweli zote za ki-Biblia kuwa tunda la shukurani, kusifu, kufurahia wema, na ibada ya upendo. Mahubiri yamwekayo Kristo kuwa kitovu hayaweki kando mwenendo wa kawaida wa Ukristo, bali zaidi, huonyesha chanzo chao katika ile nguvu isukumayo ya neema. Sheria za utii hazibadiliki, bali sababu ndizo zibadilikazo." (Chapell 1994: 302)[1]

b. *Tunahitaji pia kutoa msukumo wa watu kuishi kwa jinsi kifungu kinavyosema wawe.* Toa mifano kutoka kwenye maisha yako mwenyewe au kutoka kwenye maisha ya wengine, au ya makanisa, au jamii nzima, ambako badiliko lilitokea. Kuelekea mwisho wa jumbe zake, Stanley anajaribu kutupa maono au "kutoa picha ya kimaneno ya kile kinachotakiwa na kiweje. Katika muda huu wa kumaliza, ulizaa wasikilizaji wako kufikiri jinsi kanisa, jamii, familia, hata pengine dunia ingekuwaje kama Wakristo kila mahali wangelitekeleza hilo wazo jipya." (Stanley and Jones 2006: 129). Hilo linawavuvia watu kujaribu kufanya mabadiliko ambayo Maandiko na ujumbe unaagiza.

VII. Sifa na Mpangilio wa Jumbe Zenye Ufanisi

A. *Ili kuwa na ufanisi zaidi, ujumbe unapaswa uwe na hoja moja, inayobeba ujumbe wote*

1. Kwa vile *lengo* ni mabadiliko ya nafsi, *njia ifaayo zaidi* ni kuwa *na hoja moja*, siyo hoja nyingi, kwenye ujumbe wako. Hoja hiyo moja inatiririka kutoka *lengo kuu la kufikiwa* moja, lililo wazi, ambalo unataka wasikilizaji wako walifikie∁m.y, wazo maalum unalotaka kuliwasilisha; mambo maalum unayotaka yakamilishwe; kitu kimoja wanachotakiwa kukijia na wanatakiwa kufanya nini kuhusu hicho; ile sehemu ya mwisho ya utekelezaji na mabadiliko ya maisha. Stanley analiweka hilo namna hii: "Nisemapo *hoja* ninamaanisha moja kati ya mambo matatu: Matumizi kiutekelezaji, uelewa, au kanuni. Kwa njia hii, kila ujumbe unapaswa uwe na wazo moja kuu, matumizi kiutendaji, uelewa wake, au kanuni ambayo hufanya kazi kama gundi kushikamanisha vingine pamoja" (Stanley and Jones 2006: 103). Ukishakuwa na hilo vizuri akili mwako, kila kitu katika ujumbe kinapaswa kilengwe katika kuimarisha, kueleza, na kufanya hoja hiyo ikumbukwe. Kama Stanley asemavyo, katika ujumbe "tunawachukua watu kwenye safari [kuelekea maisha yaliyobadilishwa]. Ukishajua unakokwenda, uumiliki mwisho huo kwa wasikilizaji wako ili kuifanya njia safi na iliyonyoka kabisa. Hiyo inamaanisha kwamba unavikatilia mbali vitu visivyoendana na somo." (Ibid.: 109-10)

2. Ukishagundua hoja yako na kujenga ujumbe wako kwenye hilo, hatua inayofuata ni kuunda sentensi moja au msemo unaoweza kunasa. Mungu anasema nini kwa kanisa kupitia kile walichoandika waandishi wa Biblia? Utakapogundua hili, ulifinyange liwe, kauli rahisi, iliyo *katika sentensi* moja ya hoja kubwa ya kifungu—m.y., kitu kimoja unachotaka watu wako kukumbuka na kutoka nacho kutoka kwenye mahubiri. Hicho ndicho *kichwa* (ona **Dibaji B, kifungu IV.B-E**). Kiurahisi weka, wito wa mahubiri hayo kuwa *kauli iliyo wazi, yenye nguvu ya msukumo mkuu wa kifungu* kuendana na washirika walivyo. Kauli hiyo rahisi hufupisha kile unachoamini Bwana anataka wewe useme kwa washirika kutoka kwenye kifungu hicho unachokihubiri.

[1] Utofauti wa msukumo utokanao na Mungu/neema na msukumo utokanao na mwanadamu/ dhamiri kwa utii ni wazi kabisa: "Upendo unaposukuma, ndipo Bwana, makusudi yake, na utukufu wake unakuwa lengo letu. Pasipo hili, hakuna utekelezaji utakaompa changamoto mwamini kutumikia chochote kikuu zaidi ya ubinafsi." (Chapell 1994: 209)

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Sehemu zote za kifungu zinapaswa zijenge kuelekea kweli hiyo, zibubujike kutokea hapo, au zihusiane na hilo katika namna iliyo dhahiri. Kinapaswa kiwe kinakumbukika kwa urahisi. Hilo litakusaidia wewe na pia wasikilizaji wako. Kama kitakuwa kifupi na kinakumbukika, basi kitakuwa rahisi kwako kukigusia kila mahali wakati wa ujumbe wako. Kama ni kauli iliyoundwa vizuri, itakuwa dhahiri zaidi kwa wasikilizaji wako kwamba hiyo ndiyo hoja yako. Kwamba kichwa hutajwa kimsingi mwanzoni mwa ujumbe. Utofauti unaweza kuwa wakati unahubiri kifungu cha kusoma tu na kufuata ambukizo na simulizi ya kisa kutoka katika mstari huo.

3. Lengo linalounganisha ni la lazima kwa sababu angalau tatu hivi:

a. *Mstari wenyewe unadai kukaziwa.* Lengo na kusudi *la mstari* lazima liwe lengo letu tunapolifafanua andishi. Kama Chapell asemavyo, "Maana ya kifungu ndiyo maana ya ujumbe" (Chapell 1994: 23). Kuna mtiririko wa kimpangilio kwa jinsi waandishi wa Biblia wanavyowakilisha mambo. Biblia yenyewe inatoa simulizi kamili, inayojitosheleza. Hata kama mawazo katika kitabu fulani yanaonekana kama hayahusiki, kuna kusudi kubwa zaidi, au mshikamano nyuma ya kunachosemwa ambacho msomaji anayefahamishwa anaweza kugundua. Matokeo yake, jumbe zetu zinapaswa zionyeshe mshikamano wa mstari. "Ingawaje mawazo mengi na sehemu nyingi hufanyisha ujumbe, vyote hivyo vichangie kwenye lengo. Ujumbe ni kuhusu kitu kimoja" (Ibid.: 38).

b. *Wanenaji wanahitaji kitovu cha lengo.* Maandiko yana kina sana na ni magumu kueleweka. Tunzi nyingi zimeandikwa kuhusiana na kila mistari husika. Hata hivyo, jumbe zisizo na lengo maalum, zinazotanga-tanga hazitoi maelezo yakufaa. Mshikamano wa lengo mwanzoni unaweza kuonekana finyu, lakini hasa huwapa uhuru wahubiri wasinaswe katika wavu wa uwezekano ambao vifungu mbali mbali hutoa: "Kufikia wakati umemaliza kuhubiri ujumbe wako, utajua kikamilifu nguvu ya ujumbe iko wapi; utajua wapi penye "a-ha". Kufikia mwisho wa kuandaa, unajua sehemu ya ujumbe wako ambayo inakusisimua zaidi. Kwa maneno mengine, unajua *jinsi* ya kupata hoja kuu.Unajua *lini* umeipata hiyo hoja kuu. Kile unachohitaji kukazia macho ni kujenga kila kitu kuzungukia hilo." (Stanley and Jones 2006: 105)

c. *Wasikilizaji wanahitaji kitovu cha mkazo.* Kusikiliza si kama kusoma, ambapo kifungu kinaweza kurudiwa tena kusomwa kama hakikueleweka mara ya kwanza. Wasikilizaji huchoka haraka wasumbukapo kutafuta mnenaji anaelekea wapi katika maneno yake. Hata hivyo, ujumbe uliojengwa kuzungukia wazo moja ni rahisi kuufuatia. Wasikilizaji watasahau haraka orodha ya hoja. Ni rahisi zaidi kukumbuka hoja moja kuliko hoja nyingi—ikiwa hoja hiyo iko wazi, inayokumbukika, ikarudiwa, na "kuletwa mazingira" ya kwao. Usikivu wa wasikilizaji na uelewa unaweza ukasaidiwa kupitia marudio na maswali ya udadisi:

(1) Marudio. "Marudio yanahitajika kikamilifu kwa sababu msikilizaji hawezi kugeukia kitu kilichotajwa awali na kukisikiliza tena. Hotuba huwa inasonga mbele tu daima, na mnenaji lazima arudie kitu alichokisema mwanzoni, ili msikilizaji awe nacho akilini kwa lengo la kuelewa hoja itakayojengwa baadaye." (Adler 1983: 65)

(2) Maswali ya udadisi. Wakati wa ujumbe unaweza kudumisha usikivu wa wasikilizaji na mkazo wao kwa kuwauliza na kujibu, maswali ya udadisi (k.m., "Kwa nini?"; "Kwa nini panasema hivi?"; "Nini kinaendelea hapa?"; "Je anatuambia nini?"; "Hili linatuhusuje sisi katika maisha yetu leo?").

4. Kuwa na hoja moja ya mkazo katika ujumbe huonyesha tofauti moja kati ya mahubiri na kufundisha: katika kufundisha, mtu anaweza kugusia vipengele vingi vya mstari; kitovu cha mahubiri huhakikisha kwamba kila kitu kimeelekezwa kwenye mwisho moja. Mshikamano wa ujumbe humpa mhubiri uwezo kukazia kwenye somo kwa kina. Ikiwa kuna maswala mawili au zaidi yanayojitokeza katika kifungu unachokisoma, usitumie ujumbe moja ili kukamilishia hoja zote. Badala yake, zitunze kwa ajili ya wakati ujao, au fanya jumbe fupi-fupi za *mfululizo* za kifungu hicho, na kutoa hoja moja kila ujumbe moja. Katika maandalizi yako, changamoto huenda haitakuwa *kutafuta* hoja moja ya kukazia, bali *kupunguza* zile mbili au tatu ambazo ungetaka kuzitoa pia.

B. ***Mawasiliano yenye kushawishi hurahisishwa na mpangilio ulio wazi***

1. Umuhimu wa mpangilio ulio wazi. "Mpangilo na utaratibu wa kile usemacho ni njia ya ushawishi kuhusu nini useme" (Stern 1991: 199, 203, 205). Katika Utafiti wa GASS, "Asilimia Ishirini na nane ya wasikilizaji walitaja mahubiri mazuri kuwa ni yale yaliyopangilika vizuri. Kwao, mahubiri yaliyopangilika vizuri ni pamoja na kutabirika, kutokana na maandalizi ya mhubiri . . . kueleweka . . . na mahusiano ya dhati kati Andiko na hoja muhimu za mahubiri [Kwa upande mwingine] asilimia arobaini na saba ya wasikilizaji wanasema mahubiri mabaya ni yale yasiyo na mpangilio. Sifa ya msingi ya *kutokuwa na mpangilio* ni neno

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

'kuchanganya,' lililorudiwa mara kwa mara kutoka kwa wasikilizaji. Wanasimulia mahubiri marefu yanayochukua mudamwingi (kwa maelezo au kuwa na uelekeo usioendana na lengo) muda mrefu baada ya hoja kuwa imeshatajwa, au mahubiri yenye hoja nyingi mno hadi hoja muhimu inakuwa ngumu kuitambua. Anasema msikilizaji mojawapo, 'Sijui, hata kama anaielewa hoja yake muhimu, na angeisema katika sentensi moja.' Kama kauli mwenza, wasikilizaji husimulia mahubiri yasiyo na mpangilio kama yale yasiyo na uhusiano wa wazi na Maandiko." (Carrell 2000: 92-94) Hoja kuu moja, mkazo wa urahisi wake badala ya ugumu wake, na mpangilio, yote hayo yataleta *kueleweka.* Kueleweka ni muhimu mno katika ushawishi. Pasipo kueleweka, wasikilizaji wanachoka upesi kuhangaikia kufuatia mnenaji anasema nini, na anaongoza wapi. Katika kueleweka, wasikilizaji wataendelea kumfuata mnenaji, na watakuwa katika hali ya kuelewa zaidi, kukumbuka, na kutekeleza yale unayowaambia. Unapaswa uonyeshe mpangilio wako mapema katika ujumbe wako kwa njia ya *mpangilio wa hoja kuu.*

2. Mpangilio wa hoja kuu unakusaidia kupanga ujumbe wako na kuwasaidia wasikilizaji wako waelewe uko wapi. Mpangilio wa hoja kuu kimsingi, ni kiongozi cha barabara yako unayoitumia kuwaonyesha watu wako wapi utakakowapeleka katika mahubiri yako. Kwa maneno mengine, huo mpangilio wa huja kuu unawatahadharisha wasikilizaji jinsi unavyopanga kujenga wazo la kichwa cha mjadala (ona **Dibaji B, kifungu IV.E-G**). Katika mpangilio wa hoja kuu unawapa wasikilizaji wako wazo fulani la maeneo muhimu utakayoyagusia, na utaratibu utakavyogusia maeneo hayo. Kama ilivyotajwa awali: *wasikilizaji* wanahitaji kitovu cha mkazo. Wanachoka haraka sana kuhangaika kumtafuta mnenaji anaelekea wapi na anasemea nini. Mpangilio wa hoja kuu huwapa mkazo unaolengwa. Hutumika kama alama kwa wasikilizaji ya jinsi maelezo yako yatakavyoendelea. Unavyohama kutoka sehemu moja ya mstari wa biblia kwenda sehemu nyingine, unaweza kurudia ilivyosema sentensi yako ya mpangilio wa hoja kuu ili kwamba wasikilizaji waelewe wazi kabisa uko wapi. Kwa hiyo, kichwa cha mjadala wako, na mpangilio wa hoja kuu vinasaidia kuleta *uelewa wazi*, ambao pasipo huo ujumbe wako unakuwa haufai.

C. *Vipengele vitatu vya ujumbe mara nyingi husahauliwa, lakini ni vya muhimu kuleta ufanisi wa mfundisho yako: Utangulizi; Mchakato wa mabadiliko; na Hitimisho*

1. Utangulizi.

a. *Utangulizi unatakiwa kufanya angalau mambo matatu:* (1) *Kukamata usikivu wa wasikilizaji;* (2) *Kujenga uhitaji, tatizo, au mbano kihisia unaohitajika au unaopatikana kwa wasikilizaji;* na (3) *Tambulisha jawabu la ki-Biblia la swala husika, hitaji, tatizo, au mbano.* Stanley anaelezea kwa nini hilo ni muhimu sana: "Ikiwa tunatoa majibu kwa maswali ambayo hakuna mtu anayeyauliza, au tunajaribu kutatua mbano ambao hakuna yeyote anayebanwa nao, basi habari zetu zina uwezekano wa kuangukia masikio yaliyozibwa. Taarifa ambazo hazishughulikii hitaji linalosumbua, hupokelewa kama hazina maana yoyote. Zinaweza kuwa muhimu sana, lakini ikiwa wasikilizaji wetu hawaoni au hawasikii uhitaji wake, huonekana kama hazina maana. Hakuna yeyote anayeguswa. Wanaweza kukaa kimya tu hadi tunamaliza kuongea. Lakini hawataguswa Utangulizi wako unaweza kuwa ndiyo sehemu ya maana zaidi katika ujumbe wako. Ni sawa na mtu wa barabarani akipiga kelele kusema, 'Sasa twendeni!' Wawasilianaji wengi, hasa wahubiri, wana shauku sana kuingia katika kiwiliwili cha ujumbe wao [kiasi kwamba] wanatumia muda mdogo kuandaa utangulizi wao. Wanakiacha hicho kituo peke yake." (Stanley and Jones 2006: 153-54)

b. *Muda unatakiwa kutumiwa wa kuhakikisha kwamba wasikilizaji wanakuwa wamehusishwa—kwamba utakuwa unashughulikia hitaji ambalo wanalisikia hisia yake, na kuwa utakuwa unajibu swali ambalo wao wenyewe wamekuwa wanaliuliza.* Wanahitaji kujua *nini kimeandaliwa kwa ajili yao.* Stanley anahitimisha: "Karibu kila ujumbe ninaoutoa, huwa nasema, 'Jambo hili ni muhimu sababu hii.' Mara zote hueleza *kwa nini* mwisho wa utangulizi. Sasa kwa vile wanajua *wapi* tunakwenda, wanahitaji kujua *kwa nini* ninawachukua [wao] kule. Ukweli kwamba hayo yako katika Biblia inatosha kwa wengine, lakini haitoshi kwa walio wengi. Kujibu *kwa nini* kunakupa kichocheo kwa wasikilizaji wako kukufuatia sehemu inayofuatia ya ujumbe wako." (Ibid.: 187-88)

2. Mabadiliko.

a. *Wakati unabadilisha kutoka utangulizi wako kuelekea maelezo ya mstari, na kutoka mstari kuelekea changamoto kwa watu au hitimisho, unahitaji kuhakikisha kwamba wasikilizaji wako wanajua kuwa unafanya badiliko kuelekea hatua nyingine ya ujumbe wako.* Wasikilizaji watapoteza usikivu hadi hapo mhubiri anawapa "vishikizo" vya maneno ambavyo wanaweza kuning'inizia mawazo yao, usikivu, na uelewa. Kuwezesha wasikilizaji wako kujua nini kinafuata kunawasaidia kubaki nawe na kuwafanya waandamane na mawazo yako.

b. *Hata katika maelezo ya mstari, unapaswa uweke wazi unapofanya badiliko la mjadala wako kutoka*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

sehemu moja kwenda nyingine. Hiyo ni sababu moja ya kuwa na "sentensi ya mpangilio." Sentensi ya mpangilio huwa kama alama kwa wasikilizaji kuhusu jinsi maelezo yataelekea. Kadiri unavyobadili mjadala wako kutoka sehemu moja ya jambo kwenda nyingine, unaweza kurudia maneno kutoka senetnsi ya mpangilio ili kwamba wasikilizaji waelewe vizuri zaidi uko wapi.

c. *Marudio yanasaidia.* Jaribu kusema kitu kama vile, "Sasa, baada ya kujua yote hayo, tufanye nini? Kanuni hii inaonekanaje tunapojaribu kuishi kama isemavyo? Haya ni mapendekezo." (Ujue kwamba, katika mfano huu, usikivu wa wasikilizaji ulikuwa umekaziwa kwa kutumia swali la udadisi, na swali hilo la udadisi lilirudiwa mara mbili, kidogo kwa njia tofauti.)

3. Hitimisho.

a. *Watu huelekea kukumbuka kile unachowaachia*Cikiwa kitaachwa kwao kwa namna ya *kukumbukika, na ya kukamata.* Kwa hiyo, unahitaji kujua kikamilifu jinsi unavyotaka ujumbe wako uishie, na *kuandaa* hitimisho lako kupata mwisho unaokusudia.

b. *Hitimisho lako linatakiwa lilele liwe "wazo kuu," ile hoja yako moja, kuwarudishia wasikilizaji wako kwa jinsi watakayoikumbuka na watake kuitumia kimatendo maishani mwao.* Kumbuka kwamba lengo lako ni kuona maisha ya ushirika yanabadilika na kumfanania zaidi na zaidi Yesu. Hakikisha kwamba, pakiwapo hitimisho lililopangika vizuri, wasikilizaji wako wanafikishwa kituoni ambako ujumbe huu ulikusudia kufika.

D. ***Mambo ya kuzingatiwa katika mpangilio kwa ujumla***

1. Kila ujumbe unatakiwa ukidhi masharti angalau ya chini kabisa. Dr. Greg Scharf anayaita hayo yafuatayo kuwa ni "Vidokezo A-B-C vya ujumbe":

A—Je *unatumika?* Je ujumbe unaleta hali ya wahusika kujisikia unawahusu kimatendo?

B—Je ni wa *ki-Biblia?* Mstari lazima utawale ujumbe; kichwa na hoja kuu lazima zisimamie andishi; vidokezo lazima vionyeshe mistari ambayo hoja zinaelezewa kuonyesha kwamba kifungu kinashikanishwa na kinenwacho.

C—Je uko *wazi?* Ujumbe lazima uwe umepangiliwa. (Scharf n.d.)

2. Ujumbe uliopangiliwa vizuri ni wa lazima kwa ajili ya mafanikio ya kiwango cha juu sana. Wawasilianaji wenye mivuto wote wanatambua kwamba "mpangilio na utaratibu wa kisemwacho, huvutia kiwango sawa na kile utakachosema." (Stern 1991: 203).

a. *Kidokezo cha mpangilio wa ujumbe kinaweza mwanzoni kuonekana finyu, lakini kiukweli kinakusaidia kumweka huru mhubiri kutoka hali ya kuchanganyikiwa.* Ujumbe uliopangiliwa vizuri sana unasaidia kuwezesha uelewa wa kutathmini na uwazi wa maelekezo. Kwa hiyo basi: (1) unasaidia uelewa wa wasikilizaji wa msukumo na umuhimu wa ujumbe; na (2) unaongeza uwezekano wa wasikilizaji kuingia katika hatua hii mpya iliyo muhimu ya kutekeleza hilo maishani mwao.

b. *Baadhi ya wahubiri kimakosa wanafiki hivi, "ikiwa nitapangilia kile ninachotaka kusema tangu mapema, basi nitakuwa ninamzimisha Roho," hasa kwa vile Yesu alisema,"msitafakari kwanza mtakayosema, lakini lo lote mtakalopewa saa ile, lisemeni; kwa maana si ninyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu" (**Marko 13:9-11; Math 10:17-20; Luka 12:11-12**).* Kufikiri kwa jinsi hiyo kunaweza kusikika "kiroho," lakini, kiukweli, ni upumbavu wa kiroho:

(1) Dhana ya kauli ya Yesu ilihusiana na waamini kukamatwa na kuteswa wakati ambapo hawakuwa na fursa ya kujiandaa kujihami kisheria. Kauli ya Yesu haikuhusiana lolote na uandaaji wa ujumbe, kupangilia, na kuutoa. Zaidi ya yote, Yesu alisema *"usifadhaike"* kuhusu jinsi au nini kisemwe, unapotiwa mbaroni. Hakusem, "msifirie, wala kuandaa, au kupangilia utetezi kama unayo nafasi kufanya hivyo."

(2) Kila mtu, kusema ukweli, huandaa kile ambacho ni muhimu kwake (k.m., mlo atakaokula; jinsi atakavyoitumia siku), na kila mtu hutoa *fikira za awali* kuhusu cha kusema katika kila hali wakati anapopata fursa kufanya hivyo. Kunukuu kauli ya Yesu kama sababu ya kutojiandaa au kutojipanga katika ujumbe ni kisingio tu cha *uvivu au uzembe* na *maandalizi mabovu.* Kusema ukweli, kwa kutumia maneno ya Yesu kama kisingizio cha kutokuandaa na kupangilia ujumbe, utakuwa unafanya dhambi kubwa, kwa sababu:

(A) Utakuwa unamwakilisha visivyo Yesu na Neno lake kwa watu, kwa vile utakuwa unachukua kauli yake nje ya dhana, na kuitumia kuunga mkono uvivu na uzembe wako; na

(B) Utakuwa unasaliti ukweli kwamba mambo ya kidunia (k.m; mlo utakaokula au shughuli zako za kila siku), ambayo unachukua muda kuyaandaa, ni muhimu zaidi kuliko mambo ya Mungu (m.y; Neno lake), ambalo huchukui muda wa kuliandaa na

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kulipangiliaCna badala yake unakuwa na kiburi na ujasiri wa kwenda kuwahubiria watu.

(3) Kutumia kauli ya Yesu kama kisingio kutoandaa na kupangilia ujumbe wako tangu mapema kiukweli kunaonyesha kumtazama ki-chini sana, wala si kwa juu, Roho Mtakatifu.

(A) *Kila mtu ambaye anasoma kiukweli Neno la Mungu na kuandaa kifungu cha kuhubiri atakuwa (au anapaswa awe) katika ushirika wa karibu kabisa na Roho Mtakatifu.* Kuitumia kauli ya Yesu kuhusu *"kutofadhaika kuhusu kile cha kusema"* kunaonyesha ukweli kwamba kiukweli hujakuwa na ushirika na Roho Mtakatifu kabisa. Kwa hiyo, ni fikira tu kudhania, unapoinuka kuhubiri, Roho Mtakatifu ndipo "kimuujuza" atanena kupitia wewe, wakati hujakuwa katika kusema naye katika juma hilo.

(B) *Kutumia kauli ya Yesu kama kisingio kutoandaa na kupangilia ujumbe wako tangu mapema kunatokana na fikira za kiburi na kujiinua kwamba, kama ungeandaa na kujipangilia utakachosema tangu mapema, Roho Mtakatifu ni dhaifu mno, kiasi kwamba hawezi kukupa mawazo mapya wakati unahubiri ujumbe wako kuufanya uwe wa kufaa zaidi.* Hapo unakuwa unatenda dhambi kwa kujiinua mwenyewe kimakosa kwa vile, utakuwa unasema kimsingi, "Mimi nina nguvu sana kiasi kwamba nikifanya maandalizi yoyote mapema, hata Roho Mtakatifu mwenyewe hawezi kuingilia kati." Kusema ukweli, Roho Mtakatifu ana uwezekano mkubwa wa kusema kukupitia wewe ikiwa utakuwa unafanya ushirika naye katika juma hilo na kuwa umekuwa ukitumia juhudi zako zote kupanga na kuandaa ujumbe mzuri.

3. Vidokezo vya Ujumbe ulioandikwa husaidia kwa ajili ya mahubiri yenye kufaa. Vidokezo vinasaidia kupangilia kitu. Vinahakikisha kwamba vyote vinavyotakiwa kwenye ujumbe vinashughulikiwa kwa utaratibu unaofaa. Kidokezo kinakuwa lazima ikiwa Asehemu ya ki-akili@ itajitokeza kwenye ujumbe na mhubiri atasahau kitu fulani. Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu matumizi ya vidokezo:

a. *Elekeza vidokezo vyako kwenye uhitaji wako maalum.* Vidokezo vinaweza kuwa vyepesi tu, au vikawa vimepanuka zaidi. Maneno ya msingi au misemo isaidie akili za mhubiri mawazo mapya na vifungu. Sentensi fulani ambazo ni muhimu na ambazo zinahitajika zineneke kinamna maalum ziandikwe hivyo. Jinsi sahihi za kutamka maneno fulani zinaweza kuonyeshwa. Misemo, au vipengele vingine vya ujumbe vinavyohitaji kusisitizwa vinaweza kupigiwa mistari, au kuwekwa maandishi mazito, au kuandikwa herufi kubwa. Sehemu za pumziko, zinaweza kuonyeshwa kwa mistari au alama nyingine.

b. *Kutia rangi.* Kupaka mistari rangi ili kuweka alama ni mbinu nzuri sana. Rangi tofauti zinaweza kuonyesha vifungu vya Maandiko vinavyohitaji kusomwa, mistari maalum ya kusisitizwa, maswali ya udadisi, hoja muhimu, sehemu za mabadiliko, n.k. Kutia rangi pia kunasaidia kufanya masomo yaonekane kwa mhubiri wakati anatoa ujumbe wake.

c. *Tusifungwe na vidokezo vyetu.* Ni muhimu kwamba mhubiri asifungwe na vidokezo vyake, bali wakati wa mahubiri, awe anaviangalia tu ili kumwongoza. Mhubiri anatakiwa awe amekijua sana anachotaka kukisema, kiasi kwamba anaweza kuwa huru kutembea jukwaani, na pia kuwaangalia wasikilizaji wake.

4. Nguvu ya mahubiri husaidiwa na mazoezi ya kutamka kwa mdomo. Wahubiri wote *huwazia kuhusu* kile wanachotaka kusema, na wahubiri walio wengi huandaa aina fulani ya *ujumbe kwa maandishi*. Hata hivyo, walio wengi hawasimami na *kufanya mazoezi ya kutamka kwa mdomo* kabla hawajayatoa. Hilo ni kosa kubwa. Mwandishi wa Utafiti wa GASS anatahadharisha: "Mtindo wa kinywa unahitaji maandalizi ya mdomo. Walisema wahubiri wengi waliofanyiwa utafiti, 'Hofu yangu ni kuwa yawezekana yasitokee yote pamoja katika mahubiri hayo.' Hofu hiyo hiyo inaweza kuondolewa kwa kufanyia mazoezi ya mdomoni kadiri mahubiri yanavyokaribia, kabla ya muda halisi kufika.

Kama sehemu za muhtasari au dibaji inavyoandaliwa, kunahitajka 'mazoezi' ya mdomo, na kupimika kwa nguvu inayotoka katika kinywa. Upangiliwe upya. Ufungashwe upya katika makundi. Uratibiwe upya. Kadiri kila kisehemu cha mahubiri kinavyojengwa, mhubiri anatakiwa afanyie mazoezi hayo kupitia akili zake. Tunda la kinywa huhitaji zoezi la maandalizi ya kinywa. Mazoezi ya kinywa husaidia kujua utabiri wa muda; ambapo mawazo kwa kichwa pekee hakuwezi. Kati ya mbinu zote za maandalizi watumiayo wanenaji wa hadharani, rafiki yangu Kent Menzel na mimi tuligundua kwamba mazoezi ya mdomo kwa wasikilizaji ndiyo mbinu ya maandalizi ambayo inakujulisha kuliko zote, ubora wa unenaji mbele za watu." (Carrell 2000: 224-25)

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

E. ***Miundo mbali mbali ya mipangilio***

Mbinu yenye undani ya kuandaa na kupangilia ujumbe imeambatanishwa kama **Dibaji B ("Hatua za Ujumbe: Vidokezo Vichache Kabisa Kwa Wahubiri").** Ingawaje hakuna "njia sahihi" moja tu ya kupangilia au kuhubiri kifungu fulani, ifuatayo ni miundo mbali mbali ya mipangilio. Kifungu hicho hicho cha Maandiko kinaweza kuhubiriwa kutumia mbinu tofauti. Miundo hiyo ina mengi ya kufanana, na vipengele vya muundo moja vyaweza kutumiwa kwenye muundo mwingine. Kwa mfano, utangulizi wenye msingi wa tatizo ambao ni kielelezo cha aina ya "Mimi-Sisi" unaweza kutumiwa kwenye miundo mingine yeyote, kama ulivyo utekelezaji na mahitimisho yake. Hiyo ndiyo miundo pekee ya jumbe iliyopo, na hii inaweza ikabadilishwa kama ni lazima.Hata hivyo, matumizi ya miundo ya mipangilio inashauriwa kuhakikisha ujumbe unakidhi zile "A-B-C" za mipangilio ya ujumbe, ili kwamba ujumbe uwe na mafanikio kiasi iwezekanavyo kwa wasikilizaji. Vidokezo vyenye undani vya jumbe kadhaa, kulingana na miundo hii, imeambatanishwa kama **Dibaji C-I**.

1. Muundo "Fundisho" —Muundo huu hasa hufaa wakati wa kuhubiri kutoka nyaraka au sehemu nyingine za Maandiko ya maadili.
    a. *Utangulizi*
    b. *Kichwa*
    c. *Mpangilio wa hoja kuu.*
    d. *Maelezo ya kifungu husika* (ni pamoja na mifano na matumizi kiutendaji wake [au utendaji unaweza kuwekwa mwishoni])—Fuata mpangilio au mkondo wa mawazo ya kifungu unachokielezea.
    e. *Hitimisho*
2. Muundo wa "Simulizi MKM [Maelezo-Kanuni-Matumizi kimatendo]"—Muundo huu kikawaida hufaa sana wakati wa kuhubiri simulizi au vifungu vya Ki-shairi:
    a. *Utangulizi*
    b. *Mpangilio wa hoja kuu* (bado ni moja, lakini itakuwa itafanana kama hivi, "Tutakwenda kuangalia kifungu hiki mara tatu [au 'kwa njia tatu']: kwanza tutaangalia undani wake; kisha kanuni zake; ndipo matumizi kimatendo").
    c. *Rudia simulizi na maelezo ya simulizi* (katika mtindo wa simulizi, pamoja na habari za kihistoria).
    d. *Rudi nyuma na pitia kanuni zinazofundishwa.*
    e. *Kichwa* (kichwa kinakuja mahali hapa, kati ya kanuni na matumizi kimatendo; hii ni njia ya kuambukizika ambayo mara nyingi huhusu jinsi simulizi zenyewe zinavyoundwa).
    f. *Pitia kifungu mara ya tatu ukisisitiza matumizi yake kimatendo.*
    g. *Hitimisho*
3. Muundo wa "Mpangilio Wa Kihariri"—Simulizi wakati mwingine hufuatia muundo wa uandishi uhusishao matukio manne (mfano ni **Luka 8:22-25**); muundo huu hutenda kazi vizuri kwenye simulizi nyingi, visa vya miujiza, au simulizi nyingine zinazohusu hatari/uzimio:
    a. *Utangulizi*
    b. *Mpangilio wa hoja kuu* (inayozungumzia "matukio manne" ya dhana; hatari; azimio; na matokeo yake/matumizi kimatendo).
    c. *Dhana* (wazo la nyuma katika **Luka 8**, agizo la kwenda hadi ng'ambo ya ziwa).
    d. *Hatari* (katika **Luka 8**, dhoruba na mayowe kuwa "tunazama").
    e. *Ufumbuzi* (katika **Luka 8**, Yesu kama Bwana wa uumbaji, "nayo ikatulia").
    f. *Kichwa* (kama ilivyo katika muundo wa MKM, Kichwa kinakuja kabla tu ya matumizi kimatendo; hili linafikisha kilele cha usikivu wa simulizi).
    g. *Kuhusisha/matumizi kimatendo* (katika **Luka 8** swali la wanafunzi "Ni nani huyu?" ni matumizi na hutuongoza kwenye uelewa wetu kuhusu Yesu ni naniC̈ni BwanaC̈na utumikaji kwetu kwamba tunaweza, na ni lazima tumtumaini yeye, hata [na hasa] wakati maisha yametuendea vibaya kabisa).
    h. *Hitimisho*
4. Muundo wa "Mimi-Sisi-Mungu-Wewe-Sisi"—Muundo huu uliundwa na Stanley (Stanley and Jones 2006: 119-31), na unaweza kutumiwa wakati wa kuhubiri mtindo ulioandikiwa Maandiko. Kwa vile maneno yaliyotumiwa kinamna fulani ni tofauti na miundo mingine, utaelezwa kiundani zaidi hapa. Kidokezo chake ni "Cha kimahusiano," kulingana na mahusiano ya "Mimi-Sisi-Mungu-Wewe-Sisi."
    a. *MIMI*—Huanzia sentensi zake au kisa kuhusu wewe mwenyewe, au tatizo au swali ulilokabiliwa nalo, ili kujitambulisha mwenyewe (hasa hufaa unapozungumza na wasikilizaji ambao ni wapya) na somo kwa wasikilizaji. Hata hivyo, MIMI si hasa kwa ajili ya mnenaji, bali ni kuhusu *jambo la kuwaunganisha* na wale wasikilizaji. Matokeo yake, swala unaloliibua ni swali, au tatizo, au mvutano ambao watu wengine pia wanakabiliana nalo katika maisha yao.
    b. *SISI*—Kisha panua mvutano wa swala ulililoliibua kumhusisha kila mtu katika wasikilizaji (k.m.,

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

"Wakati mwingine hushangaa kwa nini ninajali kuomba [MIMI]; nadhani na wewe umewahi kujiuliza pia [SISI]," au "Kuna watu ambao siwezi kabisa kukaa nao [MIMI]; je kuna yeyote hapa anayepatwa na shida kama hii pia [SISI]?"). Tumia wakati wa kutosha kufanya hivi kuhakikisha kwamba wasikilizaji wanakuwa *wameshikika katika swala hilo.* Kwa hiyo, unaweza kuliibua jambo kwa njia tofauti©jinsi linavyotenda kwa vijana au watu wazee, watu wasiooa au kuolewa, waamini au wasioamini, nk. Stanley anaelezea: "Usibadili kutoka SISI kwenda sehemu nyingine mpaka ujisikie kwamba umeibua mvutano ambao wasikilizaji wako wana hamu sana utoe jibu lake. Yaani, usipuuze hali ya shauku. Kaza kwenye swali unalokusudia kulijibu, hadi uwe na uhakika wasikilizaji wako wanataka lijibiwe. Vinginevyo unakaribia kuzitumia dakika Ishirini au Thelathini za maisha yako ukijibu swali ambalo hakuna mtu yeyote analiuliza." (Ibid.: 125) Njia hii "inakuweka wewe kulizungumzia swala la mtumizi kimatendo mwanzoni na pia mwishoni. Ikiwa utafungua ujumbe wako na masumbufu *yako* (MIMI), na kuyahusisha na masumbufu *yao* (SISI), tayari unakuwa upo kwenye kweli ya kimatumizi" (Ibid.: 126). (Tambua kwamba Stanley anatumia muundo wa "Uzio wa Reli," na huanzia na "reli ya chini," ingawaje hatumii maneno yale.)

c. *MUNGU*—Sasa unaweza kubadilishia mawazo ya Mungu kuhusu swala hilo, m.y; msimamo wa ki-Biblia. Kwa hiyo, baada ya kwanza kuibua tatizo katika maisha na kulinganisha na watu, unahamia kwenye Biblia na ufumbuzi wa tatizo hilo. Katika kueleza kwako maelezo hayo unapaswa Akuwaingiza watu wajisikie ndani ya kinenwacho@: wakawe wamekazia macho kwenye kifungu kimoja kuliko kuruka ruka katika Biblia; uwongoze kwenye shabaha ilengwayo (m.y; usisome sehemu ndefu pasipo kueleza kitu); tia alama na uelezee maneno yasiyo ya kawaida na misemo; onyesha mambo wakati ukiendelea kama kiongozi; kama baadhi ya sehemu ya maandishi yahudumiwayo yanakufadhaisha au huna uhakika wake, sema hivyo (kama panakufadhaisha wewe, panamfadhaisha mtu mwingine katika wasikilizaji pia); wafanye wasikilizaji wasome maneno fulani kwa nguvu ili kusisitiza; fupisha ujumbe mzima katika kauli zilizopangika vizuri. (Bila shaka uwaingize watu katika ujumbe huo wakati unapotumia moja ya miundo ile ya mahubiri ya ufafanuzi pia.)

d. *WEWE*—Hapa uwaambie watu nini cha kufanya kuhusu walilolisikia. Jaribu kutafuta mahali pamoja pa utekelezaji panapoweza kuwapa changamoto kila moja kujaribisha. Stanley huwaagiza watu mara chache sana kufanya maamuzi ya mabadiliko kwa chochote; hadhani kwamba hilo lina ukweli. Hata hivyo, mara zote huwaagiza watu wajaribu kitu katika juma, au hata kwa siku, au wakati mwingine kwa mwezi. Jaribu kutafuta kitu ambacho kila mtu anaweza kufanya—na unaweza kutoa mifano ya makundi katika wasikilizaji (vijana, wazee, waamini, wasioamini, nk.), kama ulivyofanya kwenye utangulizi.

e. *SISI*—Hitimisha kwa kuwatia moyo watu jinsi kanisa, au jumuiya, au taifa, au dunia, ingeonekana kama watu wangeanza kutekeleza hilo ambalo limesemwa hapo. Hilo linaweka maono ya jinsi mambo yanaweza kuwa na yangetakiwa kuwa. Pia hukuunganisha wewe na wasikilizaji wako (m.y; wewe na wasikilizaji wako nyote "mko kwenye mtumbwi mmoja") badala ya wewe kutenganishwa na wasikilizaji wako ukiwaambia kitu cha kufanya.

VIII. <u>Mawasiliano Yenye Mvuto na "Mtindo" wa Mhubiri</u>

A. *Hakuna mtindo wowote ulio sahihi wa kuhubiri*

1. <u>Kila mtu anazo nguvu azitegemezo na mdhaifu anayotakiwa kuyabadili.</u> Usijaribu kumwiga mtu mwingine, ila jaribu kujifunza kwa wengine huku ukibakia kuwa katika uhalisi wa kwako ulivyoumbwa. Stanley anashauri: "Katika juhudi yako ya kujaribu kujenga mtindo ufaao, unahitaji kujiuliza mwenyewe maswali mawili:

    1. Nini kinafaa?
    2. Nini chanifaa mimi?

    Swali la kwanza litakuweka katika kutafuta kanuni mpya na mbinu mpya za mawasiliano. Litakuongoza ujue kwa nini wawasilianaji wengine wanaweza sana kuwachota watu katika jumbe zao na wengine hawawezi. Litakusaidia kuwa wazi kwa mawazo mapya. Litakuchochea kuwa mtu wa kujifunza maisha yote kwenye uwanja wa mawasiliano. . . . Swali la pili litakuchochea kuendelea kutathmini na kurekebisha ujumbe wako unapoutoa." (Stanley and Jones 2006: 179)

2. <u>Uzoefu peke yake haukufanyi wewe kuwa mhubiri mzuri zaidi. Badala yake, uzoefu pamoja na tathmini ya uzoefu huo utakufanya mhubiri bora zaidi.</u> Unatakiwa utathmini mahubiri yako mwenyewe na kuomba tathmini ya kweli kutoka kwa wasikilizaji washiriki wenye akili na wenye kuona mbali. Tafuta kikundi kidogo cha watu mchanganyiko (umri tofauti, jinsia tofauti, na wa historia tofauti) ambao unawaamini na ambao

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

hawaogopi kuwa wakweli kwako, na uwaombe wakufanyie tathmini za jumbe zako (kwa yote mawili-mtindo, na yahubiriwayo) mara kwa mara. Ndipo unaweza kuwa na ujasiri wa *kutendea kazi hizo tathmini* na kubadili kile kinachotakiwa kubadilishwa ili kuwa bora zaidi, mwenye mvuto, na kufaa zaidi katika mawasiliano ya Neno la Mungu. Mbinu nyingine ni nyakati fulani "kutoa karatasi ndogo katika kila kijarida, chenye maelekezo yaliyoandikwa juu: *Kufuatia mahubiri ya leo, tafadhali andika wazo kuu la ujumbe kwa maneno yako mwenyewe. Dondosha maoni yako hayo ya sentensi moja katika 'Kisanduku cha Kusaidia Mahubiri' wakati unatoka nje ya mlango. Asante.* [Ikiwa kanisa lako halina vijarida vilivyochapishwa, waombe wasikilizaji kufanya hilo kila mtu peke yake.] Unaposoma majibu yao, swali lako kama mhubiri basi linakuwa, 'Je ninaridhika kwamba wanaelewa?'" (Carrell 2000: 218) Tofauti kati ya thamani ya jumbe zilizotathminiwa kwa miaka 10; na kutokuwa na jumbe zisizotathminiwa, ni tofauti ya uzoefu wa miaka 10, na uzoefu wa mwaka 1 ukarudiwa mara 10.

B. ***Tabia au mtindo wa kuhubiri utatofautiana kulingana na mada na lengo la ujumbe husika, mazingira tunayohubiria, na uelewa na mahitaji ya wasikilizaji***

1. Maandiko yanaonyesha kwamba tunatakiwa tuwe na msisitizo na mkazo tofauti kulingana na hali ya kifungu tunachokielezea. Biblia inaweza kuelezewa na kuhubiriwa kwa sababu nyingi tofauti na kwa hali tofauti. **2 Tim 3:16** panasema kwamba Maandiko yanaweza kutumiwa kwa faida "Kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki." Katika **2 Tim 4:2** Paulo anasema vivyo hivyo kwamba kuhubiri kunaweza kuwa na kukaripia, kukemea na kuonya. Katika **1 Tim 4:11, 13, 16** na **6:2;** Paulo alimwambia Timotheo kuyatumia Maandiko kwa mafundisho. Zaidi ya matumizi hayo ya Maandiko, mahubiri ya Paulo mwenyewe pia yalikuwa ya kutia moyo (**Mdo 16:40; Wakol 2:2; 1 Wathes 2:11**), faraja (**2 Wakor 1:4; 1 Wathes 4:18**), kushawishi (**1 Wathes 2:11**), kuinua (**Mdo 20:31**), kutahadharisha au kuonya (**Mdo 13:8-12**), kutoa sababu, kudhihirisha, kuthibitisha, na kuvutia (**Mdo 18:4, 19, 28; 26:28-29**). Petro alikuwa tayari siku zote "kulikumbusha" kanisa juu ya mambo waliyoyasikia,ili kwamba wasikilizaji waweze kiurahisi "kuyakumbuka mambo hayo" (**2 Petr 1:12-15;** ona pia **Luka 24:25-27; Yohn 3:9-10; Mdo 3:12-18; 8:30-35; 17:16-31; 26:25-28**). *Matokeo muhimu ya hili ni kuwa, tunapohubiri na kutumia Andiko, siyo tu kwamba yaliyomo lazima yakamilishwe, bali pia msisitizo lazima ufuatwe, na dhana yake lazima iheshimiwe.*
2. Ili kuwashawishi watu, ni lazima ujumbe "Tuufanye sehemu yetu".
    a. *Ujumbe lazima uwe sehemu yetu.* "Hali ya mvuto wa mahubiri yoyote yanaendana sambamba na shauku, na nguvu ya mnenaji mwenyewe katika somo husika" (Buckley 1988: 14). Mhubiri anatakiwa kwanza ahusishe shauku akili zake kwa kujifunza kwa bidii na kuelewa kifungu cha kuhubiri (m.y, katika kujifunza kwake, anaanzia na "Ile reli ya juu"). Hilo litamwingiza yeye kushikika na kifungu. Kuzamia kwa dhati kiasi hicho kwenye kifungu kitakachohubiriwa kutakuwa na matokeo angalau mawili hapo atakapokuwa anakihubiri kifungu hicho:
        (1) Kutampatia msisimko kiakili kuhusiana na kifungu hicho. "Msisimko kiakili upande wa mwalimu . . . hufanya kazi ya kuzaa msisimko kwa upande wa msikilizaji" (Adler 1983: 54-55). Mwalimu mwingine wa unenaji wa kadamnasi analiweka jinsi hii: "Ni ile nguvu ndani ya sauti ya mnenaji—mwonekano wa hamu ya mnenaji mwenyewe—ndiyo inayolipua shauku kwa wasikilizaji" (Buckley 1988: 15).
        (2) Msisimko wa kiakili au nguvu inayotokana na "kumiliki" kifungu kutasaidia kutawala kikamilifu hisia ya uwasilishaji ya kifungu hicho. "Kule kufikiri ulikokufanya peke yako faraghani na sasa unakudhihirisha katika hotuba yako, lazima kuwe na nguvu ya kihisia sawa na nguvu ya kiakili [ili kuwa wa kufaa na mwenye kushawishi]" (Adler 1983: 59). Hiyo "nguvu ya kihisia" lazima iwe "halisi," siyo ya kudanganya. Ikiwa mhubiri amejifunza kwa bidii kifungu chake na kuwa "halisi" kwake—anaona umuhimu na umaana wake—ndipo ataweza kulipeleka hilo kwa wasikilizaji wake: "Mtu lazima ajitoe mwenyewe. Mtu lazima ajilazimishe kujilisha tumboni, ndipo anene Mhubiri anapozamisha fikira zake katika uwepo wa Uungu faraghani, kile asemacho hatakuwa analazimisha hisia zake. Kinyume chake anaweza kuzifisha." (Buckley 1988: 17)
    b. *Mbinu ya kumsaidia mhubiri "kuumiliki" ujumbe wake.* Stanley anashauri kwamba kabla ya kuhubiri "unatakiwa ukae chini mezani na uutoe ujumbe wako kwa wasikilizaji walio wawili kwa namna ambayo ni ya kimazumnumzo na kiuhalisi pamoja. Ujumbe lazima kinamna fulani uwe kisa chako mwenyewe unachoweza kuelezea kana kwamba unaelezea uzoefu wako binafsi." (Stanley and Jones 2006: 135)
    c. *Mfano wa kuufanya ujumbe "halisi" kwa mhubiri.* Mtu mwingine alikuwa anakwenda kutoa ujumbe kwenye kanisa la Stanley, lakini bila shaka alikuwa ameshikika sana na vidokezo vyake, na

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

yaliyomo, na jinsi atakavyohubiri, kiasi kwamba akawa amewasahau wasikilizaji wake, mahitaji yao, masumbufu yao, na matarajio yao. Kabla mtu yule hajaenda kuhubiri Stanley akamwambia: "'Je ungewezaje kuuwasilisha ujumbe huu kama mwanao wa umri wa miaka Kumi na Nane ameamua kuasi yale yote ambayo umeshamfundisha, kimaadili, kitabia, na kitheolojia, si mpaka hapo awe na sababu nzuri ya kumfanya asiwe hivyo? Je ungelisema nini asubuhi hii kama ungelijua yupo katika hali hiyo? Kwa sababu, yawezekana kuna mtoto wa mtu hapa ambaye hii inaweza kuwa ndiyo nafasi yake ya mwisho. Sasa acha kujali kuhusu vidokezo vyako. Uende kule nje, ukaomboleze kwao kama kwamba ni mtoto wako mwenyewe ndiyo yuko katika hali hiyo mbaya.' Naye akafanya hivyo." (Ibid.: 98-99)

C. ***Kanuni za hotuba za hadhara zenye mvuto hufaa pia kwa mahubiri na kwa hutuba nyingine za hadhara***

1. Uhutubiaji wenye mafanikio na wenye mvutio unaweza kuimarishwa wakati mhubiri anapochanganya ushawishi wa aina tatu (*logos, pathos,* na *ethos*) na "sheria nne" za ushawishi:

a. *"Sheria nne" za ushawishi ni:*

Sheria ya 1: Msingi (kile tunachokisikia kwanza hutia rangi kufikiri kwetu na kutusaidia tuwaze kile kitakachofuata baadaye);

Sheria ya 2: Uhitimishaji (tunachokisikia mwishoni huwa kinabakia kwenye kumbu kumbu zetu zaidi);

Sheria ya 3: Marudio (ukumbukaji huongezeka kadiri unavyofanya marudio zaidi); na

Sheria ya 4: Uangavu (kupokea habari yoyote huongezeka kiwango kikubwa itokeapo kuona na kusikia kunahusishwa). (Stern 1991: ch. 5)

b. *Jinsi aina hizo tatu za ushawishi na sheria nne za ushawishi zinavyofanya kazi pamoja.*

Logos ndiyo sababu ya ufafanuzi na maelezo ya ujumbe wa Maandiko kuwa na maana. Pathos ni sababu kwa nini lazima tuwahusishe wasikilizaji kibinafsi. Ethos ni sababu kwa nini maisha yetu yawe katika hali isiyolaumika. Msingi ni sababu kwa nini utangulizi wetu ni wa mihimu sana. Uhitimishaji ni sababu kwa nini mahitimisho yetu ni ya muhimu sana. Maridio ni sababu kwa nini marudio ya hoja yetu moja, iliyo wazi ni muhimu mno. Uangavu ni sababu kwa nini mifano yetu ni ya muhimu mno.

2. Kile usemacho, na jinsi unavyokisema vyote ni vya muhimu, lakini kwa njia tofauti.

a. *Jinsi unavyokisema kitu ni muhimu zaidi kuliko kile usemacho, kuhusinana na maswala ya kukamata usikivu wa watu na kuwafanya watege masikio yao.* Hili linaonyesha kwa nini utangulizi wako ni wa muhimu sana.

b. *Kwa upande mwingine, lile ulisemalo ni la muhimu zaidi kwa wasikilizaji wako kuliko jinsi ulisemavyo ikiwa wasikilizaji "wameshaurika kikamilifu kuwa unakaribia kuwapa jawabu la swali ambalo wamekuwa wanajiuliza, kuwapa ufumbuzi wa kitendawili ambacho wamekuwa hawezi kukitatua, au kutatua mvutano ambao wameshindwa kuutatua"* (Stanley and Jones 2006: 152). Hii ndiyo sababu ufafanuzi wetu, maelezo, matumizi kimatendo, na hitimisho ni vya muhimu sana, *ikiwa* kwanza umeukamata usikivu wa wasikilizaji katika utangulizi wako.

c. *Kanuni za mawasiliano mazuri (hoja moja; mpangilio mzuri; kuwa wazi na wenye uelekeo rasmi; kurudia na mifano ya hoja husika, nk.) Kutatamba juu ya unenaji mbovu karibu kila wakati.* Kama ahitimishavyo Stanley, "*uwazi utatamba juu ya mtindo.* Uwazi hutamba karibu juu ya kila kitu." (Stanley and Jones 2006: 175)

3. Lazima tukazie macho kwenye kipengele cha "taaluma" ya uhutubiaji wetu. Tabia ya uwasilishaji wetu inaweza kuimarisha au kupotosha ushawishi wa kile tunachotakiwa kukisema. Wahubiri wanatakiwa kufikiria kwa makusudi kabisa vipengele hivi kwenye uwasilishaji wao, kwa sababu *jinsi* mtu asemavyo kitu ni muhimu kama *nini* anakisema. Hilo ni muhimu katika kuelezea Maandiko, kwa sababu tabia ya uwasilishaji wako inaweza kiukweli, au kiupotofu kuwakilisha Neno la Mungu kwa watu.

a. *Dhana, sauti, nguvu, na kasi ya sauti, hutakiwa viwiane na mazingira.* Mwanatheolojia moja na mhubiri anahusisha mfano huu: "Siku zote nimekuwa nikitaabika na spidi ya mahubiri yangu. Wakati fulani baada ya kutoa ujumbe, mwanamke moja aliuliza kwa mshangao, 'Hivi ulibahatika kupumua?' Tangu wakati huo, nimekuwa nikihubiri kwa kituo na mwendo mzuri wa uwasilishaji, lakini bado sijafanikiwa kwenda vizuri na jumbe zangu." (Osborne 1991: 364) Watu kimsingi hawawezi kusikiliza kwa muda mrefu ambapo mhubiri habadilishi spidi, nguvu ya sauti,kina, na viwango vya kihisia. Nyanja nyingine mbili za sauti zetu zinahitaji kuangaliwa:

(1) Maswala ya sauti kinywani na matamshi. Watu wengine huweza kuishia kuwa na kinywa kikavu baada ya kuongea kwa muda fulani. Linaweza kuwa wazo jema kuwa na chupa au glasi ya maji karibu. Ikiwa una mafua au kikohozi, kutumia vidonge vya kulainisha koo, au

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kumung'unya pipi kali kabla hujaanza kuongea, au kuhakikisha unakuwa navyo karibu, kunasaidia. Jijue mwenyewe tabia za mahubiri yako. Watu wengi wana "kupe" wengi kwenye maneno waongeayo—wanasema maneno yasiyo na maana, au misemo kama vile "si unajua," au "kama," au "tu" kwamba "vijazio vya maneno" ambayo kiuhalisi hayamaanishi lolote. Haya yanaweza kuwa yanaharibu sana kwa wasikilizaji. Hata misemo kama vile "Bwana asifiwe!" na "Haleluya!" huweza kuwa "vijajilizo" visivyo na maana vinaporudiwa mara nyingi mno, na pasipo sababu. Unapowaambia watu "Bwana asifiwe", kunapaswa kuwe na sababu ya "kumfanya asifiwe," katika kile unachokisema. Baadhi ya wasikilizaji kusema ukweli huanza kuhesabu ni mara ngapi unasema maneno hayo yasiyo na maana ya kujazia! Ikiwa una matatizo katika kutamka maneno fulani (k.m, majina ya watu wa Agano la Kale), fanya mazoezi ya kuyataja hayo tangu mapema. Kuyaandika maneno kama hayo katika karatasi zako, na matamshi yake sahihi, huweza kusaidia.

(2) Vipaza sauti na maspika (vyombo vinavyotupa sauti mbali [Vyombo vya Mahubiri]). Kipengele kimojawapo cha nguvu ya sauti ya mtu ni matumizi ya Vipaza sauti na maspika [Vyombo vya Mahubiri]). Vipaza sauti na maspika huweza kutoa "sauti kali za miluzi" au tifu-tifu au kuharibu sauti kwa jinsi nyingine ambayo kiukweli hufanya washirika wasikie kwa taabu zaidi na kutomwelewa mhubiri. Zaidi ya hayo, makanisa mengi ambayo ni madogo madogo nayo yanatumia vipaza sauti ingawaje vyumba vyenyewe ni vidogo kiasi kwamba vyombo hivyo si vya lazima. Katika hali kama hizo, inaweza kuwa bora zaidi tu kuongea kwa sauti yako ya asili na kutotumia vipaza sauti kabisa.

b. *Mwonekano wa sura zetu na mikono inavyotembea kuwe na makusudi, siyo "Kulazimishwa"* kukiendana na jambo husika, ila "kujitokeze kiasilia tu na joto la nguvu ya hisia au msukumo akilini" (Buckley 1988: 174). Kwa hiyo, "mtu asipige ngumi madhabahu[2] anapotaka kuonyesha kwamba lazima kukubaliana kama sharti, wala kuinua mabega ili kuwaasa washiriki kuwa unatangaza vita" (Ibid.: 173-74).

c. *Uwe makini kwa mwonekano wa miili yetu, inavyokaa, na uvaaji wake.*

(1) Mwonekano wa mwili. Tuhakikishe nywele zinatengenezwa vizuri au kuchanwa vyema. Kama tuna utofauti wowote au hali isiyo ya kawaida ambayo washirika wetu hawajawahi kuiona kabla ya hapo (m.f. bandeji usoni, mkono kufungiwa kamba, nk.), hilo lielezwe kwa kifupi au kutolewa maelezo yake mapema mwanzoni. Hali yoyote isiyo kawaida katika kuonekana kwetu ni kitu ambacho wasikilizaji watakichunguza, nao watakuwa wanashangaa, na hicho chaweza kuwaondoa kwenye ujumbe wenyewe.

(2) Mkao. Mkao wetu unatoa habari nyingi sana kwa wasikilizaji. Ikiwa tumekuwa wakali sana, wasikilizaji wetu wanakuwa na hofu. Ikiwa tunaegama kwenye madhabahu daima, au kuonyesha hali ya uchovu tusimamapo, wasikilizaji wataelewa kuwa mada tunayotaka kuisema haina umuhimu.

(3) Uvaaji. Hakikisha kwamba tai yetu imevaliwa juu ya shati ambalo limepigwa pasi, shati lililochomekewa, viatu vimefungwa, na mifuko ya makoti yetu imefungwa vizuri. Watu hukazia macho vitu hivi, na kwa hiyo huhamishwa mawazo kwa urahisi wasisikilize ujumbe wetu. Pia, ikiwa unazo funguo au chenji za shilingi mfukoni, hakikisha huweki mkono wako mfukoni na kuzivuruga wakati unaongea. Watu wengi hufanya hilo pasipo kukusudia, na hilo huvuruga sana usikilizaji wa watu.

D. *"Upako" wa mhubiri hauna uhusiano na misisimko*

1. Watu wengine huwanena wahubiri kuwa na "Upako" kama kwamba kupiga kelele, kutembeza mikono, au kuonyesha hisia kubwa; kuwa ndiyo ishara ya kuwepo kwa Roho Mtakatifu, au kama kwamba upako wa Roho Mtakatifu ndiyo ukuu wa mhubiri mwenyewe. Mawazo kama hayo kimsingi (na ni hatari sana) ni ya makosa. Hali ya hisia *yenyewe* haina *kabisa uhusiano wowote* na ukweli kwamba mhubiri huyo anatumiwa au hatumiwi na Roho Mtakatifu. Tunajua hili angalau kwa sababu sita:

a. Hakuna popote katika Maandiko yanapoelezwa au kuhusishwa katika kuhubiri kama ishara maalum ya "upako" kwa Roho.

b. Aina zilizo nyingi au aina tofauti za mahubiri ambazo Maandiko yanatuagiza (kama vile kufundisha, kutoa moyo, kufariji, kuhoji, kudhihirisha, kuthibitisha, na kushawishi) ni kinyume na, au

[2] "*Madhabahu* ni jukwaa ambalo mnenaji hulitumia kuongelea; *mimbari* ni ile meza ambayo mnenaji huitumia kuongelea" (Buckley 1988:163).

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

yatapunguzwa kufaa kwake, kwa kutumia misisimko mingi.

c. Kupiga kelele, kuonyesha vitendo, na misisimko mingi huweza kuwa ni usanii wa kimila au kidesturi tu.

d. Kupiga kelele, kuonyesha vitendo, na misisimko kumetumiwa na watu waovu ambao wamedhihirika kutojazwa na Roho (k.m., Adolf Hitler).

e. Ikiwa yanatumiwa na mhubiri kuonyesha "upako" wake, kuonyesha misisimko kwaweza "kupotoshwa" kirahisi tu.

f. Roho wa Mungu huonyesha "upako" na kuwatumia wahubiri ambao *hawaonyeshi* dalili zozote ambazo zinatajwa na watu kuwa ndizo "Upako." Jonathan Edwards hutolewa kama mfano mzuri sana: mahubiri yake, pengine kuliko ya mwingine yeyote, ndiyo yaliyohusika na mbubujiko wa Roho ulioitwa "Uamsho Mkuu" katika Amerika kwenye miaka ya 1730-1740. Hata hivyo, "katika siku za uamsho huo, bado aliendelea kuandika jumbe zake kirefu na kuzisoma, kwa wingi na kwa kiasi kikubwa pasipo mikogo" (Piper 2004: 53).

2. Hakuna lolote katika hayo ya hapo juu linakusudiwa kushauri kwamba misisimko (au "mikiriti" kama Edwards alivyoiita, haina umuhimu au *si* sehemu ya utendaji wa Roho kwa mhubiri, au kwa maisha ya wasikilizaji wake; ni hivyo (ona Piper 2004: 84-86). Yaliyo ya muhimu hapo, ni hizo ishara za ki-nje, ambazo baadhi ya watu kimakosa huona ndizo "upako" za Roho Mtakatifu.

NUKUU ZILIZONUKULIWA

Adler, Mortimer. 1983. *How to Speak How to Listen.* New York: Collier.

Allen, Ronald. 2005. "What do Lay People Think God is Doing in the Sermon?" *Encounter* 66: 365-75.

_____. 2006. "Assessing the Authority of a Sermon." *Encounter* 67: 63-74.

_____. 2008. "How do Sermons Help People Change?" *Encounter* 69: 61-75.

Buckley, Reid. 1988. *Speaking in Public.* New York: Harper & Row.

Carrell, Lori. 2000. *The Great American Sermon Survey.* Wheaton, IL: Mainstay Church Resources.

Chapell, Bryan. 1994. *Christ-Centered Preaching.* Grand Rapids, MI: Baker Books.

Cooper, Lane. 1932. *The Rhetoric of Aristotle.* New York: D. Appleton-Century.

Flemming, Dean. 2005. *Contextualization in the New Testament: Patterns for Theology and Mission.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Freire, Paulo. 1973. *Education for Critical Consciousness.* New York: Continuum.

Goldsworthy, Graeme. 1991. *According to Plan: The Unfolding Revelation of God in the Bible.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Harris, R. Mark. 2004. *Thus Saith the Youth Pastor.* Unpublished manual.

Hiebert, Paul. 1987. "Critical Contextualization." *International Bulletin of Missionary Research* 11: 104-12.

Jamar, Steven. 2001. "Aristotle Teaches Persuasion: The Psychic Connection." *The Scribes Journal of Legal Writing* 8: 61-102.

Johnson, Dennis. 2007. *Him We Proclaim: Preaching Christ from All the Scriptures.* Phillipsburg, NJ: P&R.

LeBar, Lois, and James Plueddemann. 1995. *Education that is Christian.* Colorado Springs, CO: Chariot Victor.

Mack, Burton. 1990. *Rhetoric and the New Testament.* Minneapolis: Fortress.

Mulligan, Mary Alice, Diane Turner-Sharazz, Dawn Ottoni Wilhelm, and Ronald Allen. 2005. *Believing in Preaching: What Listeners Hear in Sermons.* St. Louis, MO: Chalice.

Osborne, Grant. 1991. *The Hermeneutical Spiral.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Pieterse, H. J. C. 1984. "Contextual Preaching: To Gerhard Ebeling on his seventieth birthday." *Journal of Theology for Southern Africa* 46: 4-10.

Piper, John. 2004. *The Supremacy of God in Preaching.* Grand Rapids, MI: Baker Books.

Plueddemann, James. 1994. "Do We Teach the Bible or do We Teach Students?" *Africa Journal of Evangelical Theology* 13: 44-53.

Reed, Eric. 1999. "The Preaching Report Card: Today's listeners grade pastors on what they hear from the pulpit." *Leadership* (Summer): 82-87.

Scharf, Greg. n.d. Trinity Evangelical Divinity School, H561—course lecture.

Stanley, Andy, and Lane Jones. 2006. *Communicating for a Change.* Colorado Springs, CO: Multnomah.

Stern, Herbert. 1991. *Trying Cases to Win.* Eau Claire, WI: PESI.

Stott, John. 1982. *Between Two Worlds: The Challenge of Preaching Today.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Theis, John. 1981. "Pronouns and Interpersonal Contact: Assessing the Impact of the Sermon." *Journal of Pastoral Counseling* 16 (Spring-Summer): 47-52.

Webb, William. 2001. *Slaves, Women & Homosexuals: Exploring the Hermeneutics of Cultural Analysis.* Downers Grove, IL: IVP Academic.

Westminster Confession of Faith. 1646. Available online at: http://www.reformed.org/documents/wcf_with_proofs/index.html.

DIBAJI A

https://portal.tiu.edu/files/uportal/teds/ptdept/Scharf.InterrogativeBibleStudy.pdf

MASOMO YA BIBLIA YA KINA KWA MAHUBIRI

Greg Scharf, Associate Professor of Pastoral Theology,
Trinity Evangelical Divinity School[3]

"Usiniulize swali lolote nami sitakueleza kweli zozote."

Mafikirio:

- Kujifunza kwa umakini juu ya dhana ya andishi lisemwalo ni sehemu muhimu ya sharti la mahubiri makini. Jinsi tunavyojifunza ndivyo kunavyoundika mahubiri.
- Uchunguzi sahihi unaweza ukaimarishwa na maswali ya dhati ya dhana ya mstari. Maswali yatasaidia kuuelewa mstari; mengine yatasaidia sana katika kuandaa mahubiri ya dhana hiyo.
- Hatuwezi kuhubiri kiuaminifu dhana ya mstari kupita linayosema. Ni lazima tujaribu kugundua kile linachojaribu kutekeleza, na jinsi ya kutekeleza.

Maswali yaliyopendekezwa (yakiwamo mawili muhimu sana yanayoulizwa na Haddon Robinson) kuongezea yale ambayo tayari unayauliza:

1. ***Je tuna nini hapa? (Andishi hili lina nini kiutekelezaji?)***

- amri
- taarifa ya tukio, mazungumzo, maombi.
- tamshi la ukombozi wa Mungu
- onyo
- tamko, "Asema Bwana"
- maelekezo ya ki-Ungu

[3] Dr. Scharf ni Mkuu wa Idara ya Theolojia ya Kichungaji ya Trinity Evangelical Divinity School, Deerfield, IL. Ni mtunzi wa *Prepared to Preach* (Christian Focus, 2005). Sehemu hii na Dibaji B imetumiwa kwa ruhusa ya Dr. Scharf. Mabadiliko madogo yamefanywa na Jonathan Menn kwa ruhusa ya Dr. Scharf.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- mfano
- ushuhuda
- ukiri
- wito
- kipindi cha mpito
- kiungo katika historia ya ukombozi
- ombolezo
- kutia moyo, au kuinua
- mkondo wa kizazi
- salamu au maneno ya Baraka
- wimbo

2. ***Kifungu hiki kinahusu nini?***[4] ***(Ni somo gani kuu kwa mstari huu?)***

Kwa mfano, kifungu hiki kimsingi kinahusu:

- maombi
- imani
- utii
- mafundisho
- uasi
- uzinzi
- hofu
- furaha
- serikali
- njia za Mungu
- au ni nguzo ya masomo mengine.

3. ***Mwandishi anasema nini kuhusu somo hili?***

Katika kujibu swali hili sisi tutafanya yafuatayo:

- Chunguza nini kingine (zaidi ya kile kinachoonekana kama ni somo kuu) kinatajwa katika mstari.
- Fupisha dhana ya kifungu kama ihusianavyo na somo la kifungu hicho.
- Tambua jinsi maswala mengine yaliyotajwa katika dhana hiyo ya maandishi yanavyohusiana na hilo unaloliita somo lako.

4. ***Ni mwitikio gani anaoutaka Roho Mtakatifu kwa waamini wasomao dhana ya maandishi hayo? (Kwa nini Roho Mtakatifu aliona ni muhimu dhana hii iingizwe katika Maandiko?)***

Kwa mfano, Roho Mtakatifu anaweza kutaka kupatikane:

- toba
- kumtumaini Mungu
- ukiri wa dhambi, kumkiri Kristo
- idadi yoyote ya aina za utiifu.

5. ***Je kifungu hiki kitamsukumaje msomaji kufanya uamuzi uliokusudiwa?***

Swali hili linalenga mkazo wetu kwenye jinsi dhana iliyotangulia inavyoonyesha maandalizi kukamilisha kusudi hilo. Tukiwa tumejizatiti kwa uelewa huo, tunaunda ujumbe wetu kwa kutumia vipengele ambavyo kifungu chenyewe kinatumia ili kutimiza kusudi ambalo kwalo liliandikiwa. Kwa mfano, twaweza kuona:

- vitu vya ustadi wa uandishi wa mvuto
- kuhoji
- mifano, yote miwili - mizuri na mibaya
- hofu ya Mungu kwa maafa yenye kuhuzunisha yaliyotajwa
- kutajwa kwa faida za imani itokanayo na utii
- hoja za mwandishi, k.m., **1 Wafal 12:15**
- kusihi moja kwa moja
- matumizi ya maneno maalum ya kiuandishi. Hivyo, kwa mfano, ushairi unaweza kutumika au msemo unaokumbukika kuamsha usikivu wa msikilizaji, k.m; **Zab 84:3**, ambayo huzungumzia kuhusu shomoro na mbayu wayu wafanyao kiota karibu na madhabahu ya Mungu.

6. ***Kifungu hiki kinachangiaje kwenye ile picha kubwa zaidi ya ukombozi?***

- Inamwelekeaje Kristo?

[4] Haddon Robinson katika *Biblical Preaching: The Development.*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Je iko wapi katika mkondo wa Ki-Bilia?
- Je ilileta matokeo gani kwa wasikilizaji wa mwanzoni kabisa/ au wasomaji?

DIBAJI B

https://portal.tiu.edu/files/uportal/teds/ptdept/Scharf.ChecklistforBeginners.pdf

HATUA ZA UJUMBE: VIDOKEZO VICHACHE KABISA KWA WAHUBIRI

Vimetolewa na kukusanywa kutoka vyanzo mbali mbali kutoka kwa Dr. Greg Scharf
Imerudiwa February 15, 2002; August 8, 2007

I. Omba wakati wote wa mchakato.

Mwombe Mungu ili ujitose kikamilifu, akupe hekima, uelewa, umakini, kutambua, kumpenda Yeye, Neno Lake na watu Wake. *Hutaumia kujifunza ukiwa kwenye magoti yako.*

II. Chagua dhana ya andishi (pia huitwa sehemu ya kuhubiri au kifungu).

A. ***Ikiwa sehemu hii ya mfululizo wa jumbe hutangulia mapema kabisa kabla ya tukio lenyewe la kuhubiri.***
Miezi kadhaa kabla mfululizo huo kuanza, chagua kitabu cha Biblia au dhana ya somo ambalo:

1. Huzungumzia mahitaji ambayo unaona washirika wanayo, au wasikilizaji wako wanajisijia ndani mwao (au yote mawili).
2. Huonyesha jinsi Mungu alivyosema kwako au njaa uliyo nayo unayojua imetoka kwa Mungu.
3. Huweka uwiano wa chakula cha kiroho. Ikiwa umekuwa ukijilisha katika Agano la Kale, fikiria mfululizo kutoka Agano Jipya; kama umekuwa katika simulizi; fikiria, mafundisho ya kimaadili; kama yalikuwa ni vipengele vidogo-dogo, fikiri kwa mtazamo wa mapana, n.k. ikiwa umekuwa ukisisitiza mafundisho, unaweza kuchagua kitabu kilicho na uwingi wa maonyo,marekebisho, au maelekezo katika mambo ya haki, ingawaje vitabu vilivyo vingi na vifungu vingi vina mchanganyiko wa yote.
4. Hulezea theolojia inayoambatana nayo ambayo inahitaji kuimarishwa.
5. Huimarisha kweli fulani au hoja kuu ya Andiko ambalo Mungu anaonyesha kulielekeza kwa kanisa la mahali hapo, au kwa maeneo mapana zaidi.
6. Huzingatia upeo wa ufahamu na upokeaji wa kanisa hilo.
7. Hutambua urefu wa wakati kwenye saa ya kalenda kuhusu masomo haya.
8. Huendana na majira ya mwaka.

B. ***Ikiwa unahubiri masomo yahusuyo ufafanuzi unaoendelea, na umekichagua kitabu cha Biblia kulingana na vigezo vilivyotajwa hapo juu na vinginevyo:***

1. Soma na usome tena kitabu kizima hadi hoja kuu zinajitikoza na sura ya hoja ya mwandishi wake inakuwa wazi.
2. Pata ushauri wa wenye mamlaka, marafiki,na makala nyingine, ili kuona ni mashauri gani uyakope au uyachukue. Soma utangulizi wao kuona au kujua historia ya nyuma yake, theolojia, tukio, uandishi, na maswala mengine muhimu ya dhana hiyo.
3. Tafiti njia kadhaa ambazo unaweza kuhubiri kitabu hicho, zikiwamo zile za ufundishaji kwa ufafanuzi wa kila kifungu, kuibua hoja maalum, au mahubiri ya masomo kutoka kitabu hicho. Andika plani ya masomo hayo yenye tarehe na mipangilio ya hoja za kuabudu kwenye karatasi, na kutenga siku za mapumziko, matukio maalum, nk.

C. ***Ikiwa unahubiri masomo kuhusu kichwa fulani kutokana na kifungu ambacho hakishikamani chote pamoja, au ujumbe moja au mahubiri:***

1. Hakikisha unakuwa na wazo fulani wakati ukitafuta andishi. Hilo ni kiungo cha ufafanuzi tuutakao—na watu wanahitaji—kufafanuliwa. Ukishatulia kwenye andishi, fuatana nalo linakuongoza, hata kama linaelekea mahali usikokutegemea. Ni heri kupangua mpangilio wa masomo ya jumbe zako, kuliko kupotosha kifungu ili kiendane na fikira zako.
2. Kama ilivyo juu, chagua andishi, kifungu cha jambo husika na urefu unaotakiwa ambao ni wazo kamili lililokamilika.
3. Ruhusu muda mwingi kwa kifungu kujitosheleza kwenye dhana ya fungu zima, mlango wote, kipengele, kitabu, makusanyo, agano na mshikamano wa maandishi uyatakayo, ikiwa unaendelea kukielezea kitabu hicho.

D. ***Kila wakati:***

1. Chagua vifungu vya dhana itakiwayo na urefu ufaao. Uchaguzi wa andishi ni yote mawili- kwa lengo na kwa mada. Usomapo Biblia kwa ajili ya kujilisha kiroho, vifungu fulani vitaruka kutoka kurasa za kitabuni kuja kwako, zitasema nawe, na zitakukamata. Unapovitazama kwa makini zaidi, uwe makini usije ukaacha kipande, wala kujaribu kuelezea kuliko itakiwavyo. *Kila sehemu ya mahubiri lazima iwe sehemu iliyojitosheleza ya wazo, na vizuri zaidi yasiwe mawazo mengi.*
    a. Waweza kuhubiri kiufafanuzi kutoka sentensi ikiwa hiyo inajenga wazo kikamilifu kufanya ujumbe.
    b. Mara zote utahubiri kutoka katika kifungu.
    c. Wakati mwingine—pengine kila wakati—utahubiri kutoka zaidi ya kifungu kimoja.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

d. Wakati mwingine utahubiri kutoka kwenye kifungu au vifungu vingi zaidi.

2. Kinachojalisha ni kwamba sehemu ya mahubiri ionyeshe kwa dhahiri wazo moja inalolijenga. Hilo ni kwamba, linapaswa kuwa na *wazo moja kuu* ambalo mwandishi wa Biblia analijenga katika kifungu.

3. Weka kikumbushio kwa kila kifungu cha kuzingatia, picha ya maneno, mifano, maswali, uelewa, makala ya gazeti au jarida au chochote kingine kinachoweza kuja kichwani wakati unakishughulikia kitabu husika kwa kina.

4. Endelea kusoma na kurudia kusoma kitabu kizima kwa kadiri ya urefu wake na ratiba zako, tafuta viunganishi, marudio, maneno ya utambulishi na misemo. Kama ni tabia yako, weka alama kwenye Biblia yako ili kukumbuka hayo.

5. Soma theolojia na vitabu vinavyozoeleka vinavyoendana na kitabu cha ki-Biblia unachotaka kukielezea.

6. Angalau miezi mitatu kabla, jizatiti kutenga vifungu na tarehe maalum na uzieleze hizo kwa wapangaji ratiba za kuabudu na viongozi wengine wa kanisa.

Sasa kwa vile umepanga masomo na kuchagua andishi, au sehemu ya kuhubiri, hatua inayofuata ni:

III. ***Kujifunza ile sehemu ya kuhubiri.***

Hatua zifuatazo siyo mwisho. Nyingi zake zinaingiliana. Wakati mwingine ufahamu utokao kwa Mungu huja haraka, hata kule kujifunza baada ya hapo huthibitisha tu ulichokipata pasipo juhudi kubwa. Mara nyingi zaidi, hasa kama mhubiri anayeibukia, utahitaji kujipa nidhamu kutumia hatua nyingi, kama siyo zote hizi kabisa, ukimtumaini Mungu aseme na wewe kadiri unavyo "jitahidi kusoma Neno na kufundisha" (**1 Tim 5:17**). Hoja ni kwamba, usipuuze njia aliyotupatia Mungu, wala kuzitegemea hizo pasipo kuutafuta uso wa Mungu kiunyenyekevu na kumwalika kunena nawe kupitia Neno lake. Itakusaidia ikiwa kwa pamoja utakuwa mtazamaji wa madogo na makubwa pia. Chunguza kwa uangalifu kwa ajili ya undani, lakini usipotelee huko. Kumbuka yote uyajuayo kuhusu theolojia na ustadi wa kifafanuzi. Tumia yale uyajuayo tayari ili kukuwezesha kutambua uyaonayo. Kisha tumia yale uyaonayo katika dhana ya andishi hili kuongeza katika yale uyajuayo. Zifuatazo ni hatua katika kujifunza dhana ya andishi:

A. ***Omba kabla, na wakati unaendelea, na baada ya mchakatu wa kusoma, kama tulivyokwisha jadili.***

B. ***Somea mahali na wakati ambapo unatarajia hutasumbuliwa wala kuingiliwa na kitu; basi jizatiti na kuwaza.***

Kimsingi uwe peke yako, bila simu karibu ambayo itakakulazimu kuijibu, na awepo mtu wa kuzuia wageni. Meza yako iwe wazi vya kutosha ili vitu mabali mbali visikamate macho yako; na pia zana zako ziwe karibu mkononi mwako. Kama unatumia kompyuta katika hatua hizi, ni lazima ujiadibishe kinidhamu usije ukawa unafanya michezo nayo.

C. ***Jiadibishe mwenyewe kutofikiri mno kuhusu wasikilizaji na haja zao; au mwenyewe na mahitaji yako kwa ajili ya ujumbe wakati unatazama andishi hilo.***

Haya yote mawili yanaweza kukutenga na hali ya kuona kile ambacho kifungu hicho kinalenga.Yaani, yanaweza kuleta upotoshaji, badala ya ufafanuzi makini.

D. ***Soma au jaribu kusoma andishi katika lugha yake asilia angalau mara moja,kama unaweza.***

Angalia maneno yaliyotumiwa. Tumia itifaki na vitu vingine ili kupata maana sahihi.

1. Uwe makini kwa taaluma ya lugha ilivyoandikwa na uandishi wake. Kwa mfano, ikiwa vitenzi vinaelekeza, usikigeuze kifungu kuwa ni amri kama kwamba ni agizo, mpaka pawe na sababu nzuri katika dhana nzima ya kufanya hivyo.

2. Ikiwa kifungu ni simulizi ndefu au sehemu ya kihistoria na uwezo wako kuelewa lugha si mkubwa sana, fanya kila uwezalo kwa muda ulio nao. Lengo lako ni kusoma simulizi si utafiti mdogo, tathmini kitaaluma ya lugha, bali kuchunguza lile tukio, lilivyotokea, mpangilio, mtazamo wake, tabia yake, majibizano na mbinu stadi za uelewa maandishi na vipengele vya staili ambavyo vinamsaidia mwandishi kuelezea hoja yake. Kwa mfano, unaweza kuangalia yale yanayorudiwa-rudiwa, yaliyoachwa, yaliyojumuishwa, ya kuburudishia, ya kukazia msimamo, nk.

3. Mwombe Bwana akusaidie kuimarisha ustadi wa kuelewa ndani zaidi yake na hata kati ya mistari. Kusudia muda mwingi wa kuchimba ndani ya dhana ya andishi, wa kumeza na kutafakari.

E. ***Fanya tafsiri yako mwenyewe, ukiiandika kwa namna ambayo inaelekeza muundo wake.***

Orodha ya vidokezo inalifanya hilo vizuri. Ikiwa una matatizo na lugha ya asilia, usikate tamaa. Kupunguza kasi katika hatua hii ni vizuri. Utaelekea sana kuona undani fulani kwa mfano vitu vinavyorudiwa, ulinganishi kati ya viwili tofauti, viunganishi, mpangilio wa maneno, makusudio, n.k.

F. ***Soma na urudie kusoma andishi katika Biblia sehemu unayokusudia kuhubiri, na uandike chochote kinachokugusa.***

Huu ni wakati mzuri wa kutazama:

1. Maneno yanayounganisha, semi za kusudio, viungo, vipingamizi na mifano mingine ya kiuandishi na taaluma ya lugha. Kumbuka kwamba maneno hupata maana yake kutokana na kazi katika sentensi na pia kujifunza asilia ya maneno hayo, ambayo ndiyo hasa chimbuko la maana zake.
2. Maumbo, vitu vingine vya hotuba, na mifano.
3. Marudio, ambayo kimatamshi yamepigiwa mistari.
4. Maneno yaliyo funguo za kitheolojia: neema, upendo, hofu, kweli, furaha, nk.
5. Wahusika.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

6. Mpangilio.
7. Lugha ya kimamumbo.
8. Yaliyotiwa chumvi.
9. Tafsiri nyingine mbadala
10. Mifananisho.
11. Uebrania
12. Maneno yasiyo katika mpangilio wa kawaida.
13. Hotuba yenye mtindo maalum, au ya kizamani.
14. Maswali ambayo andishi linaonyesha kuuliza, yawe yametajwa au hayajatajwa.
15. Matatizo ambayo andishi linajaribu kuyataja akilini mwako, au yanayoweza kutegemewa kuinuka katika akili za wasikilizaji wako.
16. Ladha na hali ya andishi.

G. ***Kazia macho kwenye dhana.***

Karibu kila andishi lina dhana. Hili linachanganya desturi na theolojia ya dhana kama ilivyo dhana ya kiuandishi kwa kifungu ndani ya kitabu, maneno, au kauli.

H. ***Soma kifungu hicho katika tafsiri nyingine kwa kutafuta uelewa zaidi ambao huenda huujui.***

Lengo la hoja hii ni kupata kukielewa kile *kilichopo* katika andishi. Hii ndiyo hatua katika kusoma Biblia ambacho wengine wanakiita *kuchunguza.*

I. ***Chunguza andishi.***

Huu ndio moyo wa usomaji wa Biblia. Anzia na kuhoji yale ya msingi kabisa (nani, Nini, lini, Kwa nini, na Vipi) ya kuelekea ndani zaidi ya kifungu hicho. Maswali ya lazima ni pamoja na:

1. Andishi hili ni nini? M.y; kulingana na jinsi lilivyo kwa maneno yake, tambua kazi yake katika dhana iliyopo. Kwa mfano, Je hili ni onyo, maombi, taarifa, maelezo, ufafanuzi, mithali, shambulio la maneno, hoja, kutia moyo, fundisho, mfano, kitu kingine, au mchanganyiko wa haya au vitu vingine? Hili kikawaida huwa dhahiri, lakini mara nyingi husahaulika. Hii huhusiana moja kwa moja na jinsi ujumbe wako utakavyokuwa. Kwa mfano, ikiwa kifungu unachokielezea ni onyo kuhusu matokeo ya kutotii, ujumbe wako uwe wa kuonya kuhusu matokeo ya kutokutii vivyo.
2. Je mwandishi anaandika kuhusu nini? M.y; nini kichwa cha kifungu hiki? Sehemu hiyo itataja au kuhusisha vitu mbali mbali. Unahitaji kutambua ni kipi kati ya hivyo ndicho kitu kikuu.
3. Je mwandishi wake anajaribu kusema nini kuhusu somo lake? M.y; sehemu iliyobakia je inaendana na kichwa?
4. Mwitikio gani anaotaka Roho Mtakatifu kwa wale wataosikia au kusoma kifungu hicho?
5. Je kifungu hiki kinamsukumaje msomaje afanye lililokusudiwa? M.y; angalia na kujifunza mwandishi aliyevuviwa anavyolijenga wazo la dhana husika. Kwa mfano ikiwa andishi linafanya hivyo kwa mtindo wa mahojiano badala ya mifano, unaweza ukahitaji ujumbe wako ukusanye nguvu kwa njia kama hiyo hiyo.
6. Je kifungu hiki kinachangiaje kwenye picha kubwa zaidi ya ukombozi? Usiamue tu kifungu kikoje, lakini pia ujue kinaingiaje katika picha kubwa zaidi ya Maandiko. Ili kufanya hilo, angalia jinsi andishi hilo linavyotenda kwenye kitabu na mfululizo wa maandiko yote. Kwa nini Roho Mtakatifu aliingiza kifungu hicho katika Biblia? Je sehemu hii inachangia nini katika ujumbe mkubwa zaidi wa Biblia? Hilo, bila shaka, litahusisha jinsi linavyoelekeza kwa Kristo. Nini *kusudi* la kifungu hiki? Hilo litaelekeza jinsi litakavyofanya kazi katika kanisa.

J. ***Tazama mkondo wa kifungu unavyokutahadharisha vitu fulani.***

Ona hasa sehemu V. “Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuhubiri simulizi,” na VI. “Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuhubiri mashairi na unabii,” hapo chini.

K. ***Endelea kuuliza maswali hadi uwe umekamata maana ya kutosha ya andishi hilo.***

Huku ndiko *kutafsiri.* Lengo ni kugundua *nini* kifungu kinamaanisha (yaliyomo) na *kwa nini* kiko katika Biblia (kusudio lake). Ingawaje tunakabili utazamaji tukiwa na fikira za kuwazia uchache iwezekanavyo, kutafsiri kunahitaji uelewa wa kutosha wa Ki-Biblia na kitheolojia kuuliza maswali yatakayokusaidia kugundua kusudi la Mungu katika kukiweka kifungu hicho katika mchanganyiko wa Maandiko mazima. Yeye aliye nacho ataongezewa zaidi. Unaona kile ukijuacho.

L. ***Fikia uamuzi wa msingi kuhusiana na kifungu unachokisoma.***

Kujiuliza maswali mazuri kuhusu andishi, lazima ufikie maamuzi kadhaa.

1. Tenga, au tengeneza kauli moja, rahisi ya nguvu ya kifungu. Nini Mungu anasema kwa kanisa kupitia alichoandika mwandishi wa ki-Biblia? Ukishagundua hilo, sehemu zote za kifungu zijengwe kuelekea kweli hiyo, ongoza kutokea hicho, au jihusishe nacho kwa njia inayodhihirika. Kama hayatakuwa hivyo,unaweza ukawa bado hujagundua kitovu hasa cha kifungu hicho. Uchunguzi wako wa viunganishi, makusudio, n.k; utakusaidia kuona viunganishi vya kifungu. Dumu katika kujifunza hadi wazo kuu linajitokeza na kuwa wazi kabisa. Liandike hilo.
2. Kagua maamuzi yako na uyarekebishe kwa kuangalia mamlaka nyingine kama vile maoni, theolojia na vifaa zana nyingine. Daima inalipa kuanzia naoni ya kitaaluma na ndipo uendelee na hayo yaliyozoeleka zaidi. Wengine wanaweza kutumia maoni ya kitaalamu kama sehemu ya tafsiri na kwa kugusia hatua zilizotajwa hapo juu. Kama umeamua kufanya

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

hili, angalia usimfanye mwingine awe anafikiri kwa ajili yako wewe.

M. ***Acha kifungu kiseme nawe.***

Tenga muda kwa ajili ya hili. Jikabidhi kwa kweli hiyo uliyoiona; tafuta nuru zaidi; jinyenyekeze mwenyewe mbele za Mungu; tafakari juu ya hiyo kweli kuu.

1. Pasipo kuelewa kifungu kinasemaje, na kwa nini; na pasipo hicho kusema na wewe, usijaribu kukihubiri. Mamlaka yako kama mhubiri yanatokana na kuhubiri kile ambacho andishi linakifundisha, ingawaje ni kwa wasikilizaji tofauti na wale wa kwanza walioandikiwa.
2. Ikiwa kifungu hakineni nawe, tafuta vizuizi vya kiroho au vya kimahusiano ambavyo vinaweza kuwa vinakufunga kwenye ujumbe huo. Kisha muulize Mungu kama umekiacha kitu katika kifungu hicho au kama iko sababu nyingine kwa nini Neno lake haliingii ndani mwako. Hili linaweza kutokea wakati unadhania kwamba huu ni ujumbe tu kwa ajili ya wengine na kujiweka mwenyewe juu zaidi ya dhana ya andishi. Kipindi fulani katika juma, unahitaji kuendelea kwa imani na kukiri kwamba ikiwa Mungu aliweza kusema kupitia punda wa Balamu, anaweza kusema kupitia kwako hata kama nguvu ya dhana ya andishi hilo kwako ni ndogo kuliko unavyotaka.

Baada ya kutambua kwa uwezo wako wote msukumo mkuu wa kifungu, lazima sasa:

IV. Uunde kile kisemwacho katika kifungu kuwa ujumbe (m.y, ufafanuzi wa andishi ambao utahubiri).

Hili linahusisha, kwa kiwango cha chini kabisa, hatua zifuatazo.

A. ***Fikiri juu ya uhitaji wa washirika kuhusiana na msukumo ulivyo katika kifungu hicho.***

Muulize Bwana anataka kusema nini kupitia andishi hilo kwako kabla wewe hujafanya hivyo kwa watu awajuao watakuwapo kwenye ibada siku ambayo utakwenda kuhubiri.

B. ***Andika kichwa cha ujumbe wako.***

Kimsingi, weka kichwa cha ujumbe kiwe cha kueleweka, chenye kauli ya nguvu kuhusu msukumo mkuu wa kifungu *kwa jinsi kinavyohusiana na washirika.* Kauli hii rahisi inafupisha kile unachoamini Bwana anataka wewe usema kwa washirika kutoka kwenye kifungu unachokihubiri. Kichwa hicho kitapaswa kionyeshe uaminifu, umoja, utimilifu, na kueleweka.

Kwa mfano, ikiwa unahubiri **Waeb 12:1-11** kichwa chako kinaweza kuwa, *"Dumisha msimamo wako kwa Kristo!"*

C. ***Kipime kichwa chako.***

Uliza maswali kama haya:

1. Je kichwa kimetajwa karibu na mwanzo wa ujumbe kuhubiriwa?
2. Je nimekitaja kichwa hiki mara kwa mara? (Je itamchukua mda mrefu kiasi gani mtu aliyechelewa kuja ibadani kuelewa nazungumzia nini?)
3. Je nimewaandaa wasikilizaji wangu kwa ajili ya kichwa hicho?
4. Je kichwa hicho kiko wazi na ni kimoja na siyo ni mawazo mengi yasiyohusiana yaliyolundikana pamoja?
5. Je kichwa kimenyokeana, au kina maneno au mawazo yasiyo ya lazima?
6. Je kichwa hicho kinaendana na watu wa sasa tofauti na kuelezea tukio tu Ala nyakazi zile za ki-Biblia@?
7. Je kichwa hicho kinalenga mtu binafsi, kiko rahisi, na hakina kona?
8. Je kichwa hicho kinakumbukika?
9. Je msikilizaji mwenye akili sana, aliyejazwa na Roho, anayekisoma kifungu hicho kwa uangalifu, atakubali kwamba kichwa hiki kinaonyesha kiusahihi kweli kuu ya kifungu?

D. ***Rekebisha kichwa cha somo kila iwezekanavyo.***

E. ***Kipitie kifungu unachokielezea kuona jinsi kinavyojenga hoja za kichwa unachokihubiri.***

1. Tumia taarifa hizi kutengeneza vidokezo vyenye hoja kuu ambavyo siyo tu vinajenga wazo la kichwa cha somo, bali vinahusiana na kila kimoja kinamna fulani iliyo rahisi kupokea na kukumbukika. Kimsingi, uhusiano huo utapendekezwa na muundo wa kifungu hicho.
2. Mahusiano hayo hufungiwa ndani ya *sentensi ya kimpangilio.* Sentensi hii haitaji kilichomo katika kifungu au ujumbe; bali hutahadharisha wasikilizaji jinsi unavyopanga kujenga wazo la kichwa chake.

F. ***Andika sentensi ya mpangilio.***

1. Hii huweza kuwa aina moja wapo, lakini namna iliyo rahisi kabisa ni kuwa na neno la ufunguo ambalo ni jina katika hali ya uwingi, likaboreshwa kwa idadi ya hoja kuu ziendanazo na vidokezo kwa pamoja kuchanganya na utendaji wa kutosha kuelezea uhusiano kati ya kichwa na hoja kuu. Kwa mfano, katika ujumbe kuhusu **Waeb 12:1-11**, ikiwa kichwa ni *"Dumisha msimamo wako kwa Kristo,"* sentensi ya kimpangilio inaweza kuwa, *"Kifungu kinatupatia sababu tatu kudumisha msimamo wetu kwa Kristo, hata wakati haielekei kuonyesha uthamani wake: (1) Kristo amehakikisha matokeo; (2) Umebadilishwa; (3) Mungu anamiliki."* "Sababu" ndio ufunguo wenyewe. Huo ufunguo siyo somo la kifungu au ujumbe. Unaelezea uhusiano kati hoja kuu, ambazo kila moja ni sababu katika hili. Maneno ya funguo yaweza kuwa: "fikira," "kweli," "funguo," "kona," "hatua," n.k.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

2. Kwepa kutumia maneno ya funguo kama vile "mambo" au "hoja" katia sentensi ya kimpangilio kwa sababu ni ya kijumla mno hiiyo hayafai katika makusudi ya kuweka wazi mahusiano kati ya hoja kuu.

G. ***Andika hoja kuu za vipengele.***

1. Katika mfano kutoka **Waeb 12:1-11**, hapo juu, hoja kuu zaweza kuwa:
   a. *Kristo amehakikisha matokeo* (**mst. 1-4**);
   b. *Umebadilishwa* (**mst. 5-8**); and
   c. *Mungu ndiye atawalaye* (**mst. 9-11**).
2. Tambua kwamba katika mfano kutoka **Waeb 12:1-11** hoja kuu zilitajwa mwanzoni katika sentensi ya kimpangilio, na kisha kurudiwa kama hoja kuu katika kiwiliwili cha ujumbe; hilo si lazima liwe hivyo siku zote. Hoja kuu lazima zihusishe wazi kabisa sentensi ya kimpangilio, lakini si lazima kurudia kile kilichonenwa na sentensi ya kimpangilio neno baada ya neno. Kwa mfano katika kuhubiri juu ya **Waef 2:11-16**, kichwa chaweza kuwa, *"Maisha yetu ni mapya katika Kristo."* Sentensi ya kimpangilio yaweza kuwa, *"Leo tutaangalia maisha yetu mapya katika kona mbili: Sisi ni nani haswa katika Kristo, na Tunatakiwa tufanye nini kuhusiana na hilo."* Hoja kuu zaweza kuwa:
   a. *Kristo ametufanya "mtu mpya"* (**mst. 11-16**).
   b. *Kwa vile sisi "ni mtu mpa," lazima tutendeane kama moja.* (**mst. 14-16**).
3. Ikiwa una ugumu kuibua hoja kuu za kweli kuziunga na andishi, waweza kupitia kichwa chako kuelezea andishi linafundisha nini kihalisia.

H. ***Jenga kila hoja kuu.***

Njia za kujengea hoja kuu ni pamoja na:

1. *Kuonyesha* na *kusoma* dhana ya andishi inakotokea. Naliita hili "*kuunganisha*."
2. *Kuthaminisha* hizo hoja. Hili ni la lazima itokeapo hoja kuu haijitoshelezi katika andishi lilikotokea.
3. *Kuelezea,kukuza,kunyambua,na kuthibitisha.* Hili linaweza kuletesha kuongeza rangi kwenye simulizi. Njia sita za kusaidia kufanya hilo ni: kuelezea; mfano; kueleza maana; kufananisha na kulinganisha; tathmini ya mara kwa mara; na kugawanya.
4. *Kuonyesha mfano wake.* Kuonyesha kimfano kunatenda kama daraja kutoka ulimwengu wa ki-Biblia kuja ulimwengu wa sasa. Tambua, hata hivyo, mifano inaweza ikalemea ujumbe.
5. *Kutumia kimatendo.* Hili linahusisha kuwaalika wasikilizaji kujitoa kwenye mafundisho kwa njia zilizo sahihi. Zinaweza kuwa toba, utii, imani, kuabudu au mchanganyiko wa hizo au mwitikio mwingine. Jukumu letu ni kuagizia mwitikio ambao andishi linahitaji ufanyike.

I. ***Andika hitimisho la ujumbe wako.***

Hili siku zote litahusisha kurejea na kutumia kile kichwa. Hili pia laweza kujumuisha hoja kuu. Hapa ndipo unaporejesha ujumbe kitovuni pake.

J. ***Andika utangulizi wa ujumbe.***

Hili linapaswa kinamna fulani liibue swala au swali ambalo andishi linaloelezewa linajibu.

K. ***Andika ujumbe kikamilifu.***

Kazia kuchagua neno bora kabisa kila mahali, na mabadiliko ya wazi ambayo, mara kwa mara huunganisha sehemu zote za ujumbe kwa kile kichwa.

L. ***Fupisha maandishi kuwa nukuu zenye urahisi.***

M. ***Fanya mazoezi ya ujumbe kwa sauti.***

Kimsingi jaribu kufanyia mazoezi mahali pale pale utakapouhubiria, mpaka uwe umelizoea somo lako ulililoliandaa.

N. ***Uhubiri ujumbe kwa nguvu za Roho Mtakatifu.***

Kwa maombi kabisa mwombe Mungu anene kukupitia wewe.

O. ***Mwagilia mbegu ya Neno kwa maombi.***

V. Mambo maalum ya kuzingatia unapohubiri simulizi (m.y; hadithi; simulizi za kihistoria).

A. ***Nyanja maalum za simulizi (kinyume na nyaraka za kimaadili).***

1. Matumizi ya simulizi. Mwombe Bwana akusaidie kujenga ustadi wa kusoma ndani zaidi na hata kuonyesha yaliyoko kati ya mistari.
2. Sehemu ya kiini kwa simulizi hiyo, yaweza isiwepo kwenye andishi lenyewe, bali ikawa nyuma au mbele yake.
3. Katika kuhubiri simulizi,inasaidia kuuliza, *ni nani ambaye unataka wasikilizaji wako wamfananie katika simulizi hiyo?* Kichwa chako kinaweza kukazia theolojia ya kifungu, au masomo mazuri au mabaya yaliyomo, kulingana na nani unayetaka kusanyiko limfananie.
4. Kueleza simulizi ndani ya simulizi kwaweza kuwachanganya wasikilizaji.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

5. Ni rahisi kusahau simulizi katika manabii.

B. ***Kuhusu sehemu ya mahubiri:***

1. Kama ilivyotajwa hapo juu, chagua kama andishi la kuhubiri, kifungu chenye mambo yafaayo na yenye urefu utakiwao ambao ni kipande kamili cha wazo. Kinachojalisha kwamba, sehemu ya kuhubiri kiudhihirisho kabisa inapeleka wazo moja ambalo linaliibua kwa njia ya hedaya au simulizi ya andishi. Hilo maana yake, kunapaswa kuwe na wazo linalotawala ambalo mwandishi wa ki-Biblia analijenga katika kifungu. Ikiwa sehemu ya simulizi katika Maandiko inaruka vifungu kwa vile havitaji kweli unazojisikia washirika wanahitaji kusikia, angalau kwa kiwango kidogo onyesha jinsi vifungu hivyo ulivyoviruka vinavyochangia katika ujumbe wote kiujumla, na jiandae kwa ajili ya kifungu unachokielezea.
2. Ufunguo ni kutafuta hoja anayojaribu kuitaja mwandishi katika simulizi hiyo. Kwa nini Roho Mtakatifu alikijumuisha kifungu hiki katika mafululizo wa maandishi hayo? Inaweza kuhusiana na mtu fulani aliyeanguka dhambini katika simulizi hiyo, au tabia ya Mungu kama ilivyofunuliwa katika simulizi hiyo, lakini yote mawili yatakuwapo. Kipi utakisisitiza katika ujumbe wako kitategemeana na uelewa wako wa mahitaji ya washirika wako.

C. ***Kuchunguza simulizi ya andishi.***

Yafuatayo ni mambo muhimu kuyafanya kuhusiana na andishi la simulizi:

1. Mpangilio wake (muda, mahali).
2. Mtazamo wa msimuliaji.
3. Wahusika wake na jinsi wanavyoelezwa.
4. Mazungumzo, na jinsi yanavyoingizwa.
5. Mwendelezo jinsi kisa kinavyoendelea tangu mwanzo hadi mwisho.
6. Maneno, hasa maneno ya kitheolojia na maneno yanayoelezea.

D. ***Kuhoji andishi lenye simulizi.***

Yafuatayo ni maswali ya muhimu kujiuliza wakati wa kuchunguza andishi la simulizi:

1. Nini dhana ya simulizi hii? Ni mazingira gani au hali gani inayowekwa kwenye simulizi hii? Kazia sehemu yoyote au kipengele chochote chenye mvutano ambacho kinahitajika kitatuliwe?
2. Nani anayesimulia kisa hiki? (Hili linasaidia kujenga mtazamo.)
3. Ni nani wahusika wakuu wa simulizi? Nini waweza kugundua kuhusu hao kutokana na andishi lenyewe? Kutoka vyanzo vingine?
4. Ni mahali gani yanafanyikia mazungumzo katika simulizi?
5. Je kuna sehemu ambayo ina mtu moja tu anayeongea katika simulizi?
6. Je kuna maoni ya uhariri? Yazingatie hayo hasa kwa vile yanaweza kuwa na ufunguo uliovuviwa wa simulizi hiyo.
7. Je kuna simulizi zozote nyingine ndani ya simulizi
8. Nini mpangilio wa msingi kwa maelezo rahisi kabisa? (Kikawaida)
9. Nini sehemu za simulizi hiyo? Fikiria vipengele, au vipande vya onyesho, au milango katika kitabu.
10. Je kipande kinachoelezwa kinachangia picha iliyowekwa na simulizi hiyo? 11. Ikiwa simulizi ina somo, ni lipi hilo?
12. Ni maneno gani yanayochangia zaidi kwenye wazo la simulizi?
13. Je simulizi hii inachangia kiasi gani kwenye ile hoja kubwa zaidi ya kitabu hiki? Je inatendaje kazi⊂m.y; je inaonya, inatia moyo, ni mafundisho, mfano, nk.?
14. Ni mwelekeo gani wa kihisia upo katika simulizi hiyo?
15. Ni sehemu gani tena katika Biblia washiriki hawa au tukio hili linatajwa tena; na tunaweza kujifunza nini kwenye hizo sehemu?

E. ***Kuhusiana na kichwa:***

1. Uliza jinsi kifungu cha simulizi unachokielezea kinavyojenga hoja za kichwa unachokihubiri. Kwa ujumla, simulizi au kisa kitaweka hoja yake ama kwa vipengele vilivyomo kimoja kimoja ambapo ujumla wake hufanya hoja kuu (kiitwacho kwa mzunguko), ama kama kitu kizima (kiitwacho simulizi ya kimatumizi).[5]
2. Kugundua jinsi inavyojenga hoja yake, chunguza vipengele vya matukio yake, au sura zake za simulizi tukiuliza kama mwandishi anavitumia hivyo kujengea hoja yake, kufundisha somo, n.k;.. au kama, kwa upande mwingine, ni matofali tu ya kujenga kuelekea hitimisho kubwa zaidi. Ikiwa lile la mwanzo ndilo lenyewe, kila sehemu inayofanya kazi; ikiwa ni ile ya mbele ni wazo kuu tu lililoletwa basi sehemu zote kwa pamoja hutumika. Hili litakuongoza wewe jinsi utakavyoieleza simulizi hiyo na jinsi unavyoitumia.
3. Kulingana na urefu wa andishi, unaweza kuamua kusoma na/ au kuelezea kisa kizima, ukihusisha sehemu zake na kurandanisha na maisha ya leo, na kualika utendeaji kwa kila kipande cha tukio. Ikiwa sehemu hizo hazisimami peke yake, utahitaji kusoma au kueleza simulizi timilifu na kuiweka iwe ya siku za leo na kuitumia yote kule mwishoni.

[5] Maoni haya yanatoka kwa Dr. Harry Shields' 1996 Trinity Evangelical Divinity School D. Min. Andiko la kiutafiti: *Toka Hadithi Yake hadi Hadithi Yetu: Ni mwongozo wa ustadi kwa Simulizi ya Kiufafanuzi ya Agano la Kale.*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

F. ***Kuhusiana na sentensi ya kimpangilio:***

Sentensi ya kimpangilio kwa ajili ya ujumbe wako hunufaisha hata wakati wa simulizi ambapo ungeweza kuamua kutoiibua kwa sababu kuisimulia hadithi ile vizuri kunafunua mwendelezo wa kifungu na kuunganisha vipengele pamoja. Yaani, unaweza bado ukaona inasaidia kuimegua simulizi katika "Vipande vya matukio," au kuona kwa mfano, "mazungumzo" matatu, au kugundua "makosa" manne, aliyoyatenda mhusika mkuu.

VI. <u>Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuhubiri ushairi na unabii.</u>

A. ***Kuhusu sehemu ya kuhubiri:***

Kama ilivyotajwa hapo juu, chagua andishi la kuhubiri, kifungu chenye ujumbe husika na chenye urefu ufaao ulio kipande timilifu cha wazo. Mara nyingi hili litahusisha Zaburi nzima, tamko zima, ombolezo lote, n.k. Kama vile tusingeelezea ubeti wa wimbo au shairi, lakini jaribu kulidaka lote, kwa hiyo si vyema sana kutaka kuelezea sehemu tu ya shairi.

B. ***Kuchunguza andishi la kishairi au la kinabii.***

1. <u>Angalia usambamba, mrandano, mwenendo, mshikano, yaliyoachwa, maneno yaliyorudiwa, maneno yanayogawanya vifungu, na mistari inayofungamana, na pia sehemu nyingine ambazo ni ngumu kuzipata katika lugha ya Kingereza.</u> Jaribu kugawanya shairi kwenye mistari inayofungamana au mafungu.
2. <u>Katika kusoma na kurudia kusoma andishi katika Biblia ambalo unataka kulihubiri, uwe unaandika chochote ambacho kinakugusa.</u> Hakikisha unakuwa makini na:
    a. Lugha ya kimaumbo
    b. Kutiwa chumvi
    c. Tafsiri inayokaribia
    d. Mifananisho
    e. Uebrania
    f. Utaratibu wa maneno usio wa kawaida
    g. Hotuba iliyo katika mtindo maalum, au ukale.
    h. Vitu vingine na fasihi ya kinabii.

C. ***Kuchunguza andishi la kishairi au unabii.***

Huu ndio moyo wa kujifunza Biblia.Anzia na kuhoji mambo ya msingi (Nani, Nini Lini, Wapi, Kwa nini, na Vipi) ili uweze kuingia ndani ya kifungu. Katika ushairi na unabii, maswali haya yanaweza kuhusisha:

1. Nani anayesema ?
2. Ni kwa nani au kwa ajili ya nani liko shairi hili, tamko hili, au maelekezo haya yaliandikwa?
3. Kinamhusu nani kifungu hiki kilichoandikwa?
4. Ni kipindi gani maandishi haya yanahusu?
5. Ni mahali gani, au sehemu zipi zinatajwa?
6. Ni msisimko gani au sura gani kifungu hiki cha ushairi kinaunda?
7. Ni maumbo gani yanaumba hali inayotegemewa?
8. Ni mtindo gani wa kihistoria ya Israeli unahusishwa? Nini kinatajwa kuhusu watu wa Mungu, adui za Mungu, na mataifa?
9. Ni mitindo gani ya kujieleza, au misemo ya kawaida inayotumiwa?
10. Vipengele vya kifungu hiki vinaelekea kufikia kujenga hitimisho

D. ***Mahitimisho ya msingi kuhusiana na andishi la kishairi au kinabii.***

Unahitaji kufikia angalau *maamuzi ya msingi manne kuhusiana na kifungu* unachojifunza:

1. <u>Ni nini hicho?</u> (Je ni karipio? Ni ombolezo? Ni tenzi ua kusifu? Ni kitu kingine?)
2. <u>Nini kinazungumziwa?</u> (M.y. Somo ni nini?—Mungu, watu wake, hitaji la mwanadamu, utakaso, au masomo maalum mangapi; au zaidi?)
3. <u>Panasema nini kuhusu somo lake?</u> (Kwa mfano; maombi ni muhimu, imani ni thawabu, nk.)
4. <u>Je kinafanyaje kazi katika kitabu, Agano, na maandishi yote kiujumla? (How does it function in its book, testament, and the canon?</u> (Kutilia mkazo hali ya anguko? Kuelekeza zaidi kwa Kristo? Kuwakumbusha wasomaji kuhusu uaminifu wa Mungu?)

E. ***Kuhusiana na kichwa:***

Uliza jinsi kifungu cha kishairi na kinabii unachokielezea kinavyojenga hoja ya kichwa unachokihubiri. Angalia hisia, mitazamo, maumbo, mikazo iliyotokana na usambamba au njia nyingine zinazojaribu kuelekeza kwenye msukumo wa kifungu kwenye dhana yake. Ikiwa huwezi kutenga na kuibua vipengele kama hivyo, unaweza kuhitaji kuangalia upya kichwa chake, mpaka uridhike kuwa sehemu zote zinajengwa kuelekea msukumo uliouona.

VII. <u>Tahadhari nne za kuzingatia akilini.</u>

A. ***Usisome nyuma ya andishi kitu ambacho hakipo hapo, au kuingiza mawazo ambayo ni tofauti na yaliyokusudiwa na***

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mwandishi.

B. ***Mtu akipuuza mitazamo ya Agano la Kale ambayo Agano Jipya limeyachukua na kuyakazia, mtu huyo anapoteza fursa ya kuthibitisha kweli ya Injili****C****k.m. kutahiriwa, ukuhani, uchungaji, Israeli kama kielelezo cha Yesu na Kanisa.***

C. Kutegemea uelewa wa taalmua ya desturi, historia, au lugha huweza kwa kiwango kikubwa kuifunga Biblia kwa wasikilizaji wasio na uelewa mkubwa kwa kuwapa picha kuwa hawawezi kuielewa au kunufaika na Biblia kwa vile hawana uelewa kama sisi wengine.

D. Kufuata hatua za hapo juu, hakukuhakikishii mafanikio.

Lazima siku zote tuutafute uso wa Bwana na kuomba msaada wake tunapofanya maandalizi, na wakati wa kuhubiri. Hata hivyo, hatua za hapo juu zimeandaliwa kutusaidia kuepukana na makosa ya kawaida, na kuongeza uwezekano wa ujumbe wetu kuwa wa uaminifu na wa kueleweka.

DIBAJI C

Math 6:19-24—Muundo wa Fundisho wa Dondoo za Ujumbe[6]

Utangulizi: Fedha. Sote tunazitaka. Sote tunazihitaji. Fedha huweza kufanya mengi mema. Ni bora kuwa nazo kuliko kuzikosa.

Je umegundua Yesu alinena kuhusu fedha zaidi kuliko swala jingine lolote? Tunajua adui mkubwa kuliko wote ni Shetani. Ungelitegemea Yesu angelisema: "Hamuwezi kumtumikia Mungu na Shetani." Lakini sivyo—"Hamwezi kumtumikia Mungu na fedha/ mali/utajiri (m.y; kupenda feedha na mali pamoja." **KWA NINI?**

Hebu fikiri kuhusu hilo: Tunapokuwa wachanga, huridhika tunapopata visenti vichache. Kisha tunakua—vile visenti havitutoshelezi tena. Tunapata ajira—lakini le kazi ya kuanzia haitutoshelezi kitambo kirefu. Twayaona mambo yote tunayotaka kufanyia kazi fedha zetu—kwa hiyo twataka zaidi. Tunapokuwa wadogo twataka baiskeli. Tunaipata. Je hiyo hututosheleza? Kisha tunahitaji gari. Tunalipata. Je linatutosheleza? Kisha tunahitaji gari kubwa zaidi, au mawili. Tunayapata; lakini je huwa tunatosheka?

Kwa nini Yesu alisema, "Hamwezi kumtumikia Mungu na fedha?" Kwa sababu alitambua kwamba huenda kitu kikubwa zaidi ambacho kitakutenga mbali na Mungu ni fedha na kumiliki mali. Sababu ni:

Kichwa: FEDHA NI KIROHO. Ni kiroho sawa kabisa na ule msalaba—naam, fedha zaweza kuwa *kiroho zaidi* kuliko msalaba. **KWA NINI?** Hayo yote ni mambo ya nje. Zaweza kutumiwa kwa mema au mabaya. Watu wengi huvaa misalaba (heleni, mikufu, hubebwa mifukoni)—lakini fedha ***hufunua*** *kile kilichopo moyoni mwetu:* mtazamo wetu kuelekea fedha, na kile tunachotaka kufanya nazo *hudhihirisha zaidi kuliko karibu kitu kingine chochote,* ndiko uliko moyo, akili, nafsi, na vipaumbele .

Kitabu cha Kianglikani cha Sala za Pamoja: Sakramenti = "ishara inayoonekana kwa nje, ya neema ya ndani ya kiroho." Kanuni hiyo hutumika kwa sehemu zote za maisha. Kile tufanyacho na fedha zetu, hudhihirisha jinsi *kiuhalisi* tunavyomuwazia Yesu Kristo**C**kama *"kipimio cha kitaalamu cha kiroho."*

Mangilio wa hoja kuu: Nataka nifanye mambo matatu: (1) Kuangalia hali ya kiroho ya fedha, (2) Kutazama kanisa la kwanza ambalo linalielewa hilo, na njinsi hilo lilivyoathiri ukubwa wa udumiaji fedha zao; (3) Hufanya matumizi maalum kiutendaji kwetu.

I. Hali ya Kiroho ya Fedha

Math 6:19-20—*"Jiwekeeni hazina zenu…" "kujiwekea"* katika Kiyunani, ni neno la kiutendaji la *"hazina"*—m.y, *"Msijiwekee hazina duniani, bali jiwekeeni hazina mbinguni…"*

- **Mst. 21—**HAUSEMI, "mahali ulipo moyo, ndipo hazina yako itakapokuwapo…" (ingawaje hilo ni kweli)—lakini *"mahali ilipo hazina yako, ndipo utakapokuwako na moyo wako."* KWA NINI?
- Huwa tunaweka hazina kile kilicho cha thamani sana kwetu: Mimi namweka hazina mke wangu.Yeye ndiye mtu wa muhimu kuliko wote katika maisha yangu.: Hivyo, nitafanya kila niwezalo kuhakikisha naimarisha uhusiano wetu…. (Siyo kikamilifu—kama awezavyo kukuambia—lakini); ni jinsi *ninavyomtendea yeye* ndivyo inavyodhihirisha jinsi ninavyomuwazia (ndivyo hata sasa hunifanya niwaze…)
- Kwa hiyo Yesu ametupa ishara iliyo ya kimatendo kabisa, ya nje na yenye kuonekana—nini tunafanya na fedha zetu—ambacho hudhihirisha jinsi ilivyo hazina yetu *halisi*: dunia hii, na mambo yake, au Mungu na Ufalme wa Mungu. Kunaonyesha *mioyo yetu iko wapi.*

A. ***Kile tufanyacho na fedha zetu ni anina ya ibada:*** **Math 2:11** (mamajusi); **Marko 14:3-9** (mwanamke mwenye kibweta cha marhamu). Walitoa kitu moja kwa moja kwa Yesu:

1. Lakini Yesu hawezi kudanganyika wala hawezi kupewa rushwa: **Math 15:5-9 [SOMA].** Kuabudu ≠ kuimba & kuja kanisani.

[6] Kwa sehem kubwa, hii ni aina ya mahubiri inayoitwa mahubiri ya somo maalum kuhusu hali halisi ya fedha, japokuwa limezama kwenye kifungu maaum cha maandiko.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

2. Amri 2 Kuu Kabisa: *"Mpende Mungu & Mpende jirani yako"*—Amri ya 2 (jinsi unavyomtendea jirani) kiuhalisi ni ishara ya nje, inayoonekana kama kweli unatekeleza ile ya amri ya kwanza; ni *kipimio cha kitaalamu cha kiroho*—FEDHA NI KIROHO.

B. ***Kile tufanyiacho na fedha zetu ni udhihirisho wa imani ya kweli:*** **Yak 2:14-18** ("nenda zako kwa amani")**; 1 Yohn 3:16-17 [SOMA].** FEDHA NI KIROHO.

C. ***Kile tufanyacho na fedha zetu ni aina ya huduma:*** **Wafil 4:18** (lugha ya dhabihu ya Agano la Kale); **Yak 1:27** ("Dini" = "ni utaratibu wa ki-nje wa kufanya ibada"—ambao huchukua fedha). FEDHA NI KIROHO.

II. Kanisa la kwanza lilielewa hili

A. ***Kanisa la kwanza lilijaa sifa ya UKARIMU USIO WA KAWAIDA—***ambao *kila moja aliweza kuuona.*

B. ***KWA NINI?—Sababu Mbili:***

1. Yesu aliwabadilisha kiukweli NDANI NJE (rahisi kusema "Yesu ni Bwana" au "Nimezaliwa mara ya pili"—bali wao *walithibitisha* kwamba hilo ni kweli).
2. Walielewa *utekelezaji wa Injili:*
   - Ikiwa kristo alitusamehe sisi, je tutakuwaje watu wa kutosamehe?
   - Ikiwa Kristo alitoa kila kitu alichokuwa nacho kwa ajili yetu, tutawezaje kung'ang'ania tu fedha zetu & mali?
   - Ikiwa Kristo hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake, tutawezaje kutofungua milango ya nyumba zetu kwa ajili ya wasio na malazi au watu wengine wahitaji?

C. ***Mifano:***

1. **Luka 19:1-10—***Zakayo;*
2. **Matendo 2; Matendo 4—***Kanisa la Yerusalemu;*
3. **Mdo 11:27-30—***Antiokia.*
4. **2 Wakor 8:1-5—***Makedonia* (miaka 20 baadaye .BK56—Maelezo yaliyokuwako wakati huo: Ukame na njaa Yerusalemu—**1 Wakor 16:1-4)**
   - *KWA NINI Wamakedonia walikuwa wakarimu kiasi hicho? Jawabu:* **Mst. 5**—Maisha yao yalikuwa yamebadilishwa NDANI-NJE; walikuwa na *macho mapya*—mtazamo mpya wa thamani (m.y, kumpenda Mungu; kuwapenda jirani).
   - *2 Wakor 8-9—Ujumbe mrefu zaidi kuliko mingine kuhusu utoaji fedha, lakini hatumii neno "fedha"*—huita: *"neema;" "kazi hii ya neema;" "koinonia"* (Meza ya Bwana); *"leiturgia"* (liturujia); *"ibada; huduma"*—m .y., *maneno yote ya kiroho*—**KWA NINI?** Jibu: kwa sababu FEDHA NI KIROHO.
5. Kanisa hadi kufikia miaka ya 300 **[Soma nukuu kutoka kanisa la kwanza na jinsi walivyotumia fedha zao]:**
   - Walipindua Dola ya Kirumi. Waliishi maisha yaliyokuwa mazuri sana, yaliyo TOFAUTI na watu wengi walivyoishi maisha yao. Watu waliyatamani. Nguvu ya kutokuwa mtumwa wa fedha na vitu. Maisha yao yalikuwa yamebadilishwa ndani-njeCna walidhihirisha hilo kwa maisha yao yenye ukarimu usio wa kawaida.
   - ***JE NDICHO KITU WANACHOKIONA WATU NDANI YETU?*** **Kama siyo, kwa nini?**

III. Matumizi kimatendo

A. ***Siyo kuweka hukumu kwa yeyote:*** **2 Wakor 8:8, 13; 9:7** wote wanena Paulo HAWALAZIMISHI watu kutoaCnasi HATUPASWI kutoa kwa huzuni, au kwa kulazimishwa.

1. **KWA NINI?** Mungu hahitaji fedha zako; kule kutoa tu kwa vile umelazimishwa hakumtukuzi Yeye; naye hawezi kupewa rushwa au kupakwa mafuta kwa mgongo wa chupa kivyovyote.
2. Hivo kama ndivyo ujisikiavyo: USITOE.

B. ***Lakini sote tunajua kuwa tunatakiwa kupima maisha yetu & mwenendo kwa Bwana wetu:***

1. Mtazamo wetu kuhusu fedha, na jinsi tunavyofanya nazo, ndicho *kitu muhimu cha kimatendo cha kujipimia mwenyewe* kilichopo.
2. Ni kitu cha LAZIMA cha kujipima mwenyewe: **KWA NINI?**
   - **Math 6:22-23—**"jicho likiwa giza"—**Kupenda mali** (ile *"shauku isiyo ya kawaida, au ya kuzitegemea fedha na mali."*)**.**
   - **Kuwa na Mali/Uchoyo hutupofusha kutaka mali/uchoyo**—mwangalie tu mtu ambaye ni mfujaji wazi-wazi wa fedha kuliko wewe…m.y., *Wamakedonia walikuwa na "Macho mapya."*
   - "Mkristo" wa wastani hutoa chini ya 3% ya kipato chake—kama kila moja Marekani anayejiita "Mkristo" angetoa angalau 10%, pangelikuwa na zaidi ya **>$150 Billion** zilizopo kwa ajili ya umisheni, kanisa, masikini & wahitaji.
   - Afrika (Waislamu humimina MAMILIONI kwenye nchi za Afrika zilizo chini ya Sahara)—Obama kujaribu kufanya uchumi wa Marekani uwe wa kijamaa—kw a kiwango kikubwa ni kwa sababu kanisa halitendi kama kanisa lilivyokuwa wakati wa ile miaka 300 ya awali ya kuweko kwake.
3. Mungu ni wa neema sana: hutubadilisha ndani-njeChilo peke yake linapaswa kutusababisha tuwe watoaji sana kuwasaidia

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

masikini na kuujenga ufalmeClakini pia hutupatia *KICHOCHEO* KUFANYA HIVYO:

- **Math 6:20** hutuambia *"jiwekee hazina mbinguni."* **1 Tim 6:17-19** panatuambia *jinsi ya* kuweka hazina mbinguni: utoaji wa ukarimu kuwasaidia masikini & wahitaji, na kuujenga ufalme wa Mungu.
- Hili linahitaji: **KUPANGA BAJETI—KUPANGA—KUSEMA—**(KUELEZA) Lakini *huwezi kupata hasara!*

Hitimisho: FEDHA NI KIROHO. Huenda kwenye moyo wa imani yetu, kwa sababu hufunua kile kilichomo ndani ya mioyo yetu. Nini tunafanyia fedha zetu hudhihirisha nini tunafikiria kumhusu Yesu. Hebu tuishi kama kweli tunampenda Yesu.

DIBAJI D

Waef 2:11-16—Muundo wa Fundisho wa Dondoo za Ujumbe

Utangulizi: Sote hupenda kuwa na watu wanaofanana nasi. Sababu ni nyingiCnyingine za kihalali/nyingine hapana. Martin Luther King, Jr.—"Inasikitisha kwamba saa yenye magawanyiko makubwa zaidi katika Amerika ya Kikristo ni saa 5:00 asubuhi Jumapili." (Takwimu za migongano ya rangi za ngozi katika makanisa—90%) Ni kweli pia sehemu nyingine: ukabila (Afrika; India). Matokeo maalum: Rwanda: Mauaji ya kikabila (Wahutu kinyume na Watusi); Kenya: machafuko baada ya uchaguzi (Waluo kinyume na Wakikuyu)—wengi wao walijiita "Wakristo." *Lakini hata kama hakuna machafuko yanayojitokeza,* migawanyiko ya namna hiyo kanisani ni *makosa:*

- "Kanisa tunavyotenda" huonyesha ukubwa wa kile tunachokiamini kiuhalisi.
- Maombi ya mwisho ya Yesu: **Yohn 17:18-2—**umoja *"ili ulimwengu ujue kwamba ndiwe uliyenituma."*
- Swali: lazima tujiulize: "Je hili linakubalika kitheolojia?" (Hasa, katika nchi ambayo ina jamii/makabila mengi).
- Si Kristo, wala Biblia hutambua kuwa jamii za watu, kabila, au historia za kidesturi na mila ndiyo msingi wa kugawanya kanisa.

Kichwa: Waef 2:11-16—MAISHA YETU NI MAPYA KATIKA KRISTO.

- Liweke kwa namna nyingine: kulingana na Biblia, waamini wote- siyo tu *wameunganika* katika Kristo, lakini wamefanywa *mtu mpya* katika Kristo—kwa hiyo, tumeitwa kutendeana sisi kwa sisi kama ambavyo tungetenda kwa Kristo mwenyewe.

Mpangilio wa huja kuu: Leo tutakwenda kuangalia maisha yetu mapya katika Kristo kutoka kona mbili: (1) Ninyi ni nani *hasa* katika Kristo; na (2) Nini lazima *tufanye* kuhusu hilo.

I. Kristo ametufanya "Mtu moja mpya." (**Mst. 11-16**)

A. ***Israeli na Mataifa*** (**Mst. 11-12**): **Mst. 11**—*"ninyi, wa Mataifa":* Mataifa ni akina nani?

1. Kabla ya Kristo = Makundi 2: Israeli (Waisraeli/Wayahudi) na Mataifa. (**Mst. 11**)
   - Rangi ya ngozi/jamii za watu/makabila/ukooCmagawanyiko *yasiyo na umuhimu wowote wa kitheolojia kivyovyote vile,* kwani wote walikuwa Wamataifa.
2. Hali ya kiroho ya Mataifa = walikuwa wamepotea kabisa pasipo tumaini la aina yoyote. (**Mst. 12**)—Hiyo ndiyo hali ya kila mtu asiye na Kristo.
3. Mungu aliwaita Israeli na kuwabariki (**Kumb 7:6-8; Warum 9:4**), kuwa *njia ya* Mungu kujifunulia mwenyewe duniani. (**Kumb 10; 1 Wafal 8; Isa 42**)—lakini Israeli *wakashindwa* kutekeleza jukumu lake.

B. Kristo alichokifanya (**Mst. 13-16**)

1. Aliwaleta Wamataifa kwake mwenyewe—kwa njia ya *damu yake.* (**Mst.13**)
   - Hatukujileta wenyewe kwa sababu hatukuweza.
   - Si damu ya mweusi, mweupe, Mhutu, Mtusi, Mluo, Mkikuyu, nk.—Kwa sababu *damu zote ni nyekundu & na huweza kuingiliana*—ile *damu ya Kristo* ndiyo damu pekee muhimu nayo *hutuunganisha sote.* (**Wagal 3:28; Wakol 3:11**).
2. Aliondoa ukuta kati ya Wayahudi na Mataifa. (**Mst. 14-18**)
3. Zaidi ya hapo: Aliumba jamii mpya kabisa—"mtu mpya." (**Mst.15**)
   - *"Kuumba"*—**Mst. 10 & 15**
   - *"Moja"*—**Mst. 14, 15, 16**
   - *"Mpya"*—**Mst. 15 + 4:24** ("tabia mpya" = "kumfanania Mungu"
4. Aliuondoa uadui: *kiubapa* (**mst.15**) na *kiwima* (**mst.16**)

C. ***Hili linamaanisha nini:*** Kristo ameondoa umuhimu wa rangi zote za ngozi/jamii/kabila/kiuchumi/utofauti wa jamii kati ya watu walio katika Yeye. **[SOMA Wakol 3:10-11]**

1. Je tutawezaje kivyovyote kujigawa wenyewe kwa misingi kama hiyo katika *kanisa* hata kama tofauti hizo zimeondolewa kikamilifu katika *Kristo?*
2. Hii ni dhambi ya kiwango kikubwa kwa sababu inakwenda kwenye *moyo* wa kile alichokifanya Kristo katika **mst. 14-16.**
3. Klyne Snodgrass: "Kudumisha magawanyiko ni kukana kile alichokikamilisha Kristo."

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Sasa tufanye nini?

II. <u>Kwa vile *tu* Mtu Moja Mpya, lazima *tutendeane* kama moja kati kati yetu.</u> (**Mst. 14-16**)

Utendaji unahitaji *kubadilishwa nia.*

A. *Mambo tunayotakiwa kufanya:*

1. <u>Vaeni *"nia ya Kristo"*</u> (**Waef 4:24; 1 Wakor 2:14-16; Warum 12:1-2**)—ona kwa macho ya Kristo.
   - Wafikirie wengine—nasi wenyewe—kama uhalisi wa kweli katika Kristo.
   - Waamini = wana ukaribu zaidi kuliko wana familia ambao sio waamini: Yesu msalabani⊂Mariamu/Yohana (**Yohn 19:25-27**).
   - Kusema "wao sio wa aina yetu" au "Mimi najisikia raha zaidi nikiabudu pamoja na ____" huusaliti mwili wa Kristo⊂kwa sababu wewe kiuhalisi, na nafsi ilivyo, haisimuliwi tena kwa jinsi ya rangi ya ngozi au desturi, bali ni utu mpya katika Kristo.
2. <u>Toka nje</u>: *mifano maalum* = mambo ya kiushirika, kushirikiana madhabahu, miradi ya pamoja, nk.

B. *Mambo tusiyotakiwa kufanya:*

<u>Matatizo ya *rangi ya ngozi/ukabila = utengano*</u> (**Wagal 2:11-14, 18**)—Theolojia ya rangi ya ngozi ("Wakristo wa Kijerumani" katika Ujerumani ya Ki-Nazi; theolojia ya "weusi"/theolojia ya "jinsia" kwa sababu ya kujali maswala ya ukandamizaji); makanisa yaliyoanzishwa katika misingi ya ubaguzi wa rangi/ na mikondo ya Kikabila.

1. Kanisa la Kikristo *"mtu moja mpya"*—ni *wa kipekee.*
2. <u>Kanisa ni *familia*</u> (**Warum 8:15-16; 1 Tim 3:15; 5:1-2**)—Kama vile *familia kubwa iliyopanuka*—familia husaidiana & kupendana licha ya (au kwa sababu ya) tofauti zao (**Ufu 5:9**).
3. <u>Kuifanyiza theolojia ya kudhalilisha au kuwa na mpangilio wowote wa kanisa kwa rangi ya ngozi/mbari za watu/ maswala ya ukabila</u>—hata ykjihalalishwa kiasi gani⊂ni *makosa makubwa* kwa sababu kufanya hivyo huiinua hali ya awali ambayo, katika Kristo, tayari *ilishakwisha.*
4. <u>Pia ni makosa makubwa kwa sababu huinua kitu ambacho ni *kidogo kuliko Kristo mwenyewe* kuwa ndiyo *mkazo* au mahali pa *umuhimu wa kwanza* katika kanisa</u>—hilo litakuwaje sahihi?
5. <u>Utengano *hujenga upya kuta za magawanyo* ambayo Kristo aliyavunja</u>—sasa umejengwa upya *kati ya makundi mbali mbali ya Mataifa* (ambapo katika Agano la Kale *halikuwawekea utofauti* hata kidogo).

C. *Desturi ni nini?*

1. **Mdo 2:5-11—**Uw ingi, uwingi wa desturi mbali mbali za watu ndio waliounda kanisa la awali.
   - Hata hivyo, **Mdo 2:44—"***Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote ushirika."*
2. <u>Tatizo *Udesturi = Upendeleo*</u> (**Mdo 6:1**), inafanana na dhambi ya *magawanyo:* kimsingi, tatizo la kidesturi, siyo la mbari za watu, (wote Wayahudi, bali wengine "Wayahudi wa asili ya Kiyunani" walibeba desturi nyingi za Kiyunani kuliko wengine).
   - <u>Kanisa lilishughulika nalo</u>—**Mdo 6:3, 5, 7**—na watu walikaa pamoja.

   "Maamuzi ya kidesturi yanapaswa kuachwa nyuma; ya umoja katika kristo. Jambo la muhimu zaidi siku zote ni *kujitambua.* Ni nini uhalisi wa nguvu kuliko zote kwetu⊂Kristo desturi yetu? Desturi ni muhimu⊂naam, sehemu ya lazima ya muundo wa maisha yetu⊂lakini Kristo, siyo desturi, hutupatia tafsiri ya msingi ya maisha." (Klyne Snodgrass, *NIV Application Commentary, Ephesians*)
3. <u>Desturi isielezee wa kumwekea mipaka Kristo</u>—lak ini utii kwa Kristo na mtazamo wake wa watu (yule "Mtu Moja Mpya") kunaweza *kubadilisha desturi.*
   - *Isiyofaa*—Kanisa lililo la msingi wa Taifa/desturi/rangi ya ngozi - je hilo halisemi *kwangu,* kwamba nani si mshirika wa "hilo" kundi: "Wewe si moja wetu"; "Hukaribishwi hapa."
   - *Inayofaa*—Kwa kuwa pamoja katika kanisa, kama tulivyo kikweli mtu moja mpya, tunathibitisha kweli ya Maandiko, kipaumbele cha Kristo, na kuonyesha kwamba Kristo NDIYE jibu la migongano na mivutano ya kijamii, mbari za watu, kikabila, na za kimila au kidesturi.

D. *Umuhimu mkubu wa hili:* *"Barua kutoka Meka"* ya Malcolm X **[SOMA].**

Swala ni la muhimu zaidi leo kwetu kuliko lilivyoandikwa zaidi ya miaka >40 iliyopita.

1. Uislamu uliozagaa na mkali.
2. Kwa kiwango fulani Uislamu unaonekana kama ni njia ya kuondoa utofauti wa ubaguzi wa rangi/mbari/desturi kati ya watu⊂na kanisa na Ukristo siyo—ni *aibu kubwa kwa kanisa..*

<u>Hitimisho:</u>

- Katika yote tuyafanyayo kuhusiana na kanisa, ni lazima tujiulize: "Je naweza kustahilisha hili kitheolojia?"—kwa sababu "tutendavyo kama kanisa" hudhihirisha jinsi *tunavyojitafsiri wenyewe*, na *kipi ni muhimu zaidi kwetu.*
- **Waef 2** panatueleza uhalisi wa kweli ni upi—lazima tu*fikirie upya* tunafanya nini na *kutenda* ili kufanya utendaji wetu uendane na uhalisi wa kweli.
- Kristo aliuvunja ukuta uliowatenganisha Wayahudi na Mataifa na kumfanya *"mtu moja mpya" mahali pake*; kwa hiyo Yeye alikomesha umuhimu wa rangi ya ngozi, mbari za watu, na utofauti wa kidesturi ndani yake mwenyewe na katika kanisa⊂hatupaswi kujenga ukuta ule unaotenganisha; na tofauti hizo kati kati yetu.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Alichokiunganisha Kristo, mwanadamu yoyote asikitenganishe!

DIBAJI E

Kut 1:1-22—Muundo Elekezi wa Dondoo za Ujumbe wa MKM[7]

Utangulizi: *Je mambo yamewahi kukubadilikia kutoka uzuri na kuwa mbaya zaidi maishani mwako?*

MIMI—Ugonjwa + binti aliyekasirishwa [au mifano mingine]

SISI—Mambo yanaweza kutokea maishani mwako, au katika maisha ya watu walio karibu nawe, maisha ya watu katika kanisa utakalolihudumia, ambao hukutegemea nao wakuumiza:

- Ayubu: anaendelea vizuri; akipanda juuCmkuu mpya—ghafla kabisa hawezi kufanya kitu sawa sawa.
- Daktari anasema "kaa chini"—Nancy F.: miaka 40—kansa—alionekana kama miaka 80 alipokufa.
- Rafiki wa kiume/rafiki wa kike anakutupilia mbali.
- Wakristo huko Nigeria—sheria ya Sharia—dhiki—makanisa yanachomwa moto—mauaji.

Katika mazingira kama hayo tunapaza sauti "si sawa—si haki"—na hatuwezi kumwona Mungu katika dhiki yetu.

Mpangilio wa hoja kuu: Kisa cha yale yaliyotokea kwa watu walioishi Misri ya kale zaidi ya miaka >3000 iliyopita katika **Kutoka 1** huzungumzia tatizo hili hasa. Kwa hiyo, hebu tukiangalie kifungu hiki kwa njia 3: (1) Kuona kile kilichotokea. (2) kuangalia kweli muhimu mbili zilizomo katika kisa hiki; na (3) kuona jinsi yanavyotenda kazi kwetu tunapopitia ugumu.

I. Ufafanuzi:

A. ***Kut 1:1-7***—Huunganisha na kile kilichotokea katika Mwanzo. Sote tunajua kisa kile. Yusufu aliuzwa utumwani na ndugu zake—akainuliwa kuwa juu kinafasi #2 katika Misri na kuwaokoa Wamisri na ukame—**Mwanzo 46** Baba wa Yusufu na familia yake yote wanahamia Misri na kukaa huko.

1. **Mwanzo 47:6—[SOMA]—**Hapo ndipo **Kutoka 1** inaanzia.
2. *Mungu akawa anawabariki—wakawa wanaongezeka—maisha yakawa mazuri.* LAKINI: *Kitu fulani kikatokea.*

B. ***Kut 1:8***—**[SOMA]—**Huenda ni utawala mpya. Mabadiliko yanaweza kuja maishani mwetu kwa kitambo. Hatukitarajii—hatukukipangia—lakini hata hivyo kinatokea:

1. Unampata mkuu mpya—Mpenzi wako wa kiume au mume wako anampata rafiki mwingine wa kike.
2. Kanisa lako linagawanyika—unafukuzwa.
3. Madaktari wanasema "kaa chini."

Matokeo yake yanaweza kufadhaisha sana.

C. ***Kut 1:9-11*****—[SOMA]**

Mst.10—*"kwa busara"* = kwa ustadi, kwa werevu, kwa makini.

1. Waebrania hawakuwa wanashitakiwa kwa kufanya kitu kimakosa—zaidi ya *kule kuwako.*
   - Hawakushitakiwa kwa kuwaingilia Wamisri.
   - Hawakushitakiwa kwa kujitwalia ardhi iliyo bora zaidi katika nchi.
2. Madai ya Farao yalikuwa *ya kifikira tu:*
   - Waebrania walikuwa watii na wenye thamani siku za nyuma.
   - Wangeweza kuwa *rasilimali* ya thamani nyakati za vita.
3. Upinzani wa Farao hatimaye ukawa *hauna maana yoyote.*
   - Hakuwapenda kabisaChakutaka kuongezeka kwao—hata hivyo tatizo lake hakutaka *waondoke* Misri.

Mst.11—*"kazi"* = mizigo, kazi ya lazima.

Lakini mambo yakahama kutoka ubaya kuwa mbaya zaidi.

D. ***Kut 1:12-14*****—[SOMA]—**Mistari hii inatuambia mambo 2 mapya ambayo Wamisri waliyafanya:

1. **Mst.12**—Mtazamo wa Wamisri kwa Waebrania ulibadilika:
   "Kuogopa" = pia "kujisikia vibaya, mafadhaiko, kutopenda"—kuogopa na kutopenda siku zote huenda pamoja kuhusu watu ambao mtu anawachukia—na hilo lilitokea hapa.
   - Mtazamo huo ulikuwa mpya, na ulizaa ngazi mpya ya kazi ya ukandamizaji.
2. **Mst.13-14**—kazi "*kwa bidii kabisa"* = "kwa ukali, kiutumwa." Hii haikuwa tena kazi ya hiari—ilibdilishwa kuwa ya utumwa mkali maeneo yote ya maisha.

Lakini Farao alikuwa na mpango wa uovu zaidi kuwashughulikia WaebraniaCna mpango huu mpya unaonekana katika ngazi 2:

[7] Tambua kwamba ijapokuwa ujumbe huu msingi wake ni muundo wa MKM, utangulizi wake umefuata mfumo wa Mimi – Sisi.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

E. ***Kut 1:15-22*****—[SOMA]**

1. **Mst.15-16**—Farao alianzia kuongea na wazalishaji—hili linaonyesha kutaka kuwaua watoto wote wa kiume wa Kiebrania *kwa siri.* Mnenaji moja analinena jambo hilo kwa jinsi hii: "Kwa vile yeye [mfalme] aliona kwamba hakuna njia ya kuwadhoofisha Waisraeli kwa njia zisizo za moja kwa moja, aliamua kukomesha nguvu zao kwa njia ya kuwatendea moja kwa moja. Lakini hakufanya hata hivyo, uamuzi wa kutoa amri hiyo ifanyike hadharani, akawa ameamua kufanya swala hilo kwa siri. Aliwaagiza wazalishaji kuwaua watoto wa kiume wa Ki-Israeli. Walikuwa wawaue, bila shaka, kwa siri, kwa namna ambayo wazazi wao na majirani wasingalijua uhalifu huo, na wangedhani kwamba wamekufa kutokana na sababu za kawaida; ama kabla, au wakati wa kuzaliwa." (Umberto Cassuto, *Maelezo kuhusiana na Kitabu cha Kutoka,* kilichotafsiriwa na Israel Abrahams [Jerusalem: Magnes, 1967; Central Press, 1974], 12)
2. *LAKINI:* **Mst.17-19**—Wale wazalishaji waliposhindwa kufanya hivyo, na walipoitwa mbele ya mfalme walijitetea wenyewe kwa kusema *"Hatuna hatia—wale wanawake Waebrania nsi kama wanawake Wamisri—wana ujasiri sana kiasi kwamba wanazaa wenyewe hata kabla hatujawafikia."*
    - Wanachokionyesha ni, *"Ewe Mtukufu, mara mtoto akishazaliwa, na baba yake, mama yake na majirani zake wakishamwona haiwezekani tena kumuua kwa siri."*
3. *KWA HIYO:* **Mst. 22**—Farao akaamua kuzimisha hila hizo mbovu:
    - Haendelei tena *"kusema"* kama katika **mst.15**—sasa *anaagiza.*
    - Sasa haendelei kutoa maagizo kwa wazalishaji peke yao—bali sasa anaagiza kwa *taifa.*
    - Sasa mpango wake si wa siri au wa faragha tena⊂sasa ni *hadharani.*
    - Sasa uuaji hautakuwa nyuma ya pazia au kufichika tena—bali sasa unatakiwa uwe moja kwa moja, mauaji ya jumla ya watoto wa Kiebrania: wazi wazi, kwa kuonekana, na pasipo kubakiza.

Na hapo ndipo kisa kinaishia—Kitabu cha Kiebrania huonyesha pana kituo kati ya **mst.** wa **22** na **Kut 2:1** kuonyesha kisa kinaisha. **AU JE NI KWELI KINAISHA?—**Hebu tuangalie nyuma ya pazia tuone—na tunaona nini?

II. Kanuni

Kumbuka "zile kweli 2" nilizozitaja hapo awali: Hapa twaona ile ***kweli muhimu ya 1*** *lazim a tujue wakati mambo yanabadilika kutoka ubaya kuwa mbaya zaidi:*

A. ***Wakati mambo yanapobadilika kutoka ubaya kuwa mbaya zaidi, Mungu anaweza kuwa haonekani⊂lakini bado yupo kazini.***

Inawezakana tusiisikie sauti yake, lakini kama Francis Schaeffer anavyosema, *"Yupo hapo naye hayuko kimya."*

- Mambo maovu ambayo yanatokea yanaweza kuonekana yanajitokeza ovyo ovyo na bila mpangilio wetu⊂lakini *kiuweli, ni sehemu ya mpango fulani mkubwa uliounganika, au muundo ambao, Mungu anausimamia na kuuratibu.*
- Kiukweli, Mungu mara nyingi huutumia ubaya kwa jinsi ambayo *inatatanisha* kabisa⊂kwa jinsi ambayo sisi huwa tunaona *ni kinyume kabisa* ya vile tunavyotegemea⊂ambayo huweza kuwa sababu moja, kwa nini ni vigumu sana kwetu kuona kile anachokifanya.

Hebu tuone kweli hiyo inavyodhihirika katika dhana ya andishi letu.

1. Kile kilichotokea kilikuwa kimeandaliwa na kupangwa na Mungu.
    - **Mst. 7**—Unaonyesha kwamba Mungu hakuzisahau ahadi zake katika kitabu cha Mwanzo kwa Ibrahim, Isaka, na Yakobo kuwafanya Israeli taifa kubwa, na kuwazidisha kama nyota za mbinguni; na kama mchanga wa baharini—Naam, Mungu alikuwa anazitimiza ahadi hizo hizo, hata kama Israeli walikuwa katika nchi ya kigeni.
    - **Mst.9**—Israeli wanaitwa *"watu" kwa mara* ya kwanza—wamehama kutoka familia kuwa watu—wanaweza wasiwe wameutambua ukweli—lakini Mungu—pia na Farao.
    - Hata *mabadiliko ya mazingira* hayakutokea ovyo ovyo, lakini ulikuwa ni mpango mzima ambao Mungu alimwambia Ibrahimu, karibu miaka 100 iliyotangulia—**Mwa 15:13**—**[SOMA]**
    - Kitabu cha Mwanzo kilikuwa bado hakijaandikwa—hivyo watu hawakujua—hawakuweza kuona—bali Mungu aliweza, na alikuwa mwaminifu kwa mpango wake.
2. Ushahidi wa mpango katika dhana ya andishi.
    - Uhusiano kati ya kuongezeka kwa Waebrania na uovu uliowakumba—X 3, Waisraeli wanasemekana kuongezeka—kila moja linafuatiwa na ongezeko la mvutano na kuongezeka kwa matendo kadhaa mabaya ya ukandamizaji:
    - **Mst.7 =** kazi ya lazima **mst.11**.
    - **Mst.12 =** utumwa wa kikatili **mst.13-14**, na mpango wa kuwatumia wazalishaji kuwaua watoto wachanga kwa siri katika **mst.16**.
    - **Mst.20 =** Agizo kwa watu wote la wazi kuwatupa watoto wa kiume wa Kiebrania katika mto Nile **mst.22**.
3. Mpangilio wa maneno unaonyesha mpangilio wa mambo haukuwa wa ovyo-ovyo:
    - Hebu tufanye kwamba makandamizo kwa Waebrania yalitokana na kuongezeka kwao, Mungu alikuwa amepanga kinyume chake kabisa. Katika **mst.10** mfalme wa Misri asema kwamba iliwabidi wawatendee kwa akili Waebrania ***"wasije wakaongezeka"—***katika **mst.12,** ingawa umetafsiriwa katika hali ya wakati uliopita kwenye Biblia (***"nao wakaongezeka"***), kwa Kiebrania hasa ni hali ya utimilifu wa baadaye kama ilivyo katika **mst.10**, siyo katika hali ya wakati uliopita—*"kadiri watakavyo****watesa,*** *ndivyo kadiri* ***watakavyoongezeka."***

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Mfalme wa ulimwengu alikuwa anatawala juu ya mfalme wa Misri.

B. ***Mbinu ya utendaji wa Mungu***

Tunajua mwisho wa kisa hicho—Kutoka—lakini, hili halikutokea hadi angalau *miaka 80 baadaye.* Katika sura ya **12** (*Musa bado hajazaliwa katika ile sura ya* ya 1)—laki ni kujua nini kinakuja mbele, hutusaidia kuona *mbinu* za utendaji wa Mungu.

1. **Mst.10**—Hofu kuu ya Farao ilikuwa Waisraeli wangeondoka waache Misri⊂hata hivyo, hilo ndilo lililotokea.
2. **Mst.11**—Waebrania walilazimika kujenga miji ya kuhifadhia vitu kwa ajili ya Wamisri⊂hata hivyo safari ilipowadia, Waebrania waliondoka na mali za Wamisri (**Kut 12:35-36**).
3. **Mst.22**—Agizo la mwisho la kuwatupa watoto wa Kiebrania wa kiume katika mto Nile:
   - *Kwa sababu ya amri hiyo hiyo,* mama yake Musa alimweka Musa katika mto Nile.
   - Kuongeza mbinu hiyo zaidi, Musa aliokolewa na mauti *na binti Farao mwenyewe.*
   - Kwa hiyo, *ile amri au agizo lenyewe lilitumiwa na Mungu kama chombo cha mwisho cha ukombozi wa Israeli.*
   - Tena, katika mbinu nyingine ya kipekee, ingawaje watoto wa kiume wa Ki-ebrania walikuwa wamepangiwa kifo kwa kutupwa majini, wakati wa kuondoka ulipowadia, *ni jeshi la Wamisri ndilo lililozama majini.*
4. Watu hawakuweza kuona kwa wakati huo, lakini Mungu alikuwa anatumia kila tukio katika mkasa mzima⊂mara nyingi katika namna zilizo za tofauti kabisa⊂kutekeleza makusudi na mipango yake mizuri.
   - Tunaweza tusione katika maisha yetu wenyewe chochote kizuri, isipokuwa mazingira magumu na maovu—lakini Bwana ni yeye yule, jana, leo na hata milele (**Waeb 13:8**).

Hili linatupeleka kwenye ***kweli muhimu ya 2*** *ambayo inatenda kazi kwetu nyakati za vipindi vibaya, visivyotulizana⊂nalo ni* ***jinsi*** *Mungu anavyofanya kazi—yaani:*

C. ***Mungu hufanya kazi yake kupitia watu wake.***

- Mungu hufanya kazi kupitia matendo ya uaminifu ya walio wake.
- Hutenda kazi kupitia walioamua kuweka utii kwake, kul; iko kujali raha zao na mafanikio yao wenyewe.
- Ni kweli, hutenda kazi kupitia wanaokuwa waaminifu kwake, wakipuuza hatari halisi ambazo zingewakabili.
- *Katika Kutoka 1 wale mashujaa wa kile kisa cha* **WAZALISHAJI.** Mungu alikuwa mwaminifu kwa ahadi zake kwa Israeli—ingawaje wanaweza wasiwe wameelewa hilo—na kwamba muundo wa dhana ya andishi unaonyesha hilo. Mungu alitenda kwa mpango na kufanya kwa mbinu iliyojificha—na Mungu alifanya jinsi hiyo hiyo kwa kupitia wazalishaji.

1. Dhana ya andishi inaonyesha kwamba wale wazalishaji walikuwa ni sehemu muhimu ya mpango wa Mungu.
   - Katika **mst.15-21**—neno la muhimu ni "*mzalishaji.*"
   - Katika uwingi wake, neno *"mzalishaji",* linajitokeza X7**.** Mungu *anasisitiza* umuhimu wa *watu* wake kwa jinsi wanavyotekeleza *mpango* wake.
   - Watu wanaomcha Mungu ni sehemu muhimu katika mpango na kazi yake.
2. Angalia pia mbinu ya wazalishaji.
   - Katika **mst.10** mwanzo wa mpango wake wa ukandamizaji, Farao alisema kwamba ilibidi watende *"kwa akili"* au *"kwa ujanja"* kwa Waebrania—hata hivyo *walikuwa ni wazalishaji hao hao ndio walioonyesha hekima kubwa kuliko zote na ujanja mkubwa katika kushughulika na Farao* katika **mst.18-19** walipoitwa wakatoe maelezo kwa kazi zao.
   - Walidhihirisha kile ambacho Yesu alikisema baadaye—katika **Math 10:16**—tunatakiwa tuwe: *"na busara kama nyoka na kuwa wapole kama hua."*
3. Ona *matokeo ya ile mbinu iliyojificha*—siyo tu Mungu aliwabariki (**mst. 21**), lakini—kwa nguvu zake zote za kidunia, nafasi, na fahari yake—huyo Farao anabakia *kutotajwa jina lake.* Hata hivyo wale wazalishaji wanabaki kukumbukwa kwa karne nyingi *kwa majina*—Shifra na Pua—na wataendelea kujulikana kwa majina milele yote.
   - Mungu anakujua wewe kwa jina—*je ni jina la aina gani unataka liwe mbele ya macho ya Mungu?*
   - Kumbuka—watu wanaojulikana sana siyo wenye nguvu na walio mashuhuri—lakini wale wanaoteseka na kufanya mapenzi ya Mungu ya upendo na kumcha yeye.

Kichwa: Kwa hiyo hili linatuambia nini? Linatuambia: *Twaweza tusione; inawezekana ikawa vigumu kuelewa; lakini kila kitu kinachotokea kwetu—kuchanganya na yale mabaya—yote ni sehemu ya mpango wa Mungu.*

III. Matumizi kimatendo: *Kwa hiyo hili linatuhusu nini maishani mwetu?*

A. ***Wale wazalishaji walikuwa si watu wajulikanao—Farao alikuwa na nguvu kubwa sana—alikuwa anawaita waje watoe maelezo kwa kutokutii agizo lake—na angeweza akawafyeka mara moja [KIPIGO].***

1. Waliacha kumtii kiongozi wa taifa kwa kuhatarisha maisha yao wenyewe, kwa vile walikuwa na vipaumbele vyao sawa sawa—walimjua yeye ambaye hatimaye watawajibika kutoa hesabu kwake—kwa hiyo, kama vile mjane aliyetoa zile senti zake 2 (**Luka 21:1-4**), wale wazalishaji walijitolea kila kitu walichokuwa nacho.
2. Walikuwa *hawana woga wowote* kwa sababu *kimaadili walikuwa wanamcha Mungu.*
3. Wakati tunakabiliwa na jambo la *kanuni*, je tunakubaliana na kile tunachojua kuwa ni haki—na kile tunachojua Mungu anakitaka—kwa sababu tunaogopa kupoteza kitu kidogo zaidi ya kile ambacho wazalishaji wale wangekipoteza—kitu kama fedha zetu—nafasi zetu—au urafiki wetu?

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

B. ***Sote tunakabiliwa na uchaguzi wa jinsi hii itokeapo uaminifu kwa Kristo na kwa Neno lake kunahusika:***

1. Ukiiona pochi imejaa fedha ndani yake, lakini pia unaliona jina na anuani ya mtu aliyeiangusha. Je utamrudishia au hapana?
2. Unanunua kitu dukani na yule mhudumu anakurudishia chenji iliyozidi kabisa. Je utabaki nayo?
3. Wewe ni msichana bado mdogo; nawe una mpenzi wako wa kiume; anataka mfanye mapenzi. Je utafanya nini?
4. Kule kazini kwako, mkuu wako anakuambia ufanye kitu ambacho unajua ni cha makosa. Kama hutakifanya, unaweza kuipoteza kazi yako. Je utafanya nini?

C. ***Mungu huona mambo haya madogo madogo—lakini kiukweli si mambo "madogo" hata kidogo.*** Haya ni mambo yanayodhihirisha sisi ni akina nani hasa—huonyesha tabia zetu, na huonyesha kama kweli imani yetu ni halisi au hapana.

Hitimisho: Hatujui ni muda mrefu kiasi gani kipindi cha utumwa wa kikatili katika Kutoka ulichukua—lakini ni dhahiri kilidumu muda mrefu—wa kutosha kiasi kwamba vizazi vingi vilizaliwa na kufa pasipo kuona jawabu—wala kufanikiwa kumsikia Musa—pasipo hata kujua ahadi au mpango wa Mungu.

- Kitu kama hicho kinaweza kuwa cha kweli katika maisha yetu kwa wale tuwajuao. *Uko mahali pa ugumuChuijui sababu, na huwezi kuona mwisho wake.*

1. Ndiyo maana tunalihitaji kanisa—ndiyo maana tunahitajiana!

Wakumbuke wazalishaji wale—Hawakuwa peke yao. Shifora na Pua, walikuwa katika hilo pamoja.

- Hawakuweza kuona mambo yatakuwaje—bali walimcha Mungu, na kufanya kiusahihi hata kuhatarisha maisha yao wenyewe.
- Na waliweza kutiana nguvu—na kuinuana kila mojaCna kutegemeana kila mojaCna kulia pamoja.

2. Nini kingekuwa kama *sisi* nasi tungefanya hivyo? Tunajua watu wanaoteseka wanaweza kuwa ni mtu fulani aliyepoteza kazi yake—au ana mtoto anayeumwa sana Malaria—au anahitaji fedha kwa ajili ya ada ya shule:

- Kama tungefanya mlo kwa ajili ya mtu mgonjwa au aliye mhitajiCau hata kulipa sehemu ya ada yao ya shule—je hilo lingekuwa na matokeo gani katika maisha yao?
- Mfikirie yeyote unayemjua: Kama tungefanya tu *tendo moja la kutia nguvu juma hili,* tunaweza kuanza kitu, na nani ajuanye kitakakoishia?
- Kila moja anaweza kufanya tendo la kutia moyo katika juma.
- Hilo ndilo kanisa lililo kanisa—huko ndiko kutenda kama Kristo mwenyewe.

3. Hebu tujaribu kuwa kama wale wazalishaji. Kumbuka: Mungu sasa anawaita kwa majina—tusimamapo mbele zake kutoa hesabu za maisha yetu, kama tumekuwa waaminifu, atatuita kwa majina yetu, pia.

DIBAJI F

Ufu 19:11-21—Muundo Elekezi wa Dondoo za Ujumbe wa MKM

Utangulizi: *Mfano binafsi:* Shitaka la kesi—kungojea hukumu—je nimefanya vizuri?—"Wazee wa baraza wamefikisha maamuzi yao"—hakuna tena kitu unachoweza kukifanya—kisha utoaji hukumu unafuatwa. *Mifano mingine:* uchaguzi; pendekezo la ndoa; mtihani wa wanafunzi, nk.

Ufu 19:11-21 panatuambia kuhusu uamuzi na hukumu, yenye matokeo yaliyo juu zaidi ya ngazi zote za ki-sheria, uchaguzi, ndoa, mtihani, ni uamuzi wa Yesu juu ya dunia & hukumu yake itakayoipata.

Mpangilio wa hoja kuu: Leo tutakwenda kuangalia kifungu hiki kwa namna 3: kwanza, kuangalia undani na alama zake; pili, kuangalia kanuni zinazofundishwa; tatu, kusisitiza matumizi kimatendo kwa ajili ya maisha yetu.

I. Kueleza upya Kifungu:

A. ***Dhana ya ufunuo:***

1. Aina: Waraka, unabii; Tukio la kimaafa = lenye kueleweka na wasikilizaji.
2. Dhana ya kihistoria: Himaya ya Kirumi (BK 90-95). Kama Uganda (Kenya, nk.):
   Mpangilio—Herufi kubwa; hasa barabara za vijjiini/kilimo.
   Lugha—Lugha moja kuu (Kiyunani = Kingereza/Kiswahili, nk.) + lugha nyingine.
   Jamii—Makabila mbali mbali; madhehebu mbali mbali (dhiki mbali mbali).
3. Makusudio: Kutia moyo + maonyo.

B. ***19:11-21 Maelezo yoyote ya alama kuu:***

1. **Mst. 11—***Farasi mweupe* = shujaa atekaye nyaraCkama yule Jemedari wa Kirumi atembeaye Roma.
2. **Mst. 12—***Macho yake kama mwali wa moto = aona yote*; moto-hukumu (**Ufu 1:14; 2:18, 23**).
3. **Mst. 12—***Vilemba vingi* = mataji/ enzi ya kitawala; "mengi" = zaidi ya mfalme yeyote wa kidunia (**mst. 16**).
4. **Mst. 13—***Anaitwa Neo La Mungu* = Yesu (**Yohn 1:1**).
5. **Mst. 14—***Majeshi yaliyovaa kitani safi nyeupe, & iliyo safi = Wakristo/Kanisa* (**Ufu 19:7-8**).
6. **Mst. 15—***Upanga mkali* = Neno La Mungu (**Ufu 1:16; Waeb 4:12**)—Kama vile alivyoumba hapo mwanzo wa historia kwa Neno, ndivyo atakavyohukumu na kuiharibu, ni kwa Neno.
7. **Mst. 15—***Fimbo ya chuma* = Yesu ana mamlaka kamili & nguvu; maadui wote wataangamizwa kabisa. (**Ufu2:27;**

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Zab 2:9).

8. **Mst. 17—***Karamu kuu ya Mungu* = inaendana na **Ufu 19:9** (karamu ya arusi ya Mwana Kondoo)—ni kuendana na *wokovu* ni *hukumu.*

II. <u>Kanuni</u>

A. *Kutakuwako siku ya hukumu ya mwisho; itaathiri dunia nzima na kila mtu ndani yake.* (**mst. 11-21**)

B. *Yesu anakuja tena katika dunia hii; hatakuja kama "mpole na mnyenyekevu," bali kama "Mfalme wa Wafalme, na Bwana wa Mabwana" ili "kuhukumu na kufanya vita."* (**mst. 11-12, 16**)

C. *Hukumu yake itakuwa sahihi kabisa, ya uaminifu, ya kweli, na ya haki.* (**mst.11**)

1. Itakuwa inakagua yote, yenye ukamilifu na ishughulikiayo mzizi wa matatizo. (**mst.12**)
2. Itakuwa ni ya mwisho. (**mst.11, 20-21**)
3. Kipimo cha hukumu ni Neno la Mungu. (**mst.13, 15**)

D. *Kwa wale ambao sio wake, itakuwa ya kutisha na vigumu kuamini.* (**mst.13, 15, 17-21**)

1. Siyo tu anahukumu, bali anafanya vita pia. (**mst.11**)
2. Uharibifu ndio mwisho wao na unatisha—hakutakuwa na nafasi "nyingine ya 2" (**mst.15, 17-21**)

E. *Kwa wale walio wake, itakuwa ni ya ushindi mkuu.* (**mst.14**)

Imani, tumaini, na hali ya kujitoa kwake, kutalipiwa kikamilifu. (**mst.11, 14**)

<u>Kichwa:</u> Jitoe kwa Yesu sasa, ili usiangukie kwenye hukumu yake baadaye.

III. <u>Matumizi kimatendo</u>

A. *Ikiwa Yesu si Bwana wa maisha yako, tubu na umgeukie.*

1. <u>Kama unaendelea vizuri:</u> Unajua nini kiko ndani yako; huwezi kujibadilisha mwenyewe kutoka ndani-nje.
2. <u>Kama wewe ni masikini na huendelei vizuri:</u> Mungu wa ulimwengu huu anakujua kuwa una thamani kubwa—kwa sababu alikuja moyoni akiwa ndani ya mtu aitwaye Yesu, akaishi kama masikini, na alikufa kwa ajili yako ili kukupa uzima mpya.
3. <u>Ieleze Injili & matendo yanavyotofautiana na neema:</u> Dini ya mwanadamu = nini tunafanya kwa ajili yetu wenyewe; Injili = nini Kristo amefanya kwa ajili yetu.
   - Ufufuo unadhihirisha Yeye ni *nani* na kwamba yu hai leo.
   - Alisema kwamba atarudi tena duniani. (**Math 24; Marko 13**).
   - Kifungu hiki kinatueleza nini kitatokea hapo atakaporudi.

B. *Ikiwa Yesu ni Bwana wa maisha yako, dumu kwa uaminifu kwake.*

Je tu waaminifu kiasi gani?—UPENDO: **Math 22:36-40; Yohn 13:34-35; 1 Wakor 13; 1 Tim 1:5.**

1. <u>Mifano maalum:</u>
   - "*Kikombe cha maji baridi"* (**Math 10:42**)
   - "*Ukarimu & na tayari kutoa"* (**1 Tim 6:18**)
   - Kuwasaidia masikini & wahitaji na kuujenga Ufalme wa Mungu (**Mdo 4:32-35; 2 Wakor 8:1-5; Wagal 6:10; Yak 1:27**).
   - Matendo kama hayo ya upendo = hushona pamoja *"mavazi yetu meupe"* (**Ufu 19:8**).
2. <u>Kumbuka:</u>
   - Matatizo yetu si kitu kulinganisha na kile kitakachotokea kwa wale wasio wake.
   - Matatizo yetu si kitu kulinganisha na uzuri mkuu utakaowekwa kwetu.
   - Macho yake ni mwali wa moto—kufanya kile ambacho Neno la Mungu linaagiza, katika kila sehemu ya maisha yako, ili kwamba kurudi kwake kuwe ni wakati wa ushindi mkuu kwako—hili linatakiwa *liwatie moyo* wale wanaoishi kwa uaminifu.

<u>Hitimisho:</u> Neno "hukumu" hutokana na maneno 2 ya Kilatini yanayomaanisha "kusema iliyo kweli." Yesu atafanya yote mawili-kusema kweli, na kutoa hukumu kulingana na ile kweli. Hakikisha uko tayari.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

DIBAJI G

Zab 73:1-28—Dondoo za Ujumbe wa Muundo Simulizi wa kisa

Utangulizi:

Je sisi sote huwa hatuhangaiki na tatizo la kukabiliwa na mateso mara kwa mara? Tunapungukiwa fedha; wakati watu wasiomcha Mungu wanafanikiwa kimaisha.Tunapatwa na maradhi makubwa; wakati huo huo tunawakuta wengine wako na afya njema kabisa. Tumejitahidi kufanya kitu sahihi, lakini hatuonekani kupata yale tuliyokuwa tunayatarajia au kuyaotea ndoto; wakati huo huo tunawaona wengine ambao kwa dhahiri kabisa wanapuuzia maagizo yanayotolewa na Biblia kuhusiana na jinsi tunavyotakiwa kuishi, nao wanaonekana kuwa na furaha na kufanikiwa. Katika nyakati kama hizo tunajisikia sana kama Ayubu, na kuuliza maswali yale yale ambayo aliyauliza:

- "Uko wapi Mungu?" na
- "Ni Mungu wa aina gani huyu anayeruhusu uovu na wasio haki kufanikiwa, lakini walio wasafi na wacha MunguC walio wake mwenyeweCkuteseka?" na
- "Je hakuna haki?"

Mpangilio wa hoja kuu: Leo tutakwenda kutembea katika viatu vya mtu aitwaye Asafu aliyekabiliwa na dhuluma kubwa na aliandika **Zaburi 73** ili kutuelezea. Hebu tupitie hatua nne za Zaburi hii—muktadha wake, mgogoro aliokabiliwa nao Asafu, ufumbuzi wa mgogoro ule, madhara na utendaji wake katika maisha yetu leo—kuona uelewa anaotupatia Mungu wakati waovu wanpoafanikiwa.

I. Dhana

A. ***Moja ya Zaburi muhimu sana***

1. Huanzisha Kitabu cha III katika Zaburi—ni kati kati.
2. Hushughulikia matatizo muhimu ambayo sisi sote huwa tunakabiliwa nayo.

B. ***Huyu Asafu ni nani?***

1. Ni Mlawi: Kiongozi wa zile nyimbo takatifu, aliyechaguliwa na Daudi kuhudumia mbele ya sanduku la Agano katika hema ya kukutania (**1 Nyakati 6:31-32, 39; 16:1-5**)
2. Mwonaji/ Nabii (**1 Nyakati 25:2; 2 Nyakati 29:30**)

Zaburi 12 zilitungwa na Asafu—nyingi zaidi kuliko za wengine, isipokuwa tu zilizotungwa na Daudi.

- Alikuwa kwenye moyo wa mfumo wa kuabudu wa Wa-Israeli.
- Alijua kile anachokizungumzia.

II. Upeo (mst. 1-14)

Mst.1—*"Hakika Mungu ni mwema kwa Israeli, kwa wale walio safi mioyo yao."* Lakini je, hilo ni kweli? Je aliona nini?

A. ***Kile alichokiona Asafu (mst. 2-14)***

1. **Mst. 2-7**—Si kuwa tajiri kwa nje lakini mwenye huzuni kwa ndani, bali tajiri/kidunia/kuwa na nguvu kwa nje na mwenye afya/furaha kwa ndani, mwenye mke mzuri au mume wa kujivunia.
2. **Mst. 6**—Je wamevikwa nini? Kila kitu wanachokitaka!
3. **Mst. 4, 7**—*"Unene"* = Mafanikio/Afya/Mali/Furaha.
4. **Mst. 8-9**—Ona kujifurahisha mwenyewe na kiburi:
   - *"Huweka vinywa vyao"* "ndani ya," "kati," au "kinyume na" ("kupambana kinyume na" au "kwenda tofauti na").
   - Mnara wa Babeli ni wa kweli hata hivyo--a Mungu hakuweza kuuzuia.
   - *"Uwezo wa ulimi"*—wanatamka lolote walipendalo.
5. **Mst. 10-11**—Waebrania (**mst. 10**) ni mgumu:
   - Unaweza kufananishwa na wasioamini wa kidunia au watu wa Mungu.
   - Perowne: "Ni mapana na marefu kiasi gani maji ya anasa za kidhambi ambazo wao, katika tamaa zao kubwa, hunywa." (J. J. Stewart Perowne, *The Book of Psalms, vol. 2 (Psalms 73-150),* [London: George Bell and Sons, 1878; reprint, Grand Rapids, Mich.: Zondervan, 1966], 11)
6. **Mst. 12**—Ufupisho
7. **Mst. 13-14**—Huitofautisha na hali yake mwenyewe.
   - Utajiri wa Waislamu na makandamizo yao kwa Wakristo—"Hakika Mungu yu mwema kwa Israeli, kwa wale wenye moyo ulio safi."

B. ***Mst. 13-14:***

1. Tulimalizia kusoma katika **mst.14**, lakini hebu tufuatilie hatua zetu kwa kitambo:
   - **Mst.1**—Asafu alianzia na kichwa chake cha msingi: "Hakika Mungu yu mwema…" Huanzia karibu sawa na ilivyoanza **Zab 1**: *"Amebarikiwa."*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- **Mst. 2-3**—kwa nini aliteleza kidogo: kwa sababu ya kile alichokiona□alikuwa *ameangalia nje* kwa *watu wengine.*
- **Mst. 4-12**—Alichokiona: Wenye kiburi/waovu/wale walio mbali na Mungu—jinsi wanavyositawi kimafanikio.

2. Kisha, kuanzia **mst.13**, Asafu anaangalia *kwa ndani,* yake *mwenyewe.*
   - UONE: **Mst.13**—"Hakika" (Kiebrania., *akh*), neno lile lile lililoanzia Zaburi **mst.1** = *mwendo wa Zaburi;* lakini mwendo *kwa ndani kuelekea masikitiko.*
   - **Mst.3**—"Wivu" = *kujiangalia mwenyewe, kujipenda* moyoni, kinyume na **mst.13**—"Hakika bure" = *kujihurumia*.
   - **Mst. 5**—"Hawapati *mapigo* kama wanadamu," kinyume na **mst.14**—"Nimepigwa na *kuadhibiwa* ("kutaabika, kudhikika, kupigwa") siku nzima" = *neno lile lile* (Kiebrania, *negah*).
3. Kujiangalia mwenyewe kutasababisha kujihurumia kila wakati—kama hupati kile unachokitaka, na ikiwa mawazo yako yanachokitazama ni *ubapa,* m.y, *watu wengine*, na:
   - Wanafanikiwa wakati wewe siyo.
   - Wana makanisa makubwa/ huduma kubwa, nawe huna.
   - Wana kazi, nawe huna.
   - Wana *kila kitu ambacho unakihitaji* (fedha, mafanikio, heshima, umashuhuri, mvuto, vitabu, jaza-nafasi-mwenyewe), WAKATI WEWE HUNA.
4. Anaangalia *nje* anaona *mafanikio* ya wasiomcha Mungu; ambapo sivyo inavyotakiwa iwe.

Huangalia *kwa ndani* anaona *utupu* na *hasara kimaisha*; hiyo siyo namna ambayo inatakiwa iwe.

III. Ufumbuzi (mst. 15-28) *Hebu tuangalie kwa ukaribu kile Asafu anachokiona:*

A. ***Mst. 15-17—Kiangalizi cha nyuma/bawabu ni mst. 17, lakini kugeuka nyuma huko kulianza na kugutuka/ kusita katika mst. 15.***

1. **Mst. 15**—Alikabiliwa na uchaguzi—lakini Asafu akakumbuka *jukumu* lake la msingi na *wajibu* wake.
   - Kutenda yaliyo sahihi hata kama umekabiliwa na mashaka ya kutisha (Hemingway: Ujasiri = "Neema chini ya shinikizo kubwa").
   - Mashaka na maswali ≠ maadui wa imani—Wasiomcha Mungu hawajiulizi maswali kama hayo; huchukulia mafanikio kirahisi tu, na kunung=unika au kutenda nje ya utaratibu wakati mambo yanapoharibika.
   - Hapa: Mashaka yalikuwa kwa vile alimchukulia Mungu kwa dhati kabisa; ikawa kichocheo cha imani iliyopevuka.
2. **Mst. 16**—Mawazo yanayosumbua ya ndani; hakuna ufumbuzi, lakini:
3. **Mst. 17**—"Madhabahu": Kimaandishi tofauti na kimuundo (huenda yote mawili).
   - Utii wa Asafu licha ya maswali yake na mashaka—mapambano yake na maswala magumu ya jinsi ya kuridhia mafanikio ya wasio haki na kinamna fulani hali ya ushindi wa uovu, kulinganisha na mateso yake, mbele ya wema wa Mungu mwenyewe kulitengeneza njia kwa ajili ya mpenyo mkuu ambao Mungu alikuwa amewapa.

Je Mungu alimwonyesha nini?

B. ***Mst. 18-20—Hali halisi ya wasiomcha Mungu kwa mtazamo wa Mungu***

1. **Mst. 18**—"Hakika": Neno lile lile la Kiebrania *akh* kama lile la **mst. 1, 13.** *Mwendo mwingine—lakini sasa* mwelekeo wa *kwenda juu* kwa Mungu.
2. Mwenzi wa **mst. 4-12**—Hivi ndivyo mambo *yalivyoonekana* kwa Asafu, hivi ndivyo *yalivyo*.
   - *Devil and Daniel Webster*—Nafsi za wasiomcha Mungu hutajwa kama viwavi; lakini si kama hivyo hapa—wasiomcha Mungu ni kama NDOTO.
3. KIPINDI CHA—MAAFA makuu :

   v.9—"*Wameweka" juu* kule *mbinguni* tofauti na **mst.18**—"*Unaweka"* katika *mahali panapoteleza* + "kutupa *chini*."
   - Ni walio kweli & salama kwa Mungu; wanaoteleza pekee ni wale walio mbali na Mungu.
   - Ikiwa unadhani *fedha zako, mafanikio, mamlaka, sura yako, afya, peke yake vitadumu*—UNAOTA NJOZI.
4. IPO haki! Ngazi ya Mungu ni *kubwa zaidi*—kipimo cha muda wake ni *kirefu zaidi.* LAKINI mafanikio ya kidunia *hupeperuka.* Mwisho wao HAUTAWALETEA chochote walichokitegemea maishani; wale wasiomcha Mungu/wale wasio safi moyoni, wanaishi katika ulimwengu wa ndoto; wataondoshwa ghafla. Huo ndio mwisho wao.

C. ***Mst. 21-26: Hali halisi ya wanaomcha Mungu katika mtazamo wa Mungu***

1. **Mst. 21-26**—Asafu anaipata picha halisi ya wacha Mungu.
   - Jawabu lenye ufahamu wa sehemu 2, na uelewa kutoka kwa Mungu kuhusiana na kwa nini *"Hakika Mungu ni mwema kwa Israeli, kwao walio safi mioyoni mwao":*
2. Sehemu ya 1: **mst. 21-22** = mwenzi kwa **mst.13-14.**
   - Hukumu ya haki: Jawabu la *kinyume* ambalo linashughulika na *wasiomcha Mungu.*
3. **Mst.23-26** = Sehemu ya 2 ya uelewa/jawabu:
   - Jawabu *jema* linaloshughulika na *wacha Mungu: Mungu mwenyewe yuko pamoja nao* na *ndiye utoshelevu wao sehemu zote SASA na MILELE.* Hii ndiyo picha halisi ya wacha Mungu.
4. KWA BINAFSI KABISA.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

5. INATOSHELEZA—**mst.23-24** = Matendo Matatu ya Mungu: (1) *"Kushika";* (2) *"Kuongoza";* (3) *"Kukaribisha."*
6. TOFAUTI kuu za ULINGANISHO na *maneno* anayoyatumia; yanayoonekana katika Kiebrania:
   - **Mst.17**—"*mwisho wao"* tofauti na **mst.24**—"*baadaye"* = linatokana na mzizi wa neno moja: (Kiebrania *ahar*).
   - **Mst.18**—*"penye utelezi"* tofauti na **mst.26**—"*sehemu yangu" ("fungu langu")* = mzizi wake ni neno lile lile: (Kiebrania *halaq*).
   - **Mst.12**—"*siku zote"* tofauti na **mst.26**—"*milele"* = mzizi wake ni neno lile lile: (Kiebrania *olam*).

D. ***Huyakamilisha haya yote kwenye hitimisho katika mistari 2 ya mwisho:***

1. Kama alivyoanza Zaburi sawa sawa na **Zaburi 1,** ndivyo Asafu anahitimisha karibu sawa kama **Zaburi 1 (1:6).**
2. **Mst. 27-28—**Ona amefika mbali kiasi gani na jinsi mambo yalivyofikia kugeuka:
   - Amegundua kwamba jawabu haliko kwa hayo ya nje, si katika mazingira ya mtu, bali katika *Mungu mwenyewe:*
   - Ni tofauti kati ya kuwa *mbali na Mungu* (**mst. 27**), na *kuwa karibu na Mungu* (**mst. 28**).
3. Ona tena, jinsi anavyolileta hili pamoja kwa MANENO YASIYOFANANIA NA MLINGANISHO—anatumia *maneno hayo hayo na misemo ile ile* aliyoitumia mwamzoni, isipokuwa sasa kwa uelewa mpya:
   - **Mst.12**—"*Tazama,* hawa ni waovu, siku zote wamestarehe" tofauti na. **Mst.27**—"*Tazama*, wale walio mbali nawe wataangamia"
   - **Mst.2**—"*Bali kwangu mimi,* miguu yangu ilikaribia kupotoka" tofauti na **mst. 28**—"*Bali kwangu mimi,* kumkaribia Mungu ni kwema kwangu."
4. **Mst.28**—"*Nimemfanya Bwana kimbilio langu"*
   - *"Bwana Mungu" ≠ Adonai Elohim,* lakini *Adonai Yahweh* = Jina lake *binafsi Mungu.* (Kutoka **3:13-14**)*,* linaloonekana katika Zaburi hii kwa mara ya 1 hapa: sasa anaweza kumwita Mungu kwa jina.
5. Kwa hiyo, Asafu anahitimisha na *mwenzi binafsi kwa jinsi alivyoanza:*
   - **Mst.1**—"Hakika Mungu ni mwema *kwa Israeli"* kinyume na **mst.28**—"kumkaribia Mungu ni *kwema kwangu."*

Kichwa: Licha ya yaonekanayo kwa nje, Mungu ndiye usalama wetu wa kweli na tumaini.

Uhusiano/Hitimisho:

A. ***Haishangazi kwamba Zaburi 73 ni mwanzo wa Kitabu cha III, kitabu cha kati kati kwa Zaburi zote:***

1. Huangalia nyuma na kutoa sauti ya **Zab 1.**
2. Huendelea kutoka **Zab 72** ambayo ilimtazamia mbeleni mfalme mwenye haki, kutujulisha kwamba Mungu mwenyewe ndiye mfalme wa haki anayetawala sasa na ndiye fungu letu, na kimbilio letu.
3. Inatanguliza jawabu mapema kwa Zaburi inayofuatia, **Zab 74** ambayo ni kilio cha huzuni wakati madhabahu ya hekalu yamebomolewa.
4. Huangalia mbele na kutegemea Zaburi za Kusifu ambazo ndizo zitakazokamilisha kitabu cha Zaburi.

B. ***Sisi wa Agano Jipya tunaweza kuwa na uzoefu mkubwa zaidi wa kweli za Zaburi 73 kuliko Asafu:***

1. Asafu alipaswa kuingia madhabahuni kabla hajapokea ufahamu wake huu mkubwa.
   - Sisi *ni* hekalu; sisi *ni* madhabahu. (**1 Wakor 6:19**).Katika Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu (**Yohn 14:16-17; 16:7**).
2. *Tunaye.*
   - Alisema hatatuacha kamwe. (**Waeb 13:5; Math 28:20**).
   - Hakuna chochote kinachoweza kutuondoa kutoka mkononi mwake (**Warum 8:35-39**).
3. Tunao mwili wake, kanisa (**1 Wakor 12:12-27**).
   - Ametuingiza katika familia yake mwenyewe (**Warum 8:15-16; 1 Tim 3:15; 5:1-2**).

C. ***Kwa hiyo, furahia mpendwa Mkristo, bila kujali hali inayokukabili:***

1. Mungu siyo tu kwamba yu karibu nawe;Yuko *ndani* yako; kwa hiyo *acha kujifananisha na wengine.*
   - Mungu amekuchagua *wewe*—kwa hiyo kuna tofauti gani, ikiwa watu wengine wamejaliwa vitu fulani ambavyo wewe huna?
   - Tutaishi milele na kuwa na kila kitu.
2. Dumisha mtazamo wa *vitu vya nje* kama aliokuwa nao Asafu katika **mst. 17.**
   - Muda wetu ulio mwingi, uelekeo wa mitazamo yetu huwa ni mfupi sana.
   - Dunia hii ni ya kitambo tu, lakini tunaelekea kusahahu kwamba kile tunachokifanya hapa kitaleta matokeo ambayo yataishi milele (**Math 10:24; 1 Tim 6:19**).
   - Kwa hiyo, uutumie muda wako vizuri kwa wengine, kwa sababu unampenda Yesu (**Wagal 6:10**).
3. Dumu katika uaminifu—Mwache awe ndiyo utoshelevu wako, fungu lako, daima.
   - Akitenda kile alichojua kuwa sahihi, hata kama hakuona malipo ya mara moja, ndicho kilichomlinda Asafu asiteleze kuangukia pembeni.
   - Tukifanya kile tunachojua kuwa ni sahihi, hata kama hatuoni malipo ya mara moja, kutatusaidia tukae karibu naye, na—kama AsafuCkutatusaidia kuchota nguvu kwake wakati tunakabiliwa na mashaka, woga, na matatizo.
   - Kama Asafu, kadiri tunavyomruhusu Yeye *atushike* na *kutuongoza* (Roho; Neno—**Yohn 16:13**) yeye *hutupokea* katika utukufu (**Yohn 14:3**).

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

4. Kwa vile ametupokea na kutufanya wa familia yake Kanisa, pata haja zako kutoka kwenye familia kwa ajili ya msaada, na kuwasaidia washirika wa familia yako.

- Familia hujishughulikia yenyewe.
- Anza "kuwaangalia," na kuwatendea waamini wengine kama mama, baba, ndugu wa kiume, na ndugu wa kike "halisi" (**1 Tim 5:1-2**).
- Jenga urafiki kwa Mkristo 1 au 2 ambao utaweza kuwa karibu nao kama ndugu zako wa kiume na wa kike duniani.
- Fanya kitu Juma hili Ck.m, mwalike mtu huyo kwenye chakula, mpelekee zawadi—ili kuunda uhusiano ulio mpya, na wa kina zaidi.
- Mungu anajua tunahitaji uhusiano wa ndani na watu, kama vile tunavyohitaji uhusiano wa ndani na Yeye, ili kuweza kustahimili matatizo tuliyo nayo, na dhuluma tunazoziona katika dunia hii Ckwa hiyo, ametupatia familia yake, kanisa, kutusaidia: hebu tuanze kutumia familia hiyo aliyotupatia kwa wingi mno.

DIBAJI H

Ufu l 9:11-21—Dondoo za Ujumbe wa Muundo Simulizi wa kisa[8]

Utangulizi: Visa vya mikasa /filamu/vitabu/hadithi za siku za kale zisimuliwazo na wazee katika familia.

Sentensi ya Kimpangilio: Tutakwenda hatua kwa hatua katika kifungu hiki na kuona kweli zake zinavyotenda maishani mwetu.

I. Dhana (**Mst. 11-16**)

A. Kristo anarudi duniani.
B. Hili limetabiriwa tangu mwanzo wa Ufunuo.
C. Historia yote imekuwa inasubiria dakika hiyo.
D. Majina ya Yeye aliyepanda farasi Mweupe (m.y., **mst. 11, 13, 16**).
E. Picha (maelezo/tabia na sifa) za Yeye aliyepanda farasi mweupe (m.y, eleza ishara zake).

II. Kilele (**Mst. 17-19**)

A. Majeshi ya mnyama yule yanakwenda kinyume na Kristo.
B. Huwakilisha wale wote wasio wake, bali wanaasi kinyume naye.
C. Yule mnyama, na wafalme, na majeshi yao yote yalikusanyika kinyume na mtu moja Cnani mwenye nguvu zaidi?

III. Ufumbuzi (**Mst. 20-21**)

A. Ingawaje mistari ya vita inachorwa, hakuna vita yoyote inafanyika.
B. Hakuna yeyote anaweza kusimama kinyume na Kristo arudiye.
C. Yule mnyama na Nabii wa uongo wakamatwa; na kila aliyebakia anauawa; uharibifu na aibu.
D. Sura ya hukumu kuu.
E. Yesu ndiye hatima ya ushindi, na Mshindi wa Mwisho katika historia!

Kichwa: Ni lazima tuishi katika hali ya matumaini ya uhakika ya kurudi kwa ushindi kwa Kristo.

Matumizi kiutendaji:

A. ***Kwa waliookoka:***

1. Tunaweza kuishi kwa uhakika.
2. Uhakika huu unapaswa ututie nguvu kuvulimia katika imani yetu, hasa wakati mazingira yetu ni magumu sana.

B. Kwa wasiookoka*:*

1. Hukumu kubwa inakuja, ambayo dunia haijawahi kuiona kamwe.
2. Kama bado humjui Kristo, tubu na ujikabidhi kwake sasa.

[8] Dondoo hii fupi za simulizi wa kisa huonyesha jinsi kifungu hicho hicho cha Maandiko kinavyoweza kuhubiriwa kutumia mipangilio tofauti (fananisha na kielelezo cha MKM cha kifungu hicho hicho [Dibaji F]).

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

DIBAJI I

1 Sam 30:1-31—Kidokezo cha Muundo wa Ujumbe wa Mimi-Sisi-Mungu-Wewe-Sisi

I. Utangulizi (Mimi/Sisi)

A. ***Hali yangu—kushughulikia/kuisafisha nyumba.***

1. "Je imekuja kufikia hivi?"—Sizalishi tena fedha, nk.
2. Kile alichokikamilisha Yesu katika miaka 3; kinyume na mimi.
3. Kujisikia sina thamani/kujiona sina maana.

B. ***Hali za jinsi hiyo huenda haziko kwangu tu.***

1. Akina mama nyumbani/ wafanya kazi wa nyumbani⊂hujisikia wamenaswa: "Sina maisha."
2. Mwanaume (au mwanamke) katika kazi usiyoiumilia.
3. Wanafunzi: "Kwa nini ninajifunza Kemia? Sitaitumia kamwe."
4. Waliostaafu: "Maisha yamenipita bure⊂kamwe sitawaona watoto tena."
5. Wakristo: "Mungu yuko wapi? Simwoni."

Kifungu cha kuvutia cha Maandiko ambacho chaweza kusaidia pale tunapoelekea kuwazia namna hiyo—**1 Samuel 30:**

Kichwa: Kifungu hiki kinatuambia hivi: *"Mungu hutolea thawabu Uaminifu."*

- Hata mambo madogo *hayasahauliki* na yanaweza kuwa *muhimu sana.*

Mpangilio wa hoja kuu: Hebu tupitie kifungu hiki, sehemu-kwa-sehemu, na kuona jinsi Mungu anavyotoa thawabu kwa ajili ya uaminifu.

II. Ufafanuzi wa Ki-Biblia (Mungu)

A. ***Maelezo ya hali iliyopo*** **(mst. 1-6). [SOMA]**

1. Siklagi (**1 Samuel 27**)—Daudi amkimbia Sauli; anaishi na Wafilisti zaidi ya mwaka 1; anapewa Siklagi (Mashariki ya Gaza).
2. Wafilisti wanaenda vitani kinyume na Sauli & Israeli (**1 Sam 29:1**).
   - Daudi anakuwa katika hali ngumu sana.
   - Hata alipoishi na Wafilisti, Daudi hakuishambulia Israeli (**1 Sam 27:8-12**).
   - Kile tukifanyacho nyakati tumeshuka moyo, ni ishara nzuri sana ya kile tunachokiamini kiuhalisi & kama kweli tu waaminifu au hapana.
3. Mungu aupa thawabu uaminifu wa Daudi.
   - Jemadari wa Wafilisti anamshuku Daudi (**1 Sam 29:2-3**).
   - Mungu aupa thawabu uaminifu wa Daudi na Israeli⊂ingawaje Daudi alikuwa ametengwa na Israeli, Mungu alitoa njia ya yeye kutowapiga watu wake mwenyewe.
4. **1 Sam 30:2-6—**Siklag inavamiwa; wake wanachukuliwa; watu wa Daudi wanahuzunishwa mno kiasi kwamba wanataka kumpiga kwa mawe.
   - Ni mara ngapi huwa tunajiingiza katika hali ya kukata tamaa na kushindwa kuona anachokifanya Mungu kwa ajili yetu.
   - Daudi hakuyeyuka na kukata tamaa, bali alikubali kuwajibika & kujitia nguvu katika Bwana.
   - Mithali ya Ki-Afrika: "Hata katika kulia machozi, kiongozi lazima afungue macho ili kuona njia."
   - Kama chumvi na nuru, Wakristo wote ni viongozi: kuwaongoza watu kwa Kristo; kuwaonyesha njia sahihi ya kuishi—kwa neno na kimfano. Mungu huheshimu uaminifu huo.
5. **Mst. 7-10 [SOMA]**
   - *Naivera* = kipande cha mfuko na vazi; kuhani mkuu alikuwa na urimu & thumimu kwa ajili ya kuuliza mapenzi ya Mungu.
   - *Naivera* = kipande cha mfuko na vazi; kuhani mkuu alikuwa na urimu & thumimu kwa ajili ya kuuliza mapenzi ya Mungu.
   - **Mst. 9-10**—wale 200 waliobakia—Wamechoka, lakini walifanya jambo la muhimu sana, kama tutakavyoona baadaye.

B. ***Mst. 11-20—Vita*** **[SOMA]**

1. **MST. 11-15**—Mmisri: "Mungu huupa thawabu uaminifu" (kwa njia zote mbili).
   - *Mmisri* aliponya maisha kwa kutoa habari.
   - *Daudi/Israeli* waliipata habari muhimu waliyokuwa wanaitaka—Daudi angweza kumuua huyo (alikuwa mgeni & mshiriki wa jeshi la upande wa adui); badala yake alimwonyesha huruma (ona **Math 10:42**).
   - Usishikike sana na "mambo makubwa" ya maisha haya, au yale tunayotaka kuyafanya kwa Mungu, kiasi kwamba tudharau yale yaonekanayo kuwa ni madogo na kuona "watu wasio muhimu."

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Mungu anao mpango kwa ajili yao (sisi) na yale "mambo makuu" yataweza *kuning=inia kwenye michango yao* ("kwa kuhitaji msumari")—hapa, ushindi wa Daudi ulininginia kwa huyu Mmisri aonekanaye kama si muhimu.
- Linganisha tofauti kati ya huruma ya Daudi kwa adui & kule *kukosa huruma* kulikoonyeshwa na mkuu wa Waamaleki wa Misri kwa mtumwa wake mwenyeweCkukosa huruma kule kulirudi na kusababisha kuchinjwa kwa WaamalekiCkweli, "Mungu huupa thawabu uaminifu."

C. ***Mst. 21-25—Malipo ya mara moja*** **[SOMA]**

1. Daudi alitambua kwamba "Mungu huupa thawabu uaminifu" (**mst. 23**—"*Bwana ametupatia"* ushindi).
2. Wale 200 kinyume na 400:
   - *Wale 200 walikuwa wamechoka, lakini walikuwa waaminifu kwa kile walichokuwa nacho*—Walivilinda vyombo. (**Mst. 24**).
   - *Pia walitumika kama walinzi wa nyuma*—Siklagi ulikuwa umechukuliwa kwa sababu Daudi *hakuwa* ameweka wapiganaji wowote kuulinda mji.
   - Katika mapambano kwa ajili ya roho za watu, wengine huenda nje (umisheni); wengine wanahitajika kubakia na kutoa fedha; wengine wanahitajika kukaa na kutunza nyumba.
   - *Wale 400 waliopigana walikuwa wachoyo*—waama walikuwa wanawazia kwamba watakuwa ndio wakuchukua, nyara zile zikawa *"nyara za Daudi"* (**mst. 20**)—walionyesha kwamba *fedha zetu zinatudhihirishia jinsi halisi tulivyo.*
   - *Wale 400 walikuwa hawaoni mbali*—katika mapambano mbele yao, wale 200 wangehitajika (na baadhi ya wale 400 waweza kuwa walinzi)—lakini walikuwa tayari kuwa na 1/3 ya nyara za jeshi la Daudi.
3. "Mungu huupa thawabu uaminifu," *lakini huwatumia watu wake kufanya hivyo.*
   - Hapa Mungu amtumia Daudi kwa yote; kuweka *msimamo* na *kuutekeleza*.
   - Daudi alikuwa anaheshimika sana kwa sababu yeye hakuwa mlipiza kisasi, badala yake—*aliongoza kwa mfano.*

D. ***Mst. 26-31—Matokeo ya muda mrefu*** **[SOMA]**

1. Daudi pia alishirikisha nyara kwa wazee wa Yuda.
2. Pia alishirikisha nyara zake na rafiki zake *"na kwa hao wa kila mahali alipozoelea Daudi mwenyewe kwenda"* (**Mst. 31**).
   - Wakati Daudi alipokuwa anamkimbia Sauli, watu hawa walimwonyesha urafiki na ukarimu.
   - Walikuwa waaminifu kwake, ikiwezekana hata kuhatarisha maisha yao wenyewe.
   - Huenda hawakuwa wanategemea thawabu ya aina yoyote, na huenda walishasahau hata ule wema na matendo waliyoyafanya.

III. Matumizi Kimatendo na Maono/Hitimisho (Wewe/Mimi)

A. ***Matumizi kimatendo (Wewe)***

1. Hali zote hata zile ambazo hazina umuhimu kabisa, kama wale watu 200 waliokuwa wamechoka na yule Mmisri mgonjwa ni wa muhimu.
   - Ikiwa wewe ni mwaminifu katika mambo madogo, Mungu hasahau au kuyaweka kando hayo (**Luka 16:10**).
2. Yale yaonekanayo kuwa si ya muhimu yaweza kuwa kiungo muhimu katika mnyororo unaoongoza kwenye matokeo makuu na ya muhimu ("kwa kuuhitaji msumari").
3. Mtazamo huu unatakiwa utuonyeshe kwamba maisha yetu yaonekanayo kama hayana maana nyumbani, au shuleni, au kazini, siyo hayana maana—bali yanakuwa yamewekezwa na maana fulani.
   - Twaweza tusione matunda/ thawabu kwa muda mrefu (kama wale wa Betheli, Ramothi, and Jatiri), bali hatukati tamaa.
4. Kwa sababu Mungu huwatumia watu wake ili kuupa thawabu uaminifu, twaweza kutafuta uaminifu wa wengine (kama alivyofanya Daudi), na *kuwatia moyo, kutambua, na kuwapa thawabu.*
5. Hebu tujaribu juma hili kutambua na kutangaza—hata thawabu—angalau *tendo moja la uaminifu* la mtu mwingine: *ajuaye hili laweza kuelekea wapi?*

B. ***Maono/Hitimisho (Sisi)***

Vipi kama sote tungeanza kufikiri na kutenda kwa jinsi hii?

1. Manunguniko mengi, na "ole wangu" kupungua.
2. Watenda kazi wenzetu, wanafunzi wenzetu, marafiki wanaweza kugundua kwamba huwa hatukati tamaa, au kuwa na machungu kama walivyo wengi—na hilo linaweza kimaumbile likazungumza nao kuhusiana na Yesu.
3. Fikiria jinsi ambavyo ingetia nguvu na kutoa moyo, kama tungelitambua uaminifu wa wengine:
   - Dunia haifanyi hivyo.
   - Hapo ndipo kanisa litaweza kuwa tofauti sana na dunia.
4. "Mungu huupa thawabu uaminifu"—Hajasahau, au kutupuuza. Anataka kututumia kama vyombo vyake kuheshimia uaminifu wa wengine.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

DIBAJI J

http://cecl.glcc.org/PDF/Lori_Carrell/sermons%20likley%20to%20succeed.pdf

MAHUBIRI YENYE UWEZEKANO MKUBWA WA KUFANIKIWA

Na LORI CARRELL

Je mahubiri kiukweli hubadili kuamini na tabia? Utafiti unaoendelea unafunua hoja ngumu.

Utafiti mpya unagundua tabia za mahubiri zinazoleta matokeo yadumuyo muda mrefu. Uchunguzi ulianzia kwa utafiti na mahojiano kulinganisha mitazamo ya wasikilizaji na ya wahubiri katika makanisa 102 ya nchi. Hivi sasa, mradi unaosaidiwa na Lilly grant kushirikiana na Center for Excellence in Congregational Leadership (kituo cha Ubora wa Uongozi wa Washirika) cha Ukumbi wa Kituo cha Green Lake, kimepanuka zaidi kwani wachungaji 52 wa Kipentekoste na wasikilizaji wao zaidi ya 5,000 wanashiriki katika mchakato wa kina wa tathmini ya mawasiliano ya mahubiri. Jambo kuu lililopatikana katika utafiti huo hadi leo ni kuwa wasikilizaji huthamini mahubiri, wakitambua kwamba mahubiri ni sehemu ya ibada yenye uwezo wa kuletesha kukua kwao kiroho. Kusema ukweli, wasikilizaji huwapenda wahubiri wao na kueleza kitakwimu kama dada moja mhojiwa alivyoeleza jinsi alivyoonyesha katika kauli yake, "Wachungaji hawajaishiwa—usikosee!" Wakati huo huo, mwitikio wa wasikilizaji pia hufunua kwamba ni mahubiri machache ambayo huleta matokeo ya mabadiliko ya kudumu. Wachungaji na wasikilizaji wanakubaliana kwamba badiliko kama hilo ni matokeo yaliyotakiwa ya mawasiliano ya mahubiri, na hata hivyo si kawaida. Tathmini ya mahubiri hayo machache ambayo "yana uelekeo mkubwa wa mafanikio" katika kazi ya changamoto ya mabadiliko ya kiroho inafunua sifa zifuatazo.

Mahubiri Yenye Mafanikio Hutaka Mabadiliko

Mahubiri yenye mafanikio hujengwa kuzungukia lengo lililotajwa wazi la mabadiliko linaloibukia kutokana na Maandiko; kwa mfano, "Wasikilizaji wawaombee adui zao" (Mathayo 5:46-48). Kwa mahubiri yasiyoleta mabadiliko zaidi, mabadiliko yanayotakiwa yanaweza kuhimizwa au kuelekezwa ("kuielewa neema"), lakini wasikilizaji hawawezi kutofautisha wito dhahiri wa kubadilika. Jambo la kuvutia, utafiti huo unaonyesha kwamba wasikilizaji bado wanaridhishwa na mahubiri yasiyowataka wabadilike, lakini wanasema kwamba matokeo ni uimarishaji, na siyo kukua. Katika mahubiri yenye matokeo madogo zaidi, sehemu kubwa zaidi ya mahubiri huchukuliwa na maelezo, utengenezaji wa mahubiri ambayo zaidi ni ya habari kuliko mabadiliko. Zaidi ya hayo, miitikio ya wasikilizaji huonyesha kwamba kile kinachoelezewa tayari kinafahamika kwao. Ikiwa wasikilizaji tayari wanaendana na maudhui ya mahubiri, je wanatarajiwa kubadilikaje? Mahubiri yenye mafanikio huwasukuma wasikilizaji kwenye matendo. Kuliko kushawishi tu hamasa ya kuwa tofauti (kwa mfano, "Ndiyo, ningelipenda niwe ninasamehe zaidi"), mahubiri yenye matokeo ya kudumu hujenga mawazo ya kimatendo, kutangaza nguvu na neema ya Mungu kuwezesha kukua kiroho. Iwe kwamba mkakati wa matendo umeonyeshwa kupitia simulizi au hatua fulani rasmi, wito wa kubadilika una uelekeo mkubwa wa kufanikiwa kutokea pale mawazo ya "jinsi ya kufanya" yanapochanganywa.

Mahubiri Yenye Mafanikio Huwa Yamepangiliwa Ili Kusikilizwa

Mahubiri yenye mafanikio ni mahubiri ambayo wasikilizaji wanaweza kuyakumbuka. Mpangilio wa fikira ndio ufunguo wa mchakato huo wa kuyakumbuka. Kulingana na wasikilizaji, mahubiri yaliyopangiliwa vizuri ambayo husaidia ukumbukaji ni adimu. Kwa wahubiri wengi, kifungu chenyewe huleta muundo, mstari wa pili huja baada ya mstari wa kwanza, kwa hiyo "huhubiri kupitia kifungu hicho," wakichambua mawazo wanayokutana nayo. Mkabala wa aina hiyo waweza kupatikana kama mvurugano wa kimuktadha ambao wasikilizaji huuita unachanganya. Ikiwa maudhui yanaonekana hayajaunganika, nguvu ya usikilizaji, upokeaji, na uwezekano wa kuhamasika hupungua. Walipoulizwa nini hufanya mahubiri kuwa magumu kukumbukwa na kutafakarika, jawabu #1 kutoka kwa wasikilizaji lilikuwa "kutokuwa na mpangilio."

Kufuatia ufafanuzi wa Maandiko, wahubiri wanaotoa ujumbe wenye matokeo yadumuyo muda mrefu hutumia muda wa maandalizi *wakipangilia mawazo kwa namna ambazo wasikilizaji wanaweza wakaifanyia mchakato.* Mahubiri kama hayo huandalika kwa ajili ya mawasiliano ya mdomo - sikio; yaani, mhubiri huongea na msikilizaji husikiliza. Kuchagua mahubiri yenye muundo wa uegemezi wa msikilizaji ndiyo sehemu nyeti ya uongozi wa wachungaji wakiwa wanatafuta kuwaelekeza wasikilizaji kuelekea kukua kiroho. Vipengele muhimu vya mahubiri yaliyopangiliwa kwa ajili ya wasikilizaji huwa na:

- **ufunguzi wa kukamata usikivu wa wasikilizaji ili kufanya akili zao zielekee kwenye somo lililoibuliwa dhahiri.;**
- **lengo rasmi la kukuza kiroho lililoambatanishwa katika utangulizi;**
- **hoja kuu mbili au tatu zilizoungana, zinazokumbukika zilizopangika kimaneno;**
- **viunganishi vya ki-muktadha kati ya hoja kuu ambazo zinawahamisha watu kutoka wazo moja kwenda linalofuata;**
- **Muhtasari mahususi ambao hauna maelezo yaliyozidi; na**
- **kauli inayosukuma ya kumalizia inayohusiana na lengo la kukua kiroho.**

Mahubiri yenye uelekezi wa wasikilizaji *hubakia kwenye uelekeo rasmi,* yakitoa taarifa *za kina* za kimpangilio kwa ajili ya mchakato wa kiusikilizaji, pia huwa na nidhamu katika kuchagua maudhui ili kwamba mahubiri yawe na kina badala ya kuwa mapana. Mahubiri mapana huwa na tabia ya kuwa na hoja nyingi mno, hoja kupapaswa juu juu, maelezo kuzidi mno, hoja zinazofahamika tayari kutolewa maelezo mengi mno, maelezo ya kurudia- rudia mada, kusogelea bila kugusa, au marefu bila sababu. Katika mahubiri mapana, nguvu za usikivu huyeyuka, ambazo ndizo za kuwezesha matokeo ya kudumu. Mahubiri ya kina huwa yametajirika, yakiwa na uelekeo rasmi, yenye maudhui ambayo yana sifa hizi:

- **hudumu katika uhusiano wa wazi na Maandiko;**

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

• bila shaka huunganika na lengo lililotajwa la kuletesha mabadiliko;
• huletesha kuelewa;
• huwianisha kati ya ufahamu na hisia;
• hubainisha mawazo ya kutendea kazi; na
• huitaja neema na nguvu ya Mungu kuwezesha badiliko.

Mahubiri Yenye Mafanikio Hutolewa Vizuri

Mahubiri yenye uwezekano mkubwa wa kufanikiwa huweza kuhubiriwa na wahubiri kwa staili tofauti za kimahubiri, kuanzia hali ya mhubiri mwenye shauku, ya sauti laini; hadi mahubiri ya sauti ambayo husababisha joto mwilini na kuleta shauku. Yaliyo ya kawaida ni yale yanayoelezea kiuhalisia kabisa mahusiano na hisia.

Chini ya asilimia 2 ya wachungaji walitafiti mazoezi ya mahubiri ya mdomo. Katika kupima uhitaji wa muda wao, wachungaji wanafunua kwamba unenaji jumbe haujalishi ki-paumbele. Wasikilizaji wana mtazamo tofauti, wakieleza kwamba unenaji ujumbe una umuhimu sana. Hasa hasa, baadhi ya tabia za unenaji (kama vile kusoma au ishara fulani inayotabirika) hufanya ionekane kwa wasikilizaji kwamba mchungaji wao "kwa kweli haonyeshi kujali." Jinsi tunavyosema kile tukisemacho huleta maana za kimahusiano na kihisia, iwe kwa makusudi au hapana.

Jinsi mchungaji anavyotoa maneno ya mahubiri huonyesha moyo halisi wa Mungu kwa watu wake. Utoaji ujumbe pia huonyesha hisia ya mchungaji kuhusiana na wasikilizaji, mada hiyo, na tendo la kuhubiri.

Wakati mwingine, wachungaji wanaojitahidi kutoa mahubiri (au kufundisha) ambamo "wanaelezea mambo kwa njia nzuri, ya kawaida, na inayofikika" pasipo kusudia hupooza nguvu ya maneno. Katika sehemu ya utafiti huu ulioandaliwa kutambua "ubora wa kipekee" wa wahubiri, "matumizi ya lugha ya nguvu na yenye msukumo" ulikuwa nguvu adimu kuliko zote. Uchaguzi wa maneno huathiri kumbukumbu na hamasa ya wasikilizaji. Wasikilizaji huonea shauku sana "kutiwa nguvu", kama sehemu ya kile kiwasaidiacho kukua kiroho; wasikilizaji pia hutambua mahubiri yanayotumia maneno yenye nguvu kama yenye kutia nguvu zaidi kuliko yale yenye kimsingi, lugha ya kimaelezo. Usanii na maneno yanayoibua taswira ionekanayo; ingawaje ya ukali na maneno yanayojenga usawia wa michakato migumu ya kiroho; kusisimua nafsi kwa maneno yanayoshawishi yanayohamasisha hisia kwa njia ya marudio ya silabi za mwanzo, kurandana, na ujenzi wa neno kwa kuiga sauti—yote huweza kupatikana siyo tu katika mahubiri yenye matokeo ya kudumu, lakini pia katika mawasiliano ya hadharani ya Yesu.

Mahubiri Yenye Mafanikio Huhusisha Mitazamo Ya Wasikilizaji

Mahubiri yanayoheshimu na kuhusisha maisha ya wasikilizaji huelekea zaidi kuwa na mafanikio katika lengo linalokusudiwa. Wakati wachungaji waonyesha mwito mkuu wa wasikilizaji kutaka "kuona umaana" kwaweza kuwa ni himizo mbali na Maandiko, wasikilizaji waelezea shauku yao ya kuunganishwa moja kwa moja zaidi. Kwa vile asilimia 78 ya wasikilizaji hawajawahi kuongea na wachungaji wao kuhusiana na mahubiri, haishangazi mtazamo kuhusu swala hili kutofautiana kwa kiwango kikubwa. Wengi wa wachungaji na viongozi wa Parishi hawazungumzi kabla au baada ya mahubiri kuhusiana na mahubiri hayo, na bado wote wanategemea matokeo ya badiliko la maisha. Matokeo yake wachungaji wengi huandaa mahubiri yatokanayo na hisia za kubuni kuhusiana na wasikilizaji (kwa mfano, asilimia inayokadiriwa ya "wanaoyahitaji") huendelea pasipo uelewa rasmi wa mtazamo wa wasikilizaji kuhusu mada au kifungu kilichochaguliwa.

Je wahubiri wawezaje kuvuka fikira za kudhania inapohusu kuunganisha maudhui kwa wasikilizaji? Mchakato unaohusiana na mahubiri yenye mafanikio ni kundi la mazungumzo kabla ya mahubiri ambamo mchungaji "anawasikiliza wasikilizaji." Nyakati za mazungumzo kama hayo, matayarisho ya mchungaji husaidiwa kwa majadiliano ya wasikilizaji juu ya kifungu cha mahubiri yaliyo mbeleni au masomo yanayoingilia safari zao za kiroho. Utafiti huu unaonyesha kwamba vipindi vya usikilizaji vya jinsi hii vyaweza kuongeza ubora wa mageuzi ya mawasiliano ya mahubiri. kwa...

• kuibua mawazo ya mahubiri mapya (uhitaji wa kipengele kulingana na wachungaji);
• kuongeza umaana wa mahubiri (uhitaji wa kipengele kulingana na wasikilizaji);
• kuongeza nguvu itolewayo kwa kusikiliza wakati wa mawasiliano ya mahubiri;
• kuongeza urasmi na kina cha taarifa za mwitikio usio rasmi upokelewao na wachungaji baada ya mahubiri; na
• kuwatia nguvu wachungaji kibinafsi na kitaaluma kwa kuungwa mkono na wasikilizaji na maombi wakati wa maandalizi ya mahubiri.

Ndiyo, mahubiri yanaweza kubadili kuamini na tabia, hata hivyo kuna mengi zaidi ya kujifunza kutoka kwa wasikilizaji na wahubiri kushiriki kwenye utafiti huu wa mawasiliano ya mahubiri yenye kuleta mabadiliko. Hebu wimbi hili la kwanza la ugunduzi liangaze sifa za mahubiri ambayo yana "uwezekano zaidi wa kufanikiwa" lichochee kufikiri kwako, liongeze nguvu za maombi, na liongeze nguvu yale matokeo ya kudumu.

LORI CARRELL, *Ph.D., (Profesa wa Elimu ya Mawasiliano Chuo Kikuu Cha Wisconsin-Oshkosh) ni mwandishi wa* The Great American Sermon Survey (Utafiti Mkuu wa Mahubiri ya Amerika) *(1999) na kwa sasa anafanya utafiti kuhusu "Mawasiliano ya Mahubiri Yenye Kuleta Mabadiliko" kati ta washiriki wa Kituo cha Ubora wa Uongozi wa Washirika, kwa kusaidiwa na Lilly Endowment, "the Green Lake Conference Center", na "the UW system".*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

DIBAJI K

http://cecl.glcc.org/PDF/Lori_Carrell/wasting%20time.pdf

JE UNAPOTEZA MUDA WAKO WA MAANDALIZI YA MAHUBIRI?

Na LORI CARRELL

Akiwa anakamua mpira wa kukabili shinikizo kwa mkono moja, na huku akigonga mguu sakafuni kwa mafadhaiko, mchungaji aliye rafiki yangu alitoa mwitikio wa haraka pale nilipomuuliza kuhusu maandalizi ya mahubiri yake: "Siwezi kupata muda mwingine, kwa hiyo hakuna sababu ya kuongea kuhusu hilo!" Kwa wote wanaohubiri, mkandamizo wa maandalizi ya mahubiri ni uhalisi usiokwepeka. Utafiti wa hivi karibuni wa Google unaohusu "kuokoa muda wa maandalizi ya mahubiri" ulileta zaidi ya miitikio 50,000. Lakini utafiti wetu unafunua kwamba badala ya kujaribu kuandaa kwa muda mfupi zaidi, ni muhimu zaidi kuuliza, "Nawezaje kutumia ki-ubora zaidi muda wowote wa maandalizi nilio nao?" Kundi la wahubiri walijiandikisha kwenye Kituo cha Lilly cha Ubora wa Uongozi wa Washirika huko "Green Lake Conference Center" na washirika wao wanaturuhusu kwa neema kutupa fursa isiyo ya kawaida kujifunza kutokana na uzoefu wao. Tunaamini pamoja nao kwamba mawasiliano ya ki-mahubiri yanapaswa mara kwa mara kuleta mabadiliko yanayoonekana na yanayodumu katika maisha ya watu. Hivyo tunajaribu kutafuta nini kinachosaidia, kutumia yaibuliwayo kwa wasikilizaji kama kipimo cha matokeo. Katika sehemu hii ya mafunzo, wachungaji waliandika kwa makini muda wa maandalizi yao ya mahubiri na shughuli zake, walivyojitahidi kuongeza kabisa uwezo wao wa kuleta mabadiliko ya mahubiri yao. Tulichokigundua ni kwamba *jinsi* wahubiri wanavyotumia muda wao wa maandalizi, hujalisha zaidi kuliko hata *kiasi cha muda* wanaoutumia.

Desturi za kawaida

Waweza kuwa wajiuliza kidogo kuhusu jinsi maandalizi ya mahubiri yako yanavyolinganishwa na desturi za kawaida za wahubiri wengine. Kitu cha kwanza unachotakiwa kukijua ni kuwa wachungaji wanaochagua masomo miezi mingi kabla, na wale wangojeao hadi kuvuviwa Jumamosi usiku hulingana kwa kitu kimoja: *kamwe* hakuna muda wa kutosha wa maandalizi.

Huchukua muda gani kwa wahubiri walio wengi kuandaa mahubiri yao?

Wakati, muda hutofautiana kuanzia saa 5 hadi saa 20, muda wa wastani wa maandalizi hudumu kati ya saa 12 na 13 kwa juma. Lakini wachungaji wengi walieleza "kuishi na" mstari fulani juma zima—wakati akioga, akiongoza kikao chenye watu jeuri, au anakamua mpira wa kukabili shinikizo.

Wahubiri hufanya nini katika saa zile za maandalizi ya mahubiri?

Karibu wote hutumia muda ulio mwingi wa maandalizi peke yao wakiwa, wanajifunza Maandiko na kuandika muhtasati na nukuu. Yanayofanyika nyakati za "kijifunza Maandiko" ni pamoja na ufafanuzi wake, kuchunguza Maandiko kutoka vitabu tofauti, kulinganisha mistari, kusoma itifaki, na kujifunza kuhusu viini vya maneno. Mambo mengine yanayofanyika kikawaida huhusiana na kuyapitia (asilimia 57), kufanyia mazoezi ya ndani (asilimia 47), kusoma vitabu vinavyohusiana (asilimia 47), na kuandaa viambanishi vya kusomeka (asilimia 36).

Ufumbuzi usio wa kawaida

Kadiri utafiti huu ulivyoendelea, wachungaji walianzisha namna mapya za maandalizi ya mahubiri ili kufanya mahubiri yao yalete mabadiliko zaidi. Wakati muda walioutumia ulibakia ule ule, walibadilisha jinsi ya kuutumia muda wao. Wachungaji walipunguza muda utumikao kusoma vitabu vingine vinavyohusiana, kuangalia vyombo vinavyotoa habari hizo, na kufanya marudio. Walifanya nini badala yake? Hapa pana mambo manne yaliyowasaidia kufanya maandalizi ya mahubiri yenye uwezo wa kuleta mabadiliko zaidi kwa wasikilizaji.

1) Kutambua lengo maalum la mahubiri

"Changamoto yangu ya msingi ilikuwa kuwa mwenye ujuzi zaidi na kukazia nini mahubiri yanataka yafanye kwa watu."

Je unaweza kutaja malengo ya mwitikio wa mahubiri yako matatu ya mwisho? Je wasikilizaji wako nao wangeweza kuyataja hayo? Wachungaji wengi wanaweza tu kutaja vichwa vya mahubiri, vifungu vya Maandiko, au mawazo ambayo wasikilizaji wao kwa sasa wanayafahamu. Wachungaji katika utafiti huo waliarifu kwamba, kuwa na lengo rasmi husaidia kuunda kufikiri kwao muda wote wa mchakato wa maandalizi. Kwanza, unavyojifunza Maandiko, tafuta upate somo ambalo liko wazi, lenye msukumo, na linalohusiana na Maandiko. Somo hilo likishapatikana, ruhusu lengo rasmi, lenye matarajio ya juu liibuliwe. Muda wa maandalizi utumiwao kuunda lengo la kukua kiroho hupunguza muda wa marudio na huleta maudhui yaliyo na malengo rasmi zaidi. Muda wa maandalizi utumikao kwa njia hii hulipa katika swala la matokeo ya upokeaji wa wasikilizaji.

2) Shughuli za kukuza kiroho kibinafsi

"Nahitajika niache nafasi ya Roho Mtakatifu kufanya kazi."

Wachungaji kadhaa walitambua kuwa walikuwa wanapuuza safari zao za kiroho. Wale waliofanya mabadiliko katika eneo hili la maandalizi ya mahubiri walielezea kuhusu kukutana na uzoefu wa ongezeko la unyofu, uvuvio, na hata nguvu. Mabadiliko

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

yasiyotambulika rasmi katika kuhubiri yaliyoambatana na mazoea ya maandalizi haya yasiyo ya kawaida, yalitofautiana: Kwa baadhi, kujitangaza kuliongezeka kwa sababu hali ile ya uwazi ilikosekana, wakati kwa wengine, kujitangaza kulipungua kwani kiburi kilishuka. Pasipo kujali marekebisho maalum, kama wahubiri watatumia muda mwingi zaidi katika kutafakari, kuweka kumbukumbu, au kuwa na faragha za kibinafsi; wasikilizaji watataarifu matokeo makubwa zaidi kuhusu mahubiri juu ya maisha yao ya *kiroho.*

3) Mazoezi ya mdomo

"Miaka inavyokwenda, huwa najikuta nahamia mbali zaidi na maandalizi ya mahubiri kwa jinsi mambo yanavyonichosha—na kwa kiburi. Nikidhani kuwa najua nifanyalo, hutumia muda mdogo zaidi na zaidi kujiandaa. Sikufikiria nahitaji mazoezi ya mdomo. Nilijiona mzuri wa kutosha."

Wachungaji wengi hukataa kutumia muda wa thamani kujiandaa kupitia ujumbe wao. Wakati ni kweli kwamba mazoezi ya mdomoni husaidia matumizi ya lugha na kuleta mtiririko, huo si ugunduzi wa maana haswa. Kubadilika kutoka mazoezi *ya ndani* ("kupitia kichwani tu") kuja mazoezi *ya mdomoni* huathiri mpangilio. Kutamka kwa nguvu husaidia wahubiri kuchambua mawazo makuu, kudumisha mkazo, kuzuia kwenda upande, kuunda vibadilisho, kufanya utambulisho na hitimisho kuwe kukamilifu zaidi na kulete msukumo, na kufanye matumizi mazuri zaidi ya muda wa maandalizi ya mahubiri. Wasikilizaji wanasemaje? Mahubiri yaliyoandaliwa vizuri zaidi, huwa yana uwezo wa kuleta mabadiliko zaidi.

4) Kuongea na wengine

"Mimi hutumia muda mwingi mno kushughulikia mashaka yangu binafsi, nikiwa najiuliza thamani ya kile nikifanyacho. Nahitaji mawazo mapya. Husubiri kwa ajili ya kuvuviwa nguvu mpya, lakini kisha hunibidi nihangaike ili kufanikisha. Ni mchakato wa kipweke."

Kwa sehemu ndogo ya wachungaji ambao huzungumzia mada za mahubiri ya mbeleni na wake zao, wasikilizaji, au wachungaji wengine, matokeo huongezeka. Kwa vile wachungaji wachache mno huchukua hatua kutenda hili, ufunuo huu ndio unagusa zaidi ndio wa kuelekea kuliko wote. Lakini angalia: Wasikilizaji wanapodai umaana, na wahubiri wanatamani upya wa yale yaliyozoeleka; kujihusisha na mazungumzo kabla ya mahubiri na wana parishi kwaweza kutia nguvu maandalizi ya mahubiri na matokeo. Mazungumzo ya kimataifa na wanadoa na watu wa makundi ya umri moja (hata kupitia barua pepe) pia huonyesha kuleta tofauti. Mawasiliano ya mahubiri ni uongeaji *hadharani*; hivyo uzoefu wa maandalizi ya upweke waweza usitosheleze.

Je unataka mahubiri yako yawe na matokeo makubwa zaidi? Unaweza usiwe na muda zaidi wa maandalizi ya mahubiri, lakini unaweza kutumia muda huo kwa namna tofauti. Mabadiliko ni magumu kufanyika. Mchungaji moja anasema, "Tunawaomba watu wabadilike kila juma, lakini kubadili sifa za mahubiri yangu kulikuwa kugumu zaidi kuliko nilivyowahi kudhania." Unavyojitahidi kukabili shinikizo na kuzidisha uwezo, fikiria hatua hizi zisizo za kawaida za maandalizi, na uombe kwa ajili ya matokeo yasiyo ya kawaida.

LORI CARRELL *ni profesa wa mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Wisconsin-Oshkosh. Mwanamke huyo anaendelea na utafiti wake na wachungaji wa CECL (cecl.glcc.org). Tazama mtandaoni "Dr. Lori's Blog" anuani ya askgodtv.com*

DIBAJI L

http://cecl.glcc.org/PDF/Lori_Carrell/not%20so%20simple%20sermon%20solutions.pdf

FUMBUZI-ZISIO-RAHISI SANA ZA MAHUBIRI

Na LORI CARRELL

Je unatafuta vidokezo vya haraka vya kuleta mapinduzi ya nguvu za mahubiri yako? Usitafute zaidi—kwa sababu havipo. Kadiri utafiti wetu wa mawasiliano unavyoendelea, kitu kimoja kinakuwa wazi: hakuna ufumbuzi mrahisi. Badala yake wazia kujidhatiti kimuda mrefu, siyo kurekebisha. Je unaamini kwamba mahubiri yanatakiwa kuleta matokeo ya mara kwa mara ya maisha, maisha, jumuiya, na desturi? Kuhubiri *kwako*, siyo tu kuhubiri kiujumla? Uko tayari kupambana na changamoto ya kuwezesha nguvu ya mabadiliko ya mahubiri yako? Kama ni hivyo, zifuatazo ni hatua zisizo rahisi sana—nyingi zake huhitaji ushiriki wa rafiki unayemwamini.

Tazamia Kuhubiri Kuwe Kipaumbele

Kila badiliko linahitaji msukumo. Kwa mfano, ikiwa wewe unaridhika na kipato cha Paundi tano, asitarajie kuvuka hizo. Mchungaji moja hivi karibuni amekiri kwamba matarajio yake yamepungua kwa miaka, kiasi kwamba sasa, mahubiri yake yalionekana kama "kazi ya kukidhi haja tu." Wasikilizaji nchi nzima wangelivunjika moyo sana kusikia hilo. Wanatarajia kuhubiri kuwe ndiyo jukumu la kiuongozi la mchungaji wao lililo muhimu zaidi. Nini matarajio yako? Umeitwa kusimama kwa ajili ya Yesu na kunena neno halisi la Mungu. Je umetindikiwa au kutosheka? Kichocheo cha badiliko daima ni mgogoro, lakini dhamiri ya dhati kuhusiana na wito wako pia uwe kichocheo. Je Mungu alikuita kuhubiri? Hebu rudia wito wako.

Uwe Mkweli Kuhusu Matokeo

Kama unataka kufanya mabadiliko katika kuhubiri kwako, anzia kwa kuorodhesha msaada wa rafiki yako na kutenga muda wa kukusanya habari na viashirio vya matokeo. Ni muhimu kufanya mambo yafuatayo kwa majuma kadhaa, kama unataka kutathmini kwa dhati maandalizi ya mahubiri yako na matokeo yake.

Tathmini Mchakato wa Muda wa Maandalizi Ya Mahubiri.

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Kama vile mtu anavyotunza takwimu za ulaji wa vyakula na mazoezi, unatakiwa kufuatilia muda wako wa maandalizi na mchakato wake. Unafanya nini wakati wa maandalizi? Je unayafanya hivyo kwa muda gani? Je unacheua wakati unaendesha gari? Je huwa umejaa tele wakati unasikiliza muziki? Maombi yanaingilianaje na mchakato huo? Ili kutambua kipi kinafanya kazi kwako, jadili mkondo wako wa maandalizi na rafiki yako aliyekubaliana kuwa mtenda kazi mwenza wako.

Rekodi Video Mahubiri Yako na Uyaangalie.

Hata kama utahitaji kuazima au kununua kamera hiyo na kumfundisha mtu kupiga picha mahubiri yako, fanya hivyo. Elewa kwamba mkanda duni hautakusaidia (ebu jifikirie mwenyewe kuwa ni kakivuli kadogo nyuma ya jukwaa). Sasa hapa ndipo palipo pagumu: Tafuta bakuli la bisibisi na yule rafiki yako mwaminifu na muangalie mahubiri yako. Hebu jiweke nafasi ya msikilizaji, siyo mtathimini. Jiulize, "Je Mungu aliongeaje kupitia mhubiri huyu?" Yakusanye maoni yako kisha uyajadili.

Omba Miitikio ya Wasikilizaji na Uipitie.

Weka na ufuatiliaji mdogo katika kijarida chako, ukiwauliza wasikilizaji wako kuchangia wanavyopokea mahubiri yako (hili si kwa kusudi la kukosoa mahubiri). Weka swali lenye nafasi ya kujibu kama vile "Nini mwitikio wako kuhusu mahubiri haya?" Au orodhesha maswali machache ambayo wasikilizaji watajibu kwa kusema ndiyo au hapana. Kwa mfano, "Nilikumbushwa kitu ambacho tayari nilikuwa nakiamini; Napanga nichukue hatua kutokana na mahubiri haya; au Nimefanya uamuzi wa kubadili imani yangu." Fanya wasikilizaji wasijitaje majina, na mteue mtu wa kukusanya maoni hayo. Pitia maoni hayo yaliyokusanywa pamoja na huyo rafiki yako wa kweli, ili kupata mada.

Unda Mkakati wa Utekelezaji Wenye Nguvu

Ukiwa na imani aliyokuita nayo Mungu ili kuhubiri, pitia matokeo yako ili kutambua nguvu za kuhubiri kwako. Katika mchakato wa kukutana na watu wa utafiti wetu, tunakusudia kupata "ubora usio wa kawaida" kwa kila mhubiri, kama vile katika lolote kati ya yafuatayo: uhalisia, uwazi, shauku, ujasiri, ubunifu, utendekaji katika utekelezaji, uelewekaji, nguvu katika unenaji, umakini wa akili, mtindo wa ushirikishwaji, matumizi ya lugha, ukweli katika ufupi, uelezaji visa, kuchokoza mawazo, maono, au hekima. Hata kama huna timu ya kukupatia ushauri, rafiki yako unayemwamini anaweza akawa msaada mkubwa katika kukuchambulia maeneo ya msingi ambayo una nguvu nayo. Ijapokuwa waweza ukakazia mkakati wako wa utekelezaji kwenye maeneo ambayo una udhaifu nayo, mifumo ya mafanikio yetu hukuhitaji uanzie maeneo ambayo wewe una nguvu, wakati katika hali ya maombi, unaingiza lengo la badiliko katika mahubiri yako. Hapa pana sampuli kadhaa kutoka kwa wachungaji katika utafiti wetu:

• *Kujidhatiti kwenye uwezo wangu usio wa kawaida wa kueleza visa, nitaongeza bidii zaidi kuongeza simulizi kama sehemu muhimu ya mahubiri yangu au kama kitu cha kuongezea nguvu.*

• *Kujidhatiti kwenye uwezo wangu usio wa kawaida wa kuelewesha mambo na kuchokoza fikira, nitajitahidi kutumia uwezo huo siyo tu kufafanua Maandiko, bali pia katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo wasikilizaji wangu wenye njaa ya kukua wanayahitaji.*

• *Kujidhatiti kwenye uwezo wangu usio wa kawaida wa kufikiri na uelewa mwepesi, nitaendelea kutoa muhtasari kudumisha uwazi ambao wengi wanapendezwa nao—lakini pia nitajitahidi kuingiza mkondo wa kimpangilio kwa maudhui ya mahubiri yangu. Hili litaongeza nguvu na usikivu wa wasikilizaji wanaofikiri na kujifunza kitofauti na nifanyavyo mimi.*

Jikabidhi Kwa uangalizi Utakaokusaidia

Turudi kwenye mfano wa kudhibiti ulaji tena. Kama mtu atapima mizani mara moja kila juma, kuna uwezekano kwake kufikia lengo. Waalimu binafsi "makocha" na waangalizi wa uzito wa mwili wako husaidia matokeo. Kupata "makocha" wa kuhubiri kwaweza kuonekana kama taabu kubwa mno kwa wachungaji wapendao kujitenga, lakini hatua hii ni muhimu mno. Wachungaji hao katika utafiti wetu ambao mahubiri yao yamekuwa na matokeo wamejiweka chini ya uangalizi wa timu au mwenzi, wanayesaidiana kila moja na mwenziwe katika mchakato wa mabadiliko.

Hivyo mtafute mhubiri mwingine awe mwangalizi mwelekezi wako. Panga vipindi vya kubadilishana dondoo za mahubiri, hata kama ni lazima muunganike kupitia barua pepe, na mjidhatiti kuombeana nguvu ya matokeo ya mahubiri ya kila moja. Pia tafuta kundi la wachungaji wa kukutana kwa mazungumzo kuhusu kuhubiri maswala ya mambo madogo-madogo ya Kitheolojia yanayowazunguka katika safari yenu. Kwa mfano mchungaji aliyeanza majukumu yake hivi karibuni alisema hivi, "Achana na hilo! Huwezi kuwa mchungaji peke yako katika eneo lako unayemfuata Kristo…hii ni kazi ya ufalme. Je na wewe umo?"

Waweza kuwa bado wajiuliza, "je *una hakika* hakuna kilicho rahisi zaidi ya hiki? Hata hivyo ninamtumaini Roho Mtakatifu kuifanya kazi ya Mungu kwa lolote nilitoalo madhabahuni." Lakini kabla hujaamua umeridhika na mwelekeo huu, jiulize mwenyewe, "je nimeshafanya vyote viwezekanavyo kufanyika katika vipawa na karama alizonipa Mungu?" Baada ya miezi minne ya utimizaji wa mkakati wa utekelezaji, mshiriki mojawapo aliandika barua pepe ujumbe huu: "Nimekuwa nikihubiri kwa jinsi hii kwa muda mrefu. Kubadilika kumekuwa changamoto nzito, lakini mwishowe ilinigonga —kwani huwa nawaagiza watu wabadilike kila juma."

LORI CARRELL *ni profesa wa mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Wisconsin-Oshkosh. Mwanamke huyo anaanza hatua mpya ya utafiti unaohusisha mafunzo ya mawasiliano ya wachungaji* na *wasikilizaji. Toleo hili ni la saba, katika mfululizo wa matokeo kutoka utafiti wa Kituo cha Ubora wa Uongozi wa Washirika, Rev! Wanaojiunga wanaweza kuona matoleo yaliyopita katika maktaba ya "the back-issue" katika Rev.org.*

Copyright © 2007-2014 by Jonathan Menn. All rights reserved.

MWANDISHI

Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada ya kwanza elimu ya siasa (B.A. in political science) kutoka Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, ambapo alitunukiwa shahada ya heshima kutokana na kufaulu kwa viwango vya juu, mnamo mwaka wa 1974, akajumuika na Phi Beta Kappa ambayo ni taasisi ya heshima katika kijamii. Baadae akapata J.D. ambayo ni shahada ya juu ya sheria kutoka Shule ya sheria, Cornell magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akajumuishwa kwenye "Order of the Coif legal honor society" ambayo ni taasisi inayoheshimika katika jamii inayofanya kazi za kisheria. Akaitumia miaka 28 iliyofuata akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye kama mmiliki mwenza wa Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Akawa muaminio na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu (Master of Divinity) katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya mwaka 2007 – 2013 alikuwa mkurugenzi wa Afrika Masahariki wa huduma ya "Equipping Pastors International (EPI)" Na sasa Jonathan ni mkurugenzi wa huduma ya kuwawezesha viongozi wa kanisa Afrika Mashariki "Equipping Church Leaders East Africa (ECLEA)": **www.eclea.net.** Kwa ujumla, kazi zake za mafundisho aliyoandika ya masomo ya bibilia, yanapatikana hupatikana: **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.